BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA NANE

Kikao cha Tisa – Tarehe 4 Februari, 2010

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):

Hati ya Nyongeza ya Makisio ya Matumizi Na. 1 ya Mwaka 2009/2010 [*The Supplementary Estimates of Expenditure No. 1 of 2009/2010*].

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED – KIONGOZI WA UPINZANI BUNGENI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika kipindi kirefu kidogo tumeshuhudia Waandishi wengi wa Habari katika Bara la Afrika na sehemu nyingine mbalimbali wanaofuatilia mambo mazito ya nchi huwa wanapata misukosuko.

Je, huu msukosuko alioupata Jerry Muro, si sehemu ya misukosuko hiyo wanayoipata waandishi wengine hapa duniani?

NAIBU SPIKA: Bahati yako haijaingia Mahakamani, Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu tafadhali!

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, lingekuwa limekwenda mahakamani jibu lingekuwa rahisi kweli! *(Kicheko)*

Labda niseme kwanza kwamba binadamu alivyoumbwa ni kiumbe mwenye upungufu mwingi tu hata kama angekuwa ana sifa nyingine zote lakini tukubali vilevile kwamba kutakuwa na mambo ambayo una mapungufu nayo. Waziri Mkuu anayo, Hamad Rashid Mohamed anayo na kwa hiyo waandishi wa habari vilevile wana upungufu wao kama binadamu na ndiyo maana Sheria, Kanuni na taratibu zimewekwa ili kutusaidia tuweze kuongoza mambo kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na taratibu.

Sasa yaliyompata Jerry Muro tuseme tu kwamba kama binadamu na kama mtumishi mwingine yeyote ni jambo ambalo linawezekana kabisa, yale yanayotuhumiwa dhidi yake yanawezekana kuwepo lakini yanawezekana vilevile yasiwepo ndiyo maana inabidi uchunguzi ufanyike tena wa kina ili kuweza kubaini ukweli wa yale wanayomtuhumu ni kiasi gani yana ukweli na kiasi gani si kweli. Tatizo ninalolipata Mheshimiwa Hamad ni pengine namna jambo hili lilivyoanza kushughulikiwa, kwa sababu tumekimbilia kwenye vyombo vya habari sisi tunaochunguza na yeye kama mtuhumiwa amekwenda kwenye vyombo vya habari na yeye anavitumia. Kwa hiyo, sasa ujumbe tunaowapelekea wananchi kwa ujumla unaweza ukatuchanganya sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi rai yangu ni kwamba jambo hili lifanyeni kama mnavyofanya chunguzi nyingine zozote, mtakapofikia mwisho itajulikana kama ni kesi ya kwenda mahakamani au hapana!

MHE. HAMAD R. MOHAMED – KIONGOZI WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo huwezi kutumia nafasi yako ukahakikisha hili jambo linafika Mahakamani ili kuondokana na kuandikwa andikwa kila wakati?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Hamad kwamba kwa kauli ambayo nimeshaipata baada ya kuzungumza na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani na Inspekta Jenerali wa Polisi *(IGP*), nimehakikishiwa kwamba jambo hili wataliharakisha kwani na mimi sipendi liendelee kwa sababu litaanza kuleta hisia ambazo wakati mwingine hazina msingi sana. Kwa hiyo, nadhani tutajitahidi ili tuweze kulimaliza haraka.

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Waziri Mkuu, hivi sasa kuna Mashirika na Taasisi nyingi za Serikali ambazo zimekuwa zikijiendesha bila Bodi ya kuzisimamia, miongoni mwa Taasisi hizo ni Shirika la Magazeti ya Serikali yaani *Tanzania Standard Newspapers* mchapishaji wa magazeti ya *Daily News* na Habari leo. Tangu mwezi Mei, mwaka jana taasisi hii muhimu kwa Serikali imekuwa ikijiendesha bila kuwa na Bodi ya kuisimamia wala Mtendaji Mkuu wa kuisimamia.

Je, Serikali inasema nini kuhusu mwenendo huu na endapo kutatokea tatizo hasa matumizi mabaya ya pesa katika kipindi hiki ni nani awajibike? Menejimenti ya Tanzania *Standard Newspapers* au Serikali Kuu yenyewe?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Lembeli, Mbunge wa Jimbo la Kahama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikubali kwamba ni kweli kumekuwa kidogo na kuchelewa katika jambo hili lakini linashughulikiwa na mimi nina hakika ndani ya muda si mrefu tutakuwa tumelimaliza matatizo ya hapa na pale katika kujaribu kutengeneza uongozi ambao tunadhani utatusaidia kuongoza vizuri hivi vyombo. *(Makofi)*

Lakini kwa wakati huu, kupitia Wizara tunajitahidi sana kuhakikisha kwamba mambo yanakwenda vizuri lakini hata kama itatokea kwamba kuna kasoro zimejitokeza hapa na pale bahati nzuri iko menejimenti pale hata kama si mtendaji kamilifu katika kimojawapo cha chombo hicho lakini bado ni mtendaji. Kwa hiyo, pale itakapoonekana yeye amesababisha upungufu huo ni dhahiri hatua zinazotakiwa zitachukuliwa lakini nataka nimhakikishie kwamba tunalijua na ninafikiri sasa hivi tuko karibu kulimalizia.

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Waziri Mkuu, zipo Taasisi nyingi ambazo zimekuwa hazina Bodi na kwa muda mrefu, sasa sijui unasema nini kuhusu mwenendo huu wa Serikali wa kutokuteua Bodi kila inapolazimika?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, swali limekuwa kidogo jumla maana ukisema vyombo vingi napata tatizo. Lkini inawezekana katika baadhi ya vyombo hivi pengine hatujakamilisha uteuzi lakini kama nilivyosema si kwamba shughuli haziendelei lakini tutajitahidi basi tuhakikishe kwamba kila Wizara ihimizwe ili iweze kukamilisha hilo zoezi mapema iwezekanavyo kama wote mnavyojua Bodi ndiyo chombo muhimu kwa hiyo ni dhahiri kabisa lazima Bodi hizo ziwepo na tutalisukuma ili liweze kufanyiwa kazi haraka. *(Makofi)*

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwa Tanzania bado haijaridhia uraia wa nchi mbili na kwa kuwa Tanzania wapo watu kutoka nchi za jirani wanaoishi hapa kwa muda mrefu na wengine wana makazi ya kudumu.

Na kwa kuwa zipo fununu kwamba watu hao huwa wamo katika madaftari ya kupiga kura Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar na pia kule Zanzibar baadhi yao wamepata *ZAN ID*. Na kwa kuwa baadhi yao wameonekana wakipiga kura kwa mfano uchaguzi wa *Mozambique* uliofanyika hivi karibuni.

Je, Serikali haioni hilo ni kosa kubwa na inatoa tamko gani kuhusu suala hilo?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali hatujatunga Sheria kuhusiana na uraia wa nchi mbili ni jambo ambalo limechukua muda mrefu kidogo lakini kwa sababu jambo lenyewe linahitaji uchunguzi wa kina na kwa mfumo ulivyo kwa sasa ni kwamba ukitaka kuingiza katika mfumo huo ni lazima nchi hiyo nyingine ambayo mnataka kuingiza katika maelewano hayo yenyewe kwanza iwe na mfumo wa namna hiyo na kwa taarifa nilizonazo mpaka sasa kusema kweli ni mataifa makubwa zaidi ndiyo yako kwenye mfumo huo kwa mfano Canada, Uingereza, Marekani na India. Nchi nyingi duniani bado zinatumia uraia mmoja tu lakini tutakapokuwa

tumefikia wakati tukaamua jambo hili basi tutazingatia maslahi mapana kwa maana ya nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Sasa kuhusu swali ulilouliza juu ya wananchi wenye asilia ya Msumbiji kwa maelezo yako unasema hawa wako kwenye daftari la Wapiga kura Tanzania Bara na wako kwenye Daftari la Wapiga Kura waliopo huko Visiwani na kwamba wanapiga kura kwa maana ya uchaguzi hapa ndani, sasa sina hakika maana hukusema kwa uhakika kama ni raia au si raia. Kama ni raia wa Tanzania hata kama ametokea Msumbiji halina tatizo lakini kama siyo raia na tuna uhakika kwamba hawa si raia basi asiye raia haruhusiwi kupiga kura hapa nchini, huo ndiyo msimamo wa nchi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa hili pengine nitamwomba Waziri Masha ashirikiane na wewe tuweze kuona kama kweli hili unalolieleza lipo na hatua zinazotakiwa zichukuliwe ili kurekebisha haraka iwezekanavyo. (*Makofi*)

MHE. MOHAMED HABIBU JUMA MNYAA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa maana hiyo huoni kwamba ipo haja sasa mbali ya Mheshimiwa Masha kushirikiana na mimi kwa sababu wako wananchi ambao wanazo hizo taarifa ambao wako Dar es Salaam, Zanzibar na kadhalika. Huoni kwamba ipo haja sasa Serikali kufanya uchunguzi maalum ili wale walioko katika daftari watolewe ili katika chaguzi zetu isiwe tunachaguliwa viongozi wetu na watu wa nchi za jirani?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, sina hakika kama tumetofautiana sana nadhani anachosema Mheshimiwa Mnyaa na nilichokisema kusema kweli tunasema yaleyale, kikubwa hapa ni uchunguzi na tufanye uchunguzi haraka kwa hiyo kama wako Watanzania ambao wana taarifa za uhakika kiasi hicho nataka niwasihi sana wawasilishe taarifa hizo ama kwenye Idara ya Uhamiaji haraka iwezekanavyo au hata moja kwa moja kupitia kwa Mheshimiwa Waziri na wewe mwenyewe ili tuweze kuona ni wangapi na kwa kweli waweze kuondolewa kwa sababu si haki yao kupiga kura hapa. (*Makofi*)

MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Swali kwa Waziri Mkuu na ninaomba kunukuu.

Kwa kuwa, Mkoa wa Kigoma kuna Jimbo la Kigoma Kaskazini ambako kuna mradi wa ujenzi wa barabara kuu kuanzia Mwandiga mpaka Manyovu yenye kilomita 60 kwa kweli wananchi wanashukuru sana Chama cha Mapinduzi kwa kuweza kutimiza ahadi yake ambayo wameitimiza mpaka sasa hivi barabara inaendelea na wananchi wanashukuru sana lakini kuna kasoro.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tarehe 29/7/2008 wananchi walipata barua kutoka kwa meneja wa *TANROADS* Kigoma yenye kumbukumbu namba *TANROADSKG/R10/95/13,* barua hizo zilikwenda kwa Mkuu wa Mkoa, zikaenda kwa Mkuu wa Wilaya Kasulu na Kigoma, zikaenda kwa Mkuu wa Polisi, zikaenda kwa

Mkurugenzi Mtendaji Kigoma, pamoja na Mtendaji wa Kijiji Bitale ….. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Uliza swali sasa!

MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini kwa kuwa wale wananchi walitii Sheria wakabomoa nyumba zao, walivyobomoa nyumba zao mimi nikaja nikakuuliza swali hapa Bunge mwaka 2008 wakati huohuo ukasema kuwa inatakiwa wale wananchi ambao wamewekewa nyumba zao X waweze kulipwa, lakini wale ambao walitii Sheria wakabomoa nyumba zao kabla tathmini haijatolewa wanaambiwa kuwa hawawezi wakalipwa kwani zile nyumba zao ni vifusi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa wao walitii Sheria ya kubomoa nyumba zao mapema kabisa kabla ya tamko lako, naiomba Serikali iweze kuchukua tathmini ya nyumba mojawapo ya wale wananchi waweze kulipwa nyumba hizo.

Na kwa kuwa, kuna wananchi ambao waliwekewa nyumba zao X na kulikuwa na nyumba ambazo zilikuwa na kizuizi kwa ajili ya kutengeneza barabara wakalipwa kwanza na kwa kuwa kuna wananchi wengine ambao bado ……..(*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa siyo kwamba wanakushangilia bali wanataka uulize swali ni nini tatizo. Sasa uliza swali!

MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA: Na kwa kuwa kuna wengine waliwekewa nyumba zao X walishalipwa,

WAJUMBE: Uliza swali!

NAIBU SPIKA: Kwa hiyo swali ni nini?

MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA: Je, kwa kuwa kuna wale wengine ambao waliwekewa nyumba zao X na mpaka sasa hivi hawajalipwa na kila wakifuatilia kwa Meneja wa *TANROADS* analipwa mtu mmojammoja anaweza kulipwa mtu mmoja kutoka hapa Bungeni na mwingine akalipwa kutoka hapa mpaka kule *CRDB* wanakwenda wanaruka nyumba hadi nyumba.

Je, wale wengine ambao bado hawajalipwa watalipwa lini?

NAIBU SPIKA: Hilo wala siyo swali ni hotuba kubwa kabisa unanukuliwa wewe mwenyewe, Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu tafadhali!

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, eeeh! Katibu wa Bunge, Dr. Kashililah itabidi atupeleke semina kidogo. Mimi nafikiri nimemuelewa nadhani anachosema ni kwamba barabara ya Mwandiga - Manyovu pamoja na ubora wake na pamoja na nia njema ya Serikali wako wananchi pale ambao hawajalipwa fidia kulingana na Sheria au taratibu za nchi.

Mama nitajitahidi na nitalifuatilia jambo hili kwa sababu ungekuwa umenidokeza ningeweza kulifanyia kazi vizuri sana. Lakini tutalifuatilia kwa karibu tuone nani bado na kwa nini bado ili waweze kulipwa. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Swali lilikuwa refu sana lakini ni haki yako! Sasa swali la nyongeza fupi sana siyo kwa kuwa nyingi sana.

MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, sawa! Kwa kuwa kuna wale wengine wanaoambiwa kuwa nyumba zao zilikuwa ni kifusi na walikuwa wametii Sheria ya kubomoa nyumba zao mapema lakini wanaambiwa ni vifusi je watafanya tathmini ya kuchukua nyumba mojawapo ili na wengine waweze kulipwa na wale wengine ambao hawajalipwa?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi si mtaalamu wa mambo haya kwa hiyo siwezi nikalijibu hilo swali lakini ninasema hivi, acha tufanye uchunguzi tuone nyumba zilizobomolewa kabla ya uthamini kufanyika na zile ambazo zimefanywa baada ya uthamini kufanyika, mimi nina hakika lazima kutakuwa na mfumo wa namna moja au nyingine wa kuweza kuwasaidia Watanzania hawa hata kama si fidia basi angalau kifuta machozi cha namna fulani, lakini lazima utakuwepo utaratibu tu.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Nkayamba maswali huwa yanakuwa mafupi sana. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Yahya Kassim Issa.

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni utaratibu ambao mara nyingi tunafanya katika Bunge letu Tukufu hili wa kuja Viongozi wetu kama Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kulihutubia Bunge hili. Na kwa kuwa Rais wetu aliwahi kuja hapa na mategemeo yetu makubwa ilikuwa ni kwamba kupata yale ambayo alihutubia na kama kumkinika pia kuweza kujadili katika Bunge letu Tukufu kutokana na maudhui mazuri yaliyojitokeza kutokana na hasa wakati ule ambapo palikuwa na mtikisiko fulani. *(Makofi)*

Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu unaweza kutueleza sababu za msingi kwamba hata kufikia leo hotuba ile hatujatolewa na si kawaida ya Bunge letu hili Tukufu kuwa hivyo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, hilo ni swali la Kanuni lakini kama unaweza kujibu, jibu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Yahya Kassim Issa hilo ni swali gumu. Ukiniuliza mimi sasa hivi kwa kweli siwezi kusema. Haikutolewa kwa sababu ni jukumu la Ofisi ya Rais tena Ofisi binafsi ya Rais sana sana ninachoweza kuahidi tu ni kwamba kama bado hotuba ile inahitajika mpaka leo labda niwaulize tu kwamba jamani mbona hamjatoa hiyo hotuba? Kassim anaihitaji huku hebu ileteni. Hilo naweza kufanya.

MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI: Mheshimiwa Waziri Mkuu suala la mpaka kati ya Malawi na Tanzania katika Ziwa Nyasa limekuwa tete kwa muda mrefu

sana. Je, hivi tatizo hili ni kubwa vipi na kwa kiasi kipi ambapo Serikali imeshindwa kulitatua?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, anachosema Mheshimiwa Mwalyosi ni kweli kwamba kumekuwa na mvutano au tuite ubishi kati ya pande moja yaani upande wa Malawi na sisi upande wa pili juu ya mpaka hasa uko wapi ni katikati ya Ziwa Nyasa au ni pembeni mwa ziwa Nyasa kwa upande wa Tanzania?

Hili suala la muda mrefu kidogo na lina historia ndefu lakini ni jambo linalozungumzika kwa sababu taratibu za kimataifa zipo na litamazika tu.

Nilichofanya baada ya kuona maazimio yale ya juzi yamezua hili jambo kwa nguvu sana tayari nimekwishaandika barua kupeleka kwa Katibu Mkuu Kiongozi ili aweze kuanzisha mazungumzo ya kitaalamu ili tuone namna tutakavyoweza kulisukuma jambo hili na bahati nzuri Rais wa Malawi sasa ndiye Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika kwa hiyo nadhani itasaidia kidogo kuweza kuliharakisha kidogo.

MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI: Mheshimiwa Waziri Mkuu nashukuru umeanza kulijibu swali nililotaka kuuliza lakini nilitaka kusema je, hali hii au tatizo hili linaweza kweli likazuia masuala mengine ya maendeleo ambayo yanashirikisha nchi nyingi katika maeneo hayo inaweza ikazuia tatizo hili la mpaka au mambo mengine yanaweza yakaendelea?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri mambo yote ni mazito, shughuli zile za maendeleo kwa maslahi ya nchi hizi hasa Tanzania ni muhimu, suala vilevile la kuwa na uhakika na mpaka nalo ni muhimu vilevile.

Kwa hiyo, yote ni mambo mazito na inabidi yote tuyatazame kwa maslahi mapana, ndiyo maana nilitaka kuitumia nafasi hii kulishukuru sana Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninyi Wabunge pamoja na kuona uzito wa mambo yote mawili lakini katika maazimio haya mwelekeo ni mzuri kwamba mtaridhia jambo hili kwa maana ya maslahi ya maendeleo ya hivi sasa lakini wakati uleule Serikali sasa lazima tuanze mazungumzo juu ya hili lingine lisiendelee kuwa ni kikwazo katika taratibu zetu ushirikiano.

MHE. ALHAJI DR. JUMA A. NGASONGWA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nikuulize kwamba kwa kuwa sifa au vigezo muhimu vya kugawa eneo la kiutawala nchini mwetu ni idadi ya watu na ukubwa wa eneo au jiografia ya eneo husika. Na kwa kuwa Wilaya ya Ulanga ina eneo la kilomita za mraba 25,640 eneo ambalo linapita kwa ukubwa Mkoa wa Kilimanjaro ambao una eneo la mraba la kilomita za mraba 13250 lakini pia hata Mtwara ambayo ina kilomita 16,710 na Mkoa wa Mwanza ambao una eneo la kilomita 19,683…..

NAIBU SPIKA: Swali tafadhali!

MHE. ALHAJI DK. JUMA A. NGASONGWA: Je, inawezekana sasa kufikiria kuigawa Ulanga katika wilaya mbili za Mahenge na Ulanga?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe maelezo mafupi sana kuhusu swali la Mheshimiwa Ngasongwa.

Ni kweli alivyosema vipo vigezo vingi na alivyovitaja ni baadhi tu kwa maana ya ukubwa na idadi ya watu na hapa ni vizuri tukalisema kwa sababu idadi ya watu inayozungumzwa hapa kwamba ili uweze kupata Wilaya kugawanyika mara mbili au zaidi ni lazima mgawanyo wake ukupe angalau idadi ya watu 250,000 kiwango cha chini kwa kila Wilaya itakayokuwa imepatikana na ni vizuri vile vile ikajulikana kwamba kimakadirio tu ni kwamba ili Wilaya iweze kusimamiwa na kutawalika vizuri, unahitaji angalau kilomita za mraba kati ya 5,000; 6,000 au 7,000 ili kumwezesha Mkuu wa Wilaya kufanya kazi zake vizuri.

Kwa hiyo, ni kweli kwa maana ya Ulanga na kwa maana ya Vigezo hivyo viwili kama vipo na kama alivyoeleza inaweza ikafikiriwa kwamba inaweza ikachukuliwa hivyo, lakini vipo vigezo vingine vingi.

Lakini la pili ni kwamba sisi hatuanzishi au hatufikirii tu kugawa Wilaya mpaka kwanza wadau wahusika wameona umuhimu wa jambo hilo na kuleta maombi rasmi Serikalini. Kwa hiyo, kama Ulanga wameomba tutakuwa tumeliangalia au tutaliangalia sasa kwa sababu sina maamuzi hapa ya haraka haraka wala maelezo ya haraka haraka labda nimsihi tu kwamba tuwasiliane baadaye ili nione kama kweli wamefanya hiyo kazi na tuone Serikali mpaka sasa imenong'ona nini na mimi nitamnong'oneza, inaweza pengine ikasaidia huko kwenye Jimbo unajua tena enzi hizi ni taabu kidogo ukipata kawilaya si haba. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Nafikiri Profesa unangoja kunong'onezwa huko, sasa ni zamu ya Mheshimiwa Archt. Fuya G. Kimbita.

MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kutokana na mtikisiko wa uchumi uliotokea na Mheshimiwa Rais kuchukua hatua kusaidia katika yale mazao makuu ya biashara hapa nchini na ninaamini wenzetu wa Pamba tayari wameshanufaika.

Je, sisi wakulima wa Kahawa maombi yetu yamefikia wapi hususani Chama cha Kikuu cha Ushirika cha Mkoani Kilimanjaro *(KNCU)?*

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, analolisema Mheshimiwa Kimbita ni kweli Serikali imeshatoa karibu bilioni 20 tayari kwa ajili ya zao la Pamba kupitia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Lakini kwa upande wa Kahawa ni kweli tumechelewa, tumechelewa kwa sababu baada ya tamko la Serikali kutolewa katika mfumo ule wa kunusuru yale maeneo ambayo yaliathirika sana kutokana na mtikisiko wa kiuchumi maelezo yaliyopatikana wakati huo yalichanganya maana tulilenga Vyama vya Ushirika lakini na watu binafsi vilevile.

Lakini katika maelezo yaliyotolewa, waliweka na mambo mengine ambayo kusema kweli ni madeni ya nyuma ambayo hayana uhusiano na mtikisiko wa kichumi kwa hiyo ikalazimika sasa ufanywe tena uchambuzi wa kina ili kujiridhisha na yale madeni ambayo ni sahihi na ambayo yanalingana na mtikisiko na madai mengine ya siku za nyuma kwa hiyo zoezi hilo linaendelea. Kwa upande wa Kagera, nadhani tumeshaanza tayari. Kwa hiyo, nina hakika hata upande wa Kahawa kama tutakuwa tumekamilisha sijacheki na Mzee Wassira hapa lakini nina hakika zoezi linakwenda vizuri, tukikamilisha tu tutazilipa, maana fedha zipo.

MHE. TATU MUSA NTIMIZI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Swali kwa Waziri Mkuu usafiri wa reli ya Kati umekuwa na matatizo, Wananchi wanafahamu na Serikali inafahamu na gharama za kuiweka sawa ili treni ianze kwenda zinafahamika. Mwaka juzi lilitokea tatizo hilo lakini wananchi wakaanza kusafiri kutoka Dodoma kwenda Magharibi, imekuwaje safari hii haiwezekani?

Mheshimiwa Naibu Spika, usafiri wa mabasi kutoka Dar es Salaam mpaka Mpanda, Tabora, Kigoma gharama yake imekuwa ni mara nne zaidi. Je, huoni wananchi katika kipindi hiki kigumu cha wakati wa njaa na mafuriko na bado washindwe kusafiri kutoka maeneo wanayotoka mpaka kufika sehemu hizo? Naomba ufafanuzi. *(Makofi)*

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla tukubali tu kwamba, anayoeleza Dada Tatu Mussa Ntimizi ni kweli, liko tatizo kubwa kwenye Reli ya Kati.

Kama wote tunavyojua hata bila kuzungumzia mafuriko haya, imekuwa na matatizo ya uendeshaji na kwa ujumla. Hata ufanisi katika utoaji wa huduma zake, na matokeo yake kwa kweli si mazuri sana; yameathiri sana mambo mengi na yamesababisha vile vile gharama kupanda, maana hata magari sasa nauli zake si kama zilivyokuwa wakati wa mazingira ya kawaida. Kwa hiyo, hili la mafuriko limeongeza tu donda juu ya donda.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba, kwa ujumla wake tatizo hili sasa hivi tunaliangalia kwa upana zaidi. Tuna kazi ya haraka ya kufanya kwa sasa, lakini tuna kazi ya muda ujao wa kati na muda mrefu katika kujaribu kuboresha huduma ya shirika letu la reli, lakini zaidi miundombinu yake.

Kwa hiyo, labda tu nimwombe Dada Tatu Musa Ntimizi kwamba, pengine sitakuwa na jibu la moja kwa moja katika vipengele vyote lakini nimhakikishie tu kwamba, tumeanza kulifanyia kazi hili shirika letu la reli, ili tujaribu kuzingatia

matatizo yote kwa upana wake na tuone ni hatua zipi tunaweza tukazichukua angalau kusaidia kupunguza kidogo adha ambayo sasa imejitokeza. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu kimemalizika na tumeweza kuwapata wachangiaji tisa.

Mkiuliza maswali ya moja kwa moja tena mafupi, basi mnaweza kuwa wengi zaidi. Lakini naomba kwa niaba yenu nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa majibu yake ya utulivu ya uhakika na nafikiri wote mnaridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakupongeza sana. (*Makofi*)

MASWALI NA MAJIBU

Na. 93

Ujenzi wa Maabara kwenye Sekondari ya Bukwimba.

MHE. JAMES P. MUSALIKA aliuliza:-

Kwa kuwa katika mwaka wa fedha 2007/08 Serikali ilitoa Shilingi Milioni Kumi na Nne (14,000,000/=) chini ya Mpango wa MMES kwa ajili ya ujenzi wa Maabara lakini katika taarifa ya Mkaguzi wa Ndani wa Halmashauri ya Geita inaonesha kuwa fedha hizo zilifanyiwa ubadhirifu ambao ulishatolewa taarifa kwa Waziri wa Fedha na Uchumi tangu mwezi Julai, 2009 na akaahidi kupeleka wataalam wake kuchunguza jambo hilo:-

(a) Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Bukwimba juu ya hatma ya ujenzi wa Maabara?

(b) Je, Serikali inafahamu kuwa timu mbili za wataalam zilizotumwa kuchunguza tatizo hilo, wamefanya uchunguzi wao bila kuhusishwa *WDC* wa Bodi ya Shule hiyo hivyo kuweka mashaka juu ya usahihi wa taarifa ya uchunguzi wao?

NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Philipo Musalika, Mbunge wa Nyang'wale, kama ifuatavyo.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali ilitoa shilingi 14,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa maabara katika shule ya Sekondari Bukwimba iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Geita. Fedha hizo zilipelekwa shuleni kwa ajili ya ujenzi wa Maabara hiyo kwa usimamizi wa Bodi ya shule.

Taarifa iliyotolewa na Mkaguzi wa Ndani wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita ilibaini kuwa fedha zilizotolewa zilitumika kwa shughuli nyingine za kawaida nje ya ujenzi wa maabara hivyo kufanya ujenzi wa maabara kutokamilika.

Aidha, ulibainika upungufu katika utunzaji wa kumbukumbu kwani hakukuwepo nyaraka muhimu katika daftari la fedha ambalo lingeweza kuonesha kumbukumbu za maingizo na matumizi ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Mkaguzi wa Ndani ilibainisha kutokuwepo hati za malipo ya Shilingi 9,081,700/= kwa malipo yaliyofanyika kati ya mwezi Desemba, 2007 na Aprili, 2008. Mchakato wa manunuzi kama ulivyoanishwa katika taratibu za manunuzi kwa shule za Sekondari mwaka 2004-2009 unawataka Wakuu wa Shule za Sekondari kuhakikisha malipo yanaidhinishwa na Bodi ya Shule.

Mwalimu Mkuu wa shule hii alijichukulia madaraka ya kufanya malipo bila kushirikisha Bodi yake. Aidha uongozi wa shule ulitumia fedha hizo kununua vifaa vya kufundishia na michezo ambavyo viligharimu shilingi 633,000/= na Wajumbe wa Bodi ya Shule kutopatiwa taarifa ya fedha za ujenzi ikiwa ni pamoja na kutoandikwa muhutasari wa vikao.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu timu za wataalamu zilizochunguza bila kuhusisha Bodi ya shule, Ofisi yangu inafuatilia suala hilo. Namwomba Mheshimiwa Mbunge anipatie muda. Hivi sasa katibu Tawala Mkoa wa Mwanza ameunda timu ya wataalamu ambayo inafuatilia suala hilo katika Wilaya ya Geita na taarifa itatolewa.

MHE. JAMES P. MUSALIKA: Mheshimiwa Naibu Spika nashukuru, lakini kabla sijauliza maswali madogo mawili ya nyongeza napenda kutoa masikitiko yangu kwamba, swali hili limejibiwa na Wizara tofauti.

Pesa za MMES huwa zinatolewa na Hazina kwenda Hazina ndogo ambayo ni Mwanza kwa upande wa Kanda ya Ziwa na pesa hizi zimefanyiwa ubadhirifu kwa tuhuma zilizopo na Maafisa wa Hazina ndogo Mwanza na Mkuu wa Shule hiyo Paschal Machibya, na mimi mwenyewe niliishawasiliana na Waziri lakini leo wameulizwa Halmashauri ambao hata Watendaji nilikuwa kule siku hizi mbili, walikuwa wanashangaa suala hilo hawalijui, naomba sasa.

(a) Je, Serikali sasa inaweza ikarudisha swali hili ili Bunge lijalo, Bunge la 19 lijibiwe na Wizara ya Fedha na Uchumi kwa kuwa, ndiyo watu wanaotuhumiwa na suala

hili na wala sio Waziri Mkuu na watoto yatima ya maabara ile itajengwaje kabla hatujamaliza Bunge hili?

(b) Waziri Mkuu sasa ili anisaidie anaweza akamwagiza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali akafanye *Special Audit* (Ukaguzi Maalum) katika Ofisi ndogo ya Hazina, Mwanza kwa sababu yaapo malalamiko mengi kwamba, Shule za Sekondari za MMES hazikufanya kazi yake. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Hilo ni swali au kugombana! Haya Mheshimiwa Naibu Waziri. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa James Philipo Musalika, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nikiri kwamba, naelewa ni kwanini Mheshimiwa Mbunge anaiweka kama anavyoiweka. Ni kweli kwamba, hapa kuna taratibu zimekiukwa na ni kweli kabisa kwamba, utaratibu haukufuatwa kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge na siwezi kusimama hapa na kusema kwamba nitetee hali ile, ile si hali ambayo inaridhisha na mimi napenda nimpongeze Mheshimiwa Musalika kwamba, amelifuatilia jambo hili kwa karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninavyozungumza sasa hivi, nimezungumza na Katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza na kufuatilia kwa karibu kujua kwamba, wamefikia wapi kuhusiana na jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo mawili yanayozungumzwa, kwanza Mwalimu Paschal Machibya, amehamishwa yuko Wilaya ya Nzega.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, jibu wala hao watu usiwasikilize. *(Kicheko)*

NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo nashukuru sana. Na huyu Mkaguzi wa Ndani anayezungumzwa hapa naye pia amehama hayuko pale. Kwa hiyo, nimetoa maelekezo kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, huyu *RAS* aliyeko Mkoa wa Mwanza afuatilie kwa karibu sana na kupitia hii timu ambayo ameunda atwambie nini kilichotokea, kwa sababu kinachozungumzwa hapa ni kwamba, iko timu iliyopelekwa pale na ambayo Mheshimiwa Mbunge anai-*doubt* pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Mbunge ameuliza swali hapa kwamba, Je, ni kwanini limeletwa TAMISEMI? Mimi ninavyofahamu kuna Serikali moja tu, Serikali ambayo inaendeshwa chini ya Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jakaya Mrisho Kikwete kwa hiyo *weather* tunajibu sisi au wanajibu watu wa hazina, Serikali ni ileile na nina hakika kwamba, majibu ninayoyatoa

hapa ni kwa niaba ya Serikali. Kwa hiyo, mimi naomba na kama Mheshimiwa Mbunge atafikiri kwamba, hatuwashirikishi wenzetu hawa wa Wizara ya Fedha, basi tutafanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kuhusiana na habari ya kumpeleka Mdhibiti Mkuu. Kilichozungumzwa hapa ni kwamba, aliyetoa taarifa hii ni Mkaguzi wa Ndani, Mkaguzi ni chombo cha ndani cha Halmashauri ambacho kinafanya viashiria na kuwaambia menejimenti kwamba, kuna hatari, kwamba hela zinakwenda vibaya, hii taarifa ndiyo iliyoripotiwa.

Ni kweli kabisa kama anavyosema Mheshimiwa Musalika, tumeiona na iko ripoti ninayo hapa, nimekuja na faili kuna matatizo ambayo yamejitokeza pale, sasa Mkaguzi wa Ndani ndiye ambaye *Controler and Auditor General (CAG)* akienda pale ni lazima kwanza aichukue ile ripoti. Mimi nakubaliana na mawazo ya Mbunge kwamba, katika hali ambayo imejitokeza hapa ni sahihi hata kuhitaji *CAG* aende pale atuambie kwamba, ni nini kilichotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ninataka niitahadharishe nyumba hii kwamba, Shilingi Milioni Kumi na Nne (14,000,000/=) hazitoshi kujenga maabara, ukitaka kujenga maabara na kuweka kemikali na vitu vyote vinavyohitajika kule ndani, unahitaji shilingi milioni arobaini (40,000,000/=) nilitaka muipate hiyo picha. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, swali lenyewe ni zito sana. Haya Mheshimiwa Slaa, huyu ni Mwenyekiti wa Kamati ya *Local Authority Accounts Committee (LAAC).*

MHE. DR. WILLBROD P. SLAA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kilichotokea katika Halmashauri ya Geita ni mambo ambayo Kamati yetu imeyaona katika maeneo mengi, fedha zinapelekwa lakini ama hazitumiki kama inavyotakiwa au wakati mwingine hata kile kilichodhaniwa kujengwa hakipo na yote haya tunayaona. Tatizo kubwa ni kwa sababu msimamizi wa kwanza ambaye ni Madiwani hawakupewa ufunguo wa kuweza kusimamia.

Je, Serikali inatoa mwongozo gani ili Madiwani wawezeshwe kusimamia fedha hizi nyingi na waweze kutafsiri taarifa nyingi za fedha ambazo kwa kweli kwa jinsi zinavyoandikwa kama hawatawezeshwa ni ngumu sana kwa Madiwani kusimamia?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana ndugu yangu Dr. Slaa, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Kamati ya *LAAC* katika kufichua mambo mbalimbali ambayo yanatokea katika halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Waheshimiwa Madiwani wakichaguliwa tu mara nyingi tunawapa semina mbalimbali ili kuwawezesha kutambua au kuwapa uelewa na kuhusu kuwapa nyenzo, Waheshimiwa Madiwani, kama Halmashauri wana madaraka kamili kabisa ya kuchukua hatua zozote ambazo wanaona kwamba, mtumishi ameenda kinyume na Sheria tatizo tulilo nalo ni kulindana. Kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge pia ni Madiwani, mimi nasema kwamba ni vyema mfanyakazi yeyote wa umma akiwa mbadhirifu wa aina yoyote, Waheshimiwa Madiwani wachukue hatua pale walipo na si kuja kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu au kwa Mama Kombani, na kusema kwamba, ahamishwe kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine, ni kiasi cha sisi wenyewe kutimiza wajibu wetu, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, tunaendelea hili swali ni zuri sana na linawahusu wote mkasimamie. (*Makofi*)

Na. 94

Ukosefu wa Hospitali ya Wilaya, Longido

MHE. MICHAEL L. LAIZER aliuliza:-

Kwa kuwa Longido ni Wilaya mojawapo ambayo haina Hospitali ya Wilaya na kusababisha wagonjwa wengi kukosa huduma:-

Je, ni lini Serikali itajenga Hospitali ya Wilaya ya Longido?

NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Wilaya ya Longido haina Hospitali ya Wilaya. Aidha, huduma za afya zilizopo zinatolewa katika vituo vya afya viwili na zahanati 18 zilizopo. Wilaya hii kwa kukosa Hospitali ya Wilaya huduma zote za rufaa zinafanyika katika Hospitali ya Mkoa wa Arusha – *Mount Meru Hospital.* Serikali ilishaliona tatizo hilo na kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Longido imeanza maandalizi ya kujenga Hospitali ya Wilaya kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Halmashauri ya Wilaya imetenga eneo la ekari 30(hekta 13) kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali.

(ii) Halmashauri inafuatilia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ili kupata ramani yenye viwango vinavyotakiwa kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya.

(iii) Mwaka 2009/2010, Halmashauri iliweka maombi maalum ya shilingi 600,000,000/= katika Bajeti ya mwaka 2009/2010 kwa ajili ya ujenzi kwa awamu ya kwanza. Hata hivyo, fedha hizi hazikupatikana. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Halmashauri ya Wilaya ya Longido imeweka fedha hizo katika mpango wa Bajeti yake kwa kuzingatia vipaumbele vya mwaka huo.

(iv) Wananchi wanaendelea kuhamasishwa katika vijiji mbalimbali ili waone umuhimu wa kuchangia ujenzi wa Hospitali ya Wilaya.

(v) Halmashauri inaandaa andiko la mradi ili kupeleka kwa wahisani mbalimbali kuomba fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha kuwa wananchi wa Longido wanapata huduma bora, vituo vya afya na zahanati zilizopo zinaendelea kuimarishwa. Vile vile kama wote tunavyokumbuka, Mheshimiwa Rais tarehe 21/01/2010 ametoa gari la kubebea wagonjwa wa Wilaya ya Longido. Hii yote ni kuhakikisha kuwa huduma bora za afya zinapatikana wakati taratibu za kujenga Hospitali ya Wilaya zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Longido kwamba Hospitali ya Wilaya itaendelea kujengwa hatua kwa hatua kadri fedha zitakavyopatikana.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naomba niulize swali moja la nyongeza, lakini kabla sijauliza naomba kupitia Bunge lako Tukufu, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutupa gari la wagonjwa katika kituo cha afya cha Engarenebo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika Bajeti iliyopita Halmashauri ya Longido wameweka kipaumbele kwenye ujenzi wa hospitali ya wilaya na wakaomba fedha hizo. Katika kipindi hiki bado wameweka kipaumbele kupata hospitali ya Wilaya.

Je, Serikali katika awamu hii ya bajeti ya 2010/2011 watatupa kipaumbele ili na sisi tupate hospitali, tusihangaike tena kwenda Mount Meru Hospital ambako ni mbali sana kwa watu ambao hawana uwezo na kizingatiwa kwamba, Longido wameadhirika sana baada ya mifugo kufa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido - kaka yangu, Ndugu yangu na Mbunge wa karibu sana na Jimbo langu la Siha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais, kwa hili gari la wagonjwa ambalo limepelekwa kule. Hili analolizungumza Mheshimiwa Mbunge, mimi mwenyewe hivi ninavyokuja Bungeni hapa nimetoka

kwenye ziara ya Mkoa wa Arusha na hali ambayo anaizungumzia Mheshimiwa Lekule Laizer ni kweli kwa sababu nimeiona hali iliyoko kule ni mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili analolisema hapa kwamba, wameingiza katika Bajeti, kwa kawaida sisi tunaheshimu sana mapendekezo ambayo yanakuja kwenye Bajeti na inapokuja kwa utaratibu ule ambao wameona kwamba ni kipaumbele, sisi kama Serikali tunapopitisha hatuna tena njia ya kuweza kuzuia hilo. Kwa hiyo, hili litaangaliwa kwa mtizamo huo kwamba, ni jambo muhimu. *(Makofi)*

Na. 95

Kuwaandaa Washiriki wa Mashindano ya Olimpiki

MHE. RICHARD M. NDASSA aliuliza:-

Kwa kuwa, wachezaji wetu mara nyingi wanaposhindwa kufanya vizuri katika mashindano ya Kimataifa kama yale ya Olimpiki yaliyofanyika China ambapo washiriki wetu walishindwa kwa kisingizio maandalizi duni; na kwa kuwa, mwaka 2012 mashindano ya Olimpiki yatafanyikia Uingereza ambapo washiriki wa nchi nyingine wameishaanza maandalizi.

Je, washiriki wetu wanaandaliwaje ili wasije kutoa kisingizio cha maandalizi duni pindi watakaposhindwa?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, wachezaji wetu mara nyingi wanaposhindwa kufanya vizuri katika mashindano ya Kimataifa hudai kwamba kushindwa kwao kunatokana na maandalizi duni. *(Makofi)*

Ili kuhakikisha kwamba wachezaji wetu na hata viongozi wao hawatoi maelezo ya kutofanya vizuri katika mashindano mbalimbali kama yale ya Olompiki yatakayofanyika nchini Uingereza mwaka 2012, yametokana na maandalizi duni, Serikali imefanya mambo yafuatayo:-

1. Imeajiri makocha wanne kutoka Cuba watakaofundisha michezo ya riadha, ngumi na judo ambao ni Adres Baro Curtis, Jorge Luis Bravo, Rajas Geovanis Hurtado Pementel na Jose Valdes Silva. Kwa kushirikiana na makocha wetu wazalendo watafanya kazi ya kuwaandaa wachezaji watakaoshiriki kwenye mashindano ya Olimpiki mwaka 2012.

2. Wachezaji wa Taifa wa zamani ambao tayari wamekwishafuzu viwango vya Kimataifa watajiunga na wenzao waliochaguliwa kuunda timu ya Taifa kufanya mazoezi na mashindano ya kitaifa na mengine ya majaribio ndani na nje ya nchi yetu.

3. Kuweka kambi ya muda mrefu kwa ajili ya maandalizi na kuinua viwango vya wachezaji ili kufikia vipimo vya kimataifa katika mashindano mbalimbali.

4. Kwa upande wa mchezo wa mbio ndefu, kuanzia mita 800 hadi marathoni tayari Jeshi la Wananchi wa Tanzania limefanya kazi nzuri ya kupeleka makocha wa mchezo huo katika mikoa ya Arusha, Manyara, Singida, Dodoma na Zanzibar kwenda kutafuta vipaji vipya.

Zoezi hilo limezaa matunda baada ya mchujo uliofanyika mara nne kwa wachezaji waliokuwa wamefanyiwa majaribio, wamepatikana jumla ya vijana 52. Vijana hao kwa sasa wamepelekwa Kambi ya Makutupora hapa Dodoma kwa mafunzo ya kijeshi na mara tu watakapomaliza mafunzo hayo wataanza rasmi mafunzo ya mchezo wa riadha kwa ajili ya maandalizi ya mashindano ya Olimpiki.

Aidha makocha wa kigeni walioajiriwa wameanza kufanya ziara katika mikoa ya Arusha na Manyara na Singida kwa madhumuni ya kuandaa utaratibu wa kuanza mashindano ya kupata wachezaji wa mchezo wa riadha watakaoungana na wenzao wa timu ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania ili kuunda timu ya Taifa itakayoshiriki mashindano ya Olimpiki mwaka 2012.

5. Wizara yangu inafanya mazungumzo na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuona uwezekano wa kuweka kambi ya wanamichezo hao ndani ya kambi ya jeshi ili hata vijana wengine waliochaguliwa kuunda timu ya Taifa wawe pamoja jambo ambalo litawajenga kinidhamu na mahudhurio ya mazoezi bila kukosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mkuu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Jenerali Davis Mwamunyange kwa hatua aliyoichukua ya kutekeleza azma ya Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Kikwete ya kufufua na kuendeleza mchezo wa riadha hapa nchini.

Napenda pia kutoa wito kwa taasisi nyingine kama vile Polisi, Magereza, Uhamiaji kuanza mchakato wa kuibua vipaji katika michezo mbalimbali ili nchi yetu iweze kupata wanamichezo bora watakaoshiriki mashindano ya kitaifa na kimataifa na hivyo kupata ushindi ambao utarudisha heshima ya nchi yetu katika medani ya michezo.

Napenda kutoa wito kwa Watanzania wote hasa Makampuni, Mashirika, wafanyabiashara na watu binafsi watakaoguswa na michezo ya riadha kukisaidia Chama cha Riadha nchini kwa hali na mali ili kukiwezesha kufanya maandalizi mazuri ya timu ya Taifa itakayoshiriki mashindano ya Olimpiki na mashindano mengine ya kimataifa kama inavyofanyika katika nchi nyingine duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda kumpongeza Mheshimwa Ndassa kwa swali lake ambalo limeipa Serikali changamoto kubwa katika suala zima la kufufua na kuendeleza michezo na kuziandaa timu zetu vizuri zinaposhirikia mashindano ya kimataifa. *(Makofi)*

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake marefu sana lakini yenye mwelekeo mzuri. Naomba niulize maswali mawili. Maandalizi yanaambatana pamoja na kuwa na pesa na bahati nzuri ameomba taasisi mbalimbali zisaidie lakini naomba kuuliza.

Je, Serikali yenyewe imeandaa kiasi gani cha fedha?

Suala zima la maandalizi lazima liwe na pesa lakini tunayo timu yetu ya taifa, timu ya Yanga, timu ya Simba ambazo nazo zitashiriki katika mashindano ya kimataifa.

Je, Wizara, BMT, *TFF* zitasaidiaje timu hizi ili ziweze kushinda badala ya kwenda kushiriki?

NAIBU WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Richard Ndassa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli alichokizungumza Mheshimiwa Mbunge, kwamba bila fedha huwezi ukaandaa timu. Lakini, Waheshimiwa Wabunge wote tunafahamu katika nchi yetu kuna vipaumbele na vipaumbele hivyo tutavizungumza leo.

Ukitazama Bajeti ambayo tumepitisha sisi wenyewe humu ndani, Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, ndiyo Wizara ambayo inapata fedha chache sana. Kwa hiyo hata fedha za kuandaa timu tumejikuta tunatafuta wafadhili, fedha ambayo tunapewa na Serikali wote mnafahamu haitoshi na ndiyo maana tunafanya utaratibu ambao duniani kote wanafanya, *Corporates Companies*, watu binafsi, mashirika inasaidia na katika utaratibu tuliojiwekea ambao mnafahamu tumetunga Sheria ndani ya Bunge, *the smallest unit* katika mwanzo wa kuendeleza michezo kitaifa ni klabu, klabu ina katiba yake, ina wapenzi na ina washabiki lazima hao nao wawe na uwezo wa kutafuta *funds* za kusaidia timu yao ifanye vizuri.

Serikali inaingia kwenye mashindano kwa kusaidia wakati mwingine nauli, posho kambini na vitu vidogovidogo ambavyo tuna uwezo navyo. Lakini nataka nitoe mfano hai kabisa, timu ya taifa *'Taifa Stars' TFF* yenyewe kwa kushirikiana na Serikali imeweza kushawishi kampuni ya Serengeti ambayo inaipa shilingi Milioni Mia Saba (700,000,000/=) kwa mwaka na kwa miaka mitano ni shilingi bilioni mbili pointi tano (2,500,000,000/=).

TFF imeweza kushawishi *NMB bank* kuwapa shilingi milioni mia nne kwa mwaka (400,000,000/=) hivyo kwa miaka mitano ni shilingi bilioni mbili (2,000,000,000/=) ndiyo maana timu ya taifa mnaona inafanya vizuri kwa sababu ina

shilingi bilioni nne pointi tano (4,5000,000,000/=) kwa kuomba kutoka kwa wafadhili. Basi ningeomba Simba na Yanga nao wafanye hivyo, hizi ni klabu kubwa, zina uwezo, zinaweza kupata wafadhili wa kuwasaidia, na wanapata wafadhili wengi sana lakini sasa watunze pesa na waimarishe timu zao. *(Makofi)*

Na. 96

Mashindano ya Kombe la Kagame

MHE. PARMUKH S. HOOGAN aliuliza:-

Kwa kuwa, hivi karibuni kulikuwa na Mashindano ya Kombe la Kagame, na kwamba dosari iliyojitokeza ni pale timu ya Yanga iliposhindwa kupeleka wachezaji uwanjani:-

(a) Je, ni sababu gani za msingi zilizosababisha timu hiyo isiende uwanjani?

(b) Je, kila timu iliyoshiriki mashindanyo hayo ilipata mapato gani?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mbunge wa Kikwajuni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba katika hatua ya mwisho ya kukamilisha mechi za mashindano ya kugombea kombe la Kagame yaliyofanyika mwaka juzi, Klabu ya Yanga haikupeleka timu yake uwanjani kucheza na timu ya Simba. Sababu ambayo klabu ilishindwa kupeleka wachezaji uwanjani ilitokana na viongozi wake kudai kuwa, kulikuwa na makubaliano ya pande tatu ambazo ni timu ya Yanga, Simba na Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini *(TFF)* kwamba, klabu hizo mbili zitalipwa fedha kabla ya mchezo huo, jambo ambalo kwa mujibu wa *TFF* halikuwa na ukweli wowote.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Shirikisho la Mpira wa Miguu kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati *(CECAFA)*, Mashindano ya Kombe la Kagame yanapofanyika, timu zinazothibitisha kushiriki hazipati mapato yoyote isipokuwa zinagharamiwa malazi, chakula pamoja na usafiri wa ndani ya nchi yanapofanyika mashindano hayo. Isipokuwa mshindi wa kwanza hadi wa tatu wanapata zawadi kama ifuatavyo:-

· Mshindi wa kwanza dola 30,000 sawa na shilingi milioni arobaini za Kitanzania.
· Mshindi wa pili ni dola 20,000 sawa na shilingi milioni ishirini na sita za Kitanzania.

· Mshindi wa tatu dola 10,000 sawa na shilingi milioni Kumi na tatu za Kitanzania.

Fedha hizo hutolewa na Rais wa Rwanda, Mheshimiwa Paul Kagame.

MHE. PARMUKH S. HOOGAN: Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na jibu zuri la Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini haoni kwamba, kujitoa kwa Yanga ni kuiogopa Simba? (*Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Haya mimi sielewi hapo, haya Mheshimiwa Naibu Waziri, wewe jibu ili mradi tu usiwagawe watu humu ndani. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo napenda kumjibu Mheshimiwa Parmukh Hoogan, Mbunge wa Kikwajuni, kama ifuatavyo.

Nimeeleza vizuri kwamba, kulikuwa na sababu ya msingi lakini siwezi nikajua kama Yanga waliwaogopa Simba, kwa sababu najua yeye Hoogan ni Simba. Kwa hiyo anaweza kuleta ushabiki ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kimsingi nilitaka niseme sisi wenyewe pia kama Serikali hatukupenda kitendo ambacho kilifanywa na Yanga kwa sababu ni kitendo cha aibu. Yale ni mashindano ya Kimataifa, ziko Kanuni na sheria na taratibu. Unapoingia kwenye mashindano na hapa ningependa nitoe wito kwa vilabu vyote, na wanamichezo wote unapokwenda kwenye mashindano ya kimataifa au shindano lolote ziko sheria.

Mashindano ya Klabu Bingwa ya *CECAFA (Kagame Cup)* yana sheria zake, ukiamua kuingia ni lazima utimize masharti na ndiyo maana napenda kufurahia adhabu waliyopewa, wamepewa walipe shilingi milioni 20 na wakafungiwa miaka mitano (5) kwa bahati wameweza kulipa hizo shilingi milioni 20 na wakaomba radhi. *(Makofi)*

Na. 97

Utengenezaji wa Magari, Mitambo na Mashine za Serikali

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE aliuliza:-

Kwa kuwa, Sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2004; imeweka utaratibu katika Kanuni yake ya mwaka 2005, kifungu cha 59 (1) – (5) juu ya utengenezaji wa magari, mitambo na vifaa mbalimbali vya Serikali:-

(a) Je, kwa nini Wizara/Idara mbalimbali za Serikali hazitumii ipasavyo karakana za Serikali zilizopo kila Mkoa?

(b) Je, ni nani mwenye jukumu la kisheria kuainisha karakana za watu binafsi kufanya matengenezo ya vifaa mbalimbali vya Serikali?

(c) Je, ni nani mwenye mamlaka kisheria kusema karakana za Serikali zimeshindwa kutekeleza kazi zake na hivyo kutoa kibali kazi hizo zifanyike kwenye karakana za watu binafsi?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara na Idara mbalimbali za Serikali hazitumii ipasavyo karakana za Serikali zilizopo kila Mkoa kwa sababu zifuatazo:-

(i) Kutokuzingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 inayozitaka Wizara, Idara, Wakala na Taasisi nyingine za Serikali kutumia ipasavyo karakana za Serikali kwa matengenezo ya magari na mitambo yote ya Serikali.

(ii) Uwepo wa karakana za kisasa zaidi katika sekta binafsi zenye uwezo wa kutoa huduma kwa haraka na kwa ufanisi ambao kwa sasa unakosekana kwenye karakana nyingi za Serikali.

(iii) Uchakavu wa miundombinu, ukosefu wa teknolojia pamoja na vifaa vya kisasa katika karakana za Serikali (TEMESA) zilizopo katika kila Mkoa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mwenye jukumu la kisheria kuainisha karakana za watu binafsi kufanyia matengenezo vifaa mbalimbalai vya Serikali ni Wizara ya Miundombinu kwa Mkoa wa Dar es Salaam na Makatibu Tawala wa Mikoa wakishirikiana na Ofisi za Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) kwa upande wa Mikoa mingine.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, mwenye mamlaka kisheria kusema karakana za Serikali zimeshindwa kutekeleza kazi zake na hivyo kutoa kibali kazi hizo zitengenezwe kwenye karakana za watu binafsi ni Mkuu wa Karakana ya TEMESA katika Mkoa husika, baada ya kubaini kuwa karakana yake haitakuwa na uwezo wa kufanya matengenezo husika. Kwa mfano ukosefu wa teknolojia, vifaa vya kisasa, vipuri na kadhalika. *(Makofi)*

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Taasisi na Wizara zinapeleka magari yake kwa hizi *Private Garages* bila hata ya kuwashirikisha hawa TEMESA. Je, Serikali sasa iko tayari kuzuia utaratibu huu ikizingatia kwamba katika *Garage* hizi kuna wataalamu wazuri sana na wakubwa

kuliko hata kwenye *Private Sector* lakini wanatokana tu kwamba vifaa vyao vingi ni vya kizamani kuliko vilivyo vya kisasa katika *Private Garages*?

Lakini la pili, kwa kuwa Waziri amesema kuwa wanatumia *Garage* binafsi kwa sababu zimekosa kuwa na teknolojia za kisasa. Lakini pia Serikali hii inadaiwa na TEMESA zaidi ya shilingi bilioni 2. Je, Serikali haioni kwamba wangewalipa wangekuwa na karakana za kisasa na hivyo kuweza kufanya kazi kwa ufanisi?

Kwa kuwa pia utaratibu wa zamani ulikuwa mzuri sana ambapo fedha hizi zilikuwa zinawekwa Hazina na sio kwa *COs or Accounting Officers.* Je, Serikali iko tayari kurudisha utaratibu huo wa zamani?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba katika Mikoa na Wilaya zote zile ambazo karakana za Serikali ama TEMESA zinafanya kazi vizuri tusingependelea Taasisi za Serikali na Idara zipeleke magari katika gereji za watu binafsi. Hilo tutaendelea kulisimamia na pale tu inapolazimika au inavyobidi kwa sababu moja au nyingine ya mapungufu katika karakana hizi za Serikali ndipo Wakuu wa Karakana hizi katika mikoa husika watatoa vibali kwa magari au vifaa vya Serikali kuweza kufanyiwa matengenezo katika karakana za watu binafsi.

Swali la pili, ni kweli Serikali ina madeni makubwa kwa karakana hizi za TEMESA tutafanya kila juhudi kuhakikisha kwamba tunalipa madeni hayo ili kuwezesha karakana hizi za TEMESA kuendelea vizuri. Ushauri wa Mheshimiwa Simbachawene tumeupokea, tutaufanyia kazi ili tuweze kuimarisha malipo haya yafanywe katika taratibu ambazo itawezesha karakana hizi kuendelea vizuri. Kwa hivi sasa Serikali inaendelea na mpango mahsusi wa kuzikarabati na kuzijenga upya karakana katika maeneo mbalimbali ikijumuisha M.T. *Depot* Dar es Salaam na karakana zilizo katika mkoa wa Manyara na mikoa mingine ili ziwe karakana bora na kuweza kutoa huduma nzuri ya matengenezo ya magari na vifaa vya Serikali.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Waziri ametueleza kwamba Serikali ipo katika mikakati ya kuhakikisha wanakarabati karakana zile ningependa kujua atupe *timeframe* ni lini watazikarabati?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa kukarabati karakana hizi tayari umeshaanza kutekelezwa ndani ya mwaka huu wa fedha 2009/2010.

Serikali imetenga fedha kujenga majengo mawili mapya kabisa kwa karakana ya *M.T. Depot Dar es Salaam* na pia kukarabati majengo ya karakana za TEMESA katika Mkoa wa Manyara na kununua vitendea kazi kwa ajili ya karakana kama 10 hivi kwa

Tanzania nzima. Huo mpango upo unatekelezwa na fedha zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo.

Na. 98

Ubovu wa Barabara Eneo la Sekenke - Nkongilangi

MHE. JUMA H. KILIMBAH aliuliza:-

Kwa kuwa, katika Mkutano wa Bajeti wa mwaka 2006 niliuliza swali juu ya ujenzi wa eneo korofi la Sekenke - Nkongilangi linalogawanyishwa na mtoto Kyenkang'ombe; na Naibu Waziri alitembelea eneo kwa kuona jinsi wananchi wa eneo hilo wanavyopata kero kubwa; na kwa kuwa Serikali iliagiza *TANROADS* kutengeneza eneo hilo kwa gharama ya shilingi milioni 262 fedha ambazo hawakuwa nazo:-

(a) Je, kwa nini Serikali isiangalie uwezekano wa kupata fedha kwa namna nyingine ili eneo hili litengenezwe kuwaondolea kero wananchi wa maeneo ya Roromoni, Migilango, Tyegelo, Ndurumo, Luono hadi Kidaru?

(b) Je, ni kwa nini kunakuwa na ukarabati wa viwango hafifu ambao unasababisha kuharibika mapema kwa barabara husika na kuhitajika ukarabati kwa kila mwaka?

(c) Je, Serikali inachukua hatua gani dhidi ya watendaji wasio wazuri ambao hutoa majibu yasiyoridhisha pale wanapotakiwa kutoa maelezo juu ya barabara?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Barabara ya Shelui - Sekenke hadi Sunsu yenye urefu wa km 22.8 ni ya mkoa wa Singida na inahudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS).* Aidha, kuanzia Sunsu - Roromoni - Misilango - Tyegelo - Ndurumo - Luono hadi Kidaru ni barabara ya Wilaya na inahudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Iramba.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, barabara inayopita katika maeneo ya Roromoni, Migilango, Tyegelo, Ndurumo, Luono hadi Kidaru ni barabara ya Wilaya na inahudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Iramba. Namwomba Mheshimiwa Mbunge kuwasiliana na Halmashauri husika ili waingize katika mipango yao ya maendeleo ili iweze kukarabatiwa, hivyo kuondoa kero kwa wakazi wa maeneo hayo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, matengenezo ya barabara ya Shelui - Sekenke - Sunsu (km 22.8) ambayo ni ya Mkoa yamekuwa yakifanyika kulingana na aina ya matengenezo yaliyokusudiwa kama vile matengenezo ya muda maalum, matengenezo ya sehemu korofi na matengenezo ya kawaida na pia kulingana na viwango vilivyomo kwenye mkataba.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haijapokea tuhuma hizo kwa watendaji wa Wizara kutoa majibu yasiyoridhisha kwa viongozi wanapofuatilia utekelezaji wa kazi. Mara tutakapopokea tuhuma zitachunguzwa na ikibainika, watendaji waliohusika watachukuliwa hatua za kinidhamu.

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nilikuwa tu nataka nipewe maelezo kuhusiana na ile tathmini iliyojieleza katika swali langu ya shilingi milioni 262 ambayo ilitolewa na *TANROAD* mkoa kupelekwa Wizarani juu ya matengenezo ya lile eneo korofi na Wizara ilituahidi kwamba ingetengeneza hili eneo korofi. Je, Wizara inasemaje kuhusiana na ile tathmini ambayo tayari ilishatolewa toka mwaka 2006.

Pili, nafahamu vizuri sana eneo alilolieleza katika kipengele cha (a) juu ya barabara ya Roromoni hadi Kidaru kwamba ni barabara ya Wilaya. Lakini naomba Mheshimiwa Waziri anieleze anasemaje kuhusiana na lile eneo dogo la kipande ambalo linakadiriwa ni kilomita 20 tu kwa sababu tayari tuna barabara ya mkoa inayotoka Shelui hadi Sekenke hadi Sunsu na tunayo barabara ya mkoa inayotoka Kisiriri, Kidaru na inaelekea Ibaga na ushauri ulitolewa na Mheshimiwa Rais alipokuja kwamba hilo eneo lipitishwe liwe la Mkoa.

Je, Waziri anasema yuko tayari kuweza kupitisha eneo hilo kuwa barabara ya mkoa?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tathmini ya shilingi milioni 262 kwa matengenezo ya barabara. Hili tutalifuatilia na nitaagiza wataalamu kwenda kulikagua tena na kama kiwango cha matengenezo yakikidhi basi tutajitahidi kuhakikisha kwamba tunaliweka katika hali inayokidhi haja au inakidhi mahitaji ili wananchi wasisumbuke katika eneo hili. Ama kupandisha daraja kwa eneo hili ambalo Mheshimiwa Killimbah amelitaja kuna Kamati Maalum ya Kitaifa ambayo inafanya tathmini ya kupandisha daraja barabara au kupandisha hadhi barabara katika maeneo mbalimbali Tanzania tutaielekeza ili ichunguze eneo hili na kwa vile tayari limetolewa maelekezo na Mkuu wa Nchi tulifanyie haraka ili tuweze kulipandisha pale inapokidhi viwango.

Na. 99

Serikali Kusaidia Usafirishaji wa Matunda Nje ya Nchi

MHE. FATMA M. MAGHIMBI aliuliza:-

Kwa kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa letu; na kwa kuwa Serikali ina nia ya kusaidia viwanda vya kusindika Matunda vinavyojengwa katika Mikoa mbalimbali:-

Je, Serikali ina mikakati gani wa kujenga mazingira ya kuwawezesha wakulima kusafirisha matunda nje ya nchi katika dhana ya MKUKUTA?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi, Mbunge wa Chake Chake, kama ifuatavyo:-

Serikali kwa kutekeleza kwa kushirikiana na wadau wa mazao ya matunda nchini inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ifuatayo:-

(i) Kuainisha aina za matunda na ubora unaotakiwa katika masoko ya ndani na nje na kuwapatia wakulima vipando bora, kuwafundisha kanuni bora za kuzalisha matunda na kuwapatia maelekezo ya upatikanaji wa masoko ya uhakika ya mazao hayo. Aidha, wakulima wamekuwa wakifundishwa mbinu bora za uzalishaji wa miche bora ya matunda na kusambaza kwa wakulima wenzao.

(ii) Kuandaa na kutekeleza miradi maalum ya kuwajengea uwezo wakulima kuuza matunda wanayozalisha katika soko la nje. Miradi hiyo ni pamoja na Miradi ya Kuendeleza Uzalishaji na masoko ya mazao ya ndizi (*improvement of the Banana Cropping System*) katika Mikoa ya Kagera na Kigoma (Wilaya ya Kibondo). Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Mfuko wa pamoja wa bidhaa za kilimo (*Common Fund or Commodities (CFC)* na Chama cha Wakulima wa Maembe *(Association* of Mango *Growers (AMAGRO)* katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Lindi wameweza kusambaza kwa wakulima jumla ya miche bora ya miembe 27,500.

Lengo la mradi ni kuzalisha miche bora 47,000 ifikapo 2010/2011. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Misaada la Marekani *(USAID)* wameweza kuendeleza kilimo cha matofaa (*apples*) na maparachichi *(avocados)* bora kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi katika Mikoa ya Mbeya na Iringa.

(iii) Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ikishirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko na wadau wa mazao ya bustani nchini wameanzisha Baraza la Kuendeleza Mazao hayo *(Horticulture Development Council of Tanzania (HODECT).* Baraza hilo linahusika katika kuandaa na kuratibu utekelezaji wa mazao ya bustani kwa kushirikisha Serikali na Sekta binafsi ili kuhakikisha wakulima wanapata masoko ya uhakika ya mazao ya ndani na nje ya nchi.

MHE. FATMA M. MAGHIMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa katika swali lake la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri hakuzungumzia habari ya *preservation*. Je, haoni sasa kuna haja ya kuchukua hatua za dharura za kuwafunza

wakulima juu ya *preservation* ya matunda ambayo hivi sasa yanaoza vibaya sana kama vile mananasi, machungwa na matunda mengine?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mkakati wa kilimo kwanza. Je, Serikali imefikiria habari ya *preservation* ya matunda?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, suala la utunzaji wa matunda ni suala ambalo linachukuliwa kwa uzito wa hali ya juu kabisa na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko katika kuwafundisha wakulima jinsi ya kuhifadhi, kuyafunga matunda vizuri kwenye maboksi ambayo yanavutia sana kibiashara. Kwa hiyo, mafunzo haya yanaendelea hata kupitia kwenye Shirika letu la viwanda vidogo vidogo *(SIDO)* wanafanya kazi hii.

Swali lake la pili la kuhusu kilimo kwanza nadhani katika Kilimo kwanza, kuna nguzo 10 za kilimo kwanza na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, inahusika moja kwa moja katika suala zima hili la kuwafundisha wakulima wanaozalisha matunda katika hatua hizi za *parkaging* pamoja na *preservation*.

MHE. MOHAMED R. ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Serikali ina mikakati ya kujenga masoko ya Kimataifa mkoa wa Tanga kwa maana Segera na Mkoa wa Mbeya. Lakini utaratibu huu unasimamiwa na Wizara ya Viwanda na Biashara. Wizara ya Kilimo ina mikakati gani ya kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kujua na kubaini tatizo ni nini kuchelewa kuanzishwa kwa masoko haya? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nikiri kwamba masoko anayoyaulizia ni masoko ya Kimataifa ambayo yalikuwa yanajengwa kwa programu ya AMSDP ambayo yalikuwa yajengwe masoko 20 nchi nzima lakini yameshajengwa 24 na mradi wake umeshakwisha Desemba, 2009 na thamani yake ulitumia karibu shilingi bilioni 50 kwa ajili ya masoko haya.

Nadhani akifuatilia vizuri kwa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko ya kujenga masoko ama waweze kutumia *ASDP* au *DADPs* kuweza kujenga masoko katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Na. 100

Kero ya Maji katika Mji wa Maganzo

MHE. FRED T. MPENDAZOE aliuliza:-

Kwa kuwa, idadi ya watu katika Mji wa Maganzo imeongezeka sana na kwamba kuna upungufu mkubwa wa maji na kusababisha kero kubwa kwa wananchi na kupunguza kasi ya maendeleo:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kutatua kero ya maji katika Mji wa Maganzo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fred T. Mpendazoe, Mbunge wa Jimbo la Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Maganzo ni Mji Mdogo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu wenye wakazi wanaokadiriwa kufikia 15,500 na mahitaji ya maji ni mita za ujazo 775 kwa siku. Mji huu uko umbali wa kilomita 28 kutoka Shinyanga Mjini na kilomita 48 kutoka Makao Makuu ya Wilaya ya Kishapu. Wananchi wa Maganzo hupata maji kutoka katika visima vifupi na chemchemi za vijito kwa ajili ya mahitaji yao vyanzo ambavyo havikidhi mahitaji ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupata ufumbuzi wa tatizo la maji katika Mji Mdogo wa Maganzo tarehe 14 – 16 Mei, 2008 nilifanya ziara katika Mkoa wa Shinyanga ikiwemo Jimbo la Kishapu kwa mwaliko wa Mheshimiwa Fred Tungu Mpendazoe, Mbunge ili kujiridhisha na ukubwa wa tatizo ambapo niliahidi kulitafutia ufumbuzi.

Nafurahi kumwarifu Mheshimiwa Mbunge na wakazi wa Maganzo kwamba Serikali imeamua sasa Mji Mdogo wa Maganzo uunganishwe kwenye mtandao wa maji ya mradi mkubwa wa Kahama Shinyanga. Ili kutekeleza uamuzi huu mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mjini Shinyanga imemwongezea hadidu za rejea Mhandisi Mshauri *Gibb East Africa* anayefanya usanifu wa mtandao wa majitaka Mjini Shinyanga ili afanye usanifu wa kuunganisha Mji wa Maganzo kwenye mtandao wa maji ya mradi wa Kahama Shinyanga ikiwa ni sehemu ya kuviunganisha vijiji ambavyo havikuwa vimefikiwa katika awamu ya kwanza.

Kazi ya usanifu wa miundombinu ya maji inaendelea na inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2010 na kufuatiwa na ujenzi mapema katika mwaka wa 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Mpendazoe, Mbunge wa Kishapu, kwa kutumia uzoefu na utalaam wake kushirikiana na Wizara yangu kufikia uamuzi huu ambao naamini sasa utamaliza kabisa tatizo la upatikanaji wa maji katika Mji wa Maganzo.

MHE. FRED T. MPENDAZOE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize suala moja la nyongeza. Lakini kwanza kwa niaba ya wananchi wa Mji wa Maganzo kwa dhati kabisa naomba kuishukuru Serikali kwa hatua ambayo imeichukua kutatua kero ya maji ya muda mrefu ya mji wa Maganzo.

Lakini vile vile naomba nipokee pongezi toka Serikalini kutokana na ushauri nilioutoa unaotokana na uzoefu wangu. Naomba niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa mara kadhaa nimeishauri Serikali na kuiomba Serikali katika awamu ya pili ya mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kuviingiza vijiji vya Bunambiu, Mwang'iri, Mwasubi na Ikongotale ikiwemo Maganzo ambayo sasa hivi wamekubali kuingiza katika awamu ya pili. Na kwa kuwa Serikali imekubali sasa kuingiza mji wa Maganzo ambao uko kilomita 28 kutoka Mji wa Shinyanga ambako itakuwa ni chanzo cha maji kwa ajili ya Mji wa Maganzo. Serikali haioni ni busara sasa vilevile kuviingiza vijiji vilivyobaki vya Mwahiri, Itongwetale, Mwasubi na Bunambiu katika awamu ya pili kwa sababu vijiji hivyo pia vina kero kubwa ya maji na viko karibu na chanzo cha maji ya bomba hilo kuu la kutoka Ziwa Victoria?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kweli Serikali inaona ni busara kuongeza vijiji na tunaendelea kufanya hivyo kwa awamu zinazofuata kulingana na fedha zinavyopatikana.

Lakini pia nimwelezee Mheshimwa Mpendazoe kwamba tayari kijiji hicho cha Bunambiu na vijiji vingine 12 vimo katika Mpango wa Vijiji 13 ambavyo hivi sasa vinafanyiwa usanifu katika mpango ule wa vijiji 10 wao kwa bahati nzuri wanatekeleza vijiji 3. Labda kwa faida tu kwa haraka nimtajie kwamba vijiji vya Bunambiu, Sekeibibi, Mwamadulu, Unyanyembe, Kalolebi, Ngofiwa, Bulekela, Mwamashimba, Iboja, Mwigumbi, Buginza na Nyenze vimo katika utaratibu huu wa vijiji 13. Kwa hiyo, vijiji vingine tutaendelea kuviangalia katika awamu inayofuata.

MHE SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tatizo la mji mdogo wa Maganzo linafanana kabisa na lile la mji mdogo wa Himo kule katika Mkoa wa Kilimanjaro. Na kwa kuwa ni kipindi kirefu sasa wale hawajaweza kupatiwa maji na tatizo hili linafahamika Wizarani. Leo Serikali inatueleza nini kuhusu mji ule?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri sijui unaujua huo mji?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, naujua mji wa Himo. Napenda tu nimhakikishie Mheshimiwa Raymond kwamba mji wa Himo umo katika mipango yetu ya maji. Hivi sasa najua kuna mpango mkubwa sana unaoendelea katika mji wa Himo na miji mingine pale katika mkoa mzima wa Kilimanjaro. Lakini tumetuma wataalamu wetu angalau kuangalia matatizo yanayowasibu wakazi wa Mkoa mzima wa Kilimanjaro mpaka kule Rombo na hatimaye tupate ufumbuzi ambao nina hakika kabisa na Mji wa Himo utahusika maana mimi mwenyewe nimetembelea mji wa Himo nimeshirikiana na viongozi pale mpaka kwenye vyanzo. Kwa hiyo naomba awe na subira tu kwamba muda sio mrefu tutapata majibu kwa ajili ya mji wa Himo.

Na. 101

Mradi wa Maji wa Kibaya – Kiteto Kusimama

MHE. BENEDICT N. OLE- NANGORO aliuliza:-

Kwa kuwa Mji wa Kibaya una tatizo kubwa la maji na kwamba mfumo wa mabomba ya maji yanayotumika sasa ni wa zamani miaka ya 1961 na ulikarabatiwa mara ya mwisho miaka ya 1974 na kwa kuwa mradi wa maji wa Kibaya ulishabuniwa na kuanza kutekelezwa na baadaye ukasimamishwa.

(a) Je, ni sababu zipi zilizofanya mradi huo usimamishwe?

(b) Je, ni lini Serikali itakamilisha mradi huo muhimu ili wakazi wa Mji wa Kibaya wapate huduma za maji?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Benedict Ole Nangoro, Mbunge wa Kiteto, napenda kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Kibaya ambao ni Makao Makuu ya Wilaya ya Kiteto una wakazi 15,665. Huduma ya maji katika Mji wa Kibaya inatolewa na Mamlaka ya Maji ya Mji wa Kibaya. Mahitaji ya maji kwa Mji wa Kibaya kwa mwaka 2008/2009 yalikuwa mita za ujazo 7,200 kwa siku. Vyanzo vilivyopo vya visima vina uwezo wa kuzalisha maji mita za ujao 273 lakini sasa uzalishaji ni mita za ujazo 270 tu sawa na asilimia 3.8 ya mahitaji ya wakazi 15,665. Baada ya kutoa maelezo hayo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benedict Ole Nangoro, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, mradi uliokuwepo awali ulijulikana kama *Kibaya Urban Initiative Project* ambao usanifu wake ulikamilika Novemba, 2003. Mradi huu ulikuwa unafadhiliwa na Serikali ya Sweden kupitia Shirika la Maendeleo la *SIDA*. Mradi ulihusisha uendelezaji wa maji Mjini pamoja na hospitali ya Wilaya ya Kibaya. Baada ya usanifu kukamilika ilionekana kuwa gharama za utekelezaji wa mradi ni kubwa kuliko uwezo wa mfadhili huyo, hivyo utekelezaji wake haukufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada ya kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Kibaya kwa mpango wa muda mfupi Serikali katika mwaka 2007/2008 ilituma shilingi 117,892,300 kwenda Mamlaka ya Maji mjini Kibaya. Fedha hizi zilitumika kwa ajili ya kuchimba mtaro, kufunga mabomba ya maji yenye urefu wa kilomita 5 na kununua matanki mawili ya maji ambayo bado hayajafungwa.

Nakiri kwamba Halmashauri ya Wilaya imechukua muda mrefu kununua matanki hayo kutokana na taratibu za manunuzi lakini nafurahi kumwarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari matanki hayo yamenunuliwa. Napenda kumwahidi Mheshimiwa Mbunge

na wakazi wa Mji wa Kibaya kwamba Wizara yangu itashirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto kusimamia kazi ya kusimika matanki hayo mawili na kuhakikisha kwamba maji yanafika katika vijiji vya Ngarenaro, Mafichoni, Karoleni, Bagamoyo na Jangwani.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa la Mji wa Kibaya na Vijiji vinavyouzunguka ni uhaba wa maji ya mito lakini maji chini ya ardhi yanaweza kupatikana. Katika mwaka 2009/2010, Serikali kupitia programu ya kuendeleza sekta ya maji itafanya uchunguzi wa vyanzo vipya vya maji vitakavyoweza kukidhi mahitaji ya wakazi wa Mji wa Kibaya kwa muda mrefu.

MHE. BENEDICT N. OLE - NANGORO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii, kwa niaba ya wakazi wa Kiteto, naomba kwanza nishukuru Serikali kwa jitihada zinazoendelea kutatua matatizo ya maji katika vijiji mbalimbali Wilayani. Pamoja na majibu mazuri ya Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza:-

(a) Kwa kuwa, fedha zimetumika kwa mradi huu lakini mradi haujakamilika na kwa sababu hiyo matatizo ya maji yanazidi kuwa makubwa na watu wana matatizo ya homa ya matumbo hasa watu wanaoishi Ngarenaro, Kaloleni, Bwagamoyo na Jangwani. Kwa nini Serikali iliwaahidi wakazi wa Kiteto Mjini Kibaya kwamba itatoa fedha za kutosha kukamilisha mradi huu ambao umeanza lakini haujakamilika, kwa muda mrefu sasa umesimama?

(b) Kwa kuwa, hata awamu hii ya mradi itakapokamilika bado ni asilimia ndogo sana ya wakazi wa Mji wa Kibaya ndiyo watakaopata maji safi na salama, je Serikali inasema nini kuhusu kuahidi kutoa fedha za kutosha kwa ajili ya kuchimba visima ili matatizo ya maji katika Mji wa Kibaya yaweze kupungua ama kuisha na watu wote wanaokaa Mjini Kibaya waweze kupata maji safi na salama?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu katika majibu ya swali la msingi, ni kweli Serikali tumeshatumia shilingi 117 milioni na mradi ule bado haujakamilika na matanki bado yamesimama pale, kwa hiyo ni jukumu letu kama Serikali na ninataka nimuahidi kwamba Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kukamilisha kazi ile kwa sababu haiwezekani tukaacha kiporo njiani na tukaanza miradi mingine. Kwa hiyo, hilo nataka nimuahakikishie kabisa kwamba tutashirikiana na watalaamu wa Halamashauri ile ili tuweze kwanza kupata fedha halafu kuhakikisha kwamba kazi ile inakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia naomba nimhakikishie kwamba watalaamu wa kutoka Wizarani ni muhimu kabisa wakaenda Kiteto na watakwenda kwa sababu tayari tumeona udhaifu tulionao katika Halmashauri zetu katika kutekeleza miradi hii ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jibu la nyongeza sehemu ya (b) nimesema kwenye mpango wetu wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Maji, tutafanya uchunguzi

mzito wa maji chini ya ardhi na nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kufanya uchunguzi na hivi karibuni tumekuwa na mazungumzo pia na wafadhili mbalimbali na tuliingiza Wilaya ya Kiteto katika mazungumzo yetu na ninamwomba awe na hakika, nimemhakikishia Mheshimiwa Ole-Nagoro kwamba mimi binafsi nitatembelea Wilaya ya Kiteto ili nione tatizo hili na ukubwa wake na tutaendelea kutafuta fedha. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda pia umekwisha.

Ninao wageni ambao ninapenda kuwatambulisha kwenu, kwanza kabisa kwenye *Speakers Gallery*, kuna wageni wa Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni wale wanaotoka katika Shirika linaloitwa *Engender Health* ambao wanaongozwa na Ms. Feddy Mwanga ambaye ni Technical Director, *if you are there please rise your hand*, yupo Mr. Adam Mambeya ni *Financial Director* na Dr. Mkingama Kapinga yeye ni Meneja wa Shirika hilo katika Kanda ya *Southern Highlands* na mimi binafsi hawa watu wa *Engender Health* wamenisaidia sana kupanua Kituo cha Afya ili kusudi mama na watoto walioathirika na ugonjwa wa *HIV* waweze kukaa. Wamesaidia pia kuweka maji katika kituo hicho, wamejenga pia kituo cha kutolea meno katika eneo hilo hilo, sasa hivi tunaendelea, wakipata nafasi waende kwenye vituo vya afya vingine pale Njombe Mjini. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, pia wanafanya kazi hizi katika Mikoa mingi ya Tanzania Bara pamoja Zanzibar na Mheshimiwa Waziri Mkuu pia wanashughuli naye, nafikiri leo wakipata nafasi watakuwa naye.

Waheshimiwa Wabunge, nina wageni wengine hawa ni wageni ambao ni Maafisa na Waheshimiwa Wabunge kutoka *Canadian Parliamentary Centre* ofisi ya Ghana, wanaongozwa na Rais wa umoja wa vyama vya Wabunge wanaopambana na Rushwa *APNAC* na wengi wetu ni wajumbe wa *APNAC*, sasa Rais wetu leo ndiyo amekuja na anaitwa Given Rubinda, yeye anatoka Zambia, *can you please rise*, kwa hiyo sisi wajumbe wote wa *APNAC* Rais wetu ni huyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Dr. Anthony Tsepho yeye ni *Senior Budget Expert* katika kituo kile cha *Parliamentary Center* Ghana, yupo pia Mr. Elvis Ottoh, yeye ni Mtalaamu wa mambo ya *monitoring* na *evaluation* katika kituo hicho hicho, yupo pia Ms Nasata Yakub, yeye ni Mtalaam wa mambo ya *Conflicts* naye pia anatoka *Parliamentary Centre*, Ms Christina Ofey yeye ni *Program* na *Research Assistant*, Mr. Robert Sichinga yeye ni Mshauri katika mambo ya Mikakati ya Kuandaa Programu za Kufundishia na Mr. Daniel Batidamu, *Executive Director APNAC. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni hawa wapo hapa kwanza kabisa nitaeleza baadaye kwamba itabidi wakutane na wajumbe wa *APNAC* kwa sababu wanataka kufahamu kuwepo kwetu lakini wale wa *Parliamentary Centre* pia tunao mkataba kati ya Bunge letu na *Parlaimentary Centre* ili kujifunza mambo ya *budget*, tutakuwa na mkataba wa miaka kama mitano na zipo nchi saba ambazo zimeingia katika mpango huu

na Tanzania ikiwemo, Mabunge mengine ni Benin, Ghana, Kenya, Senegal, Uganda na Zambia. Kwa hiyo, sisi Tanzania tumepata nafasi hiyo kwa sababu mpango huu wa kwanza ulioanza mwaka 2002 ulihusisha Mabunge kama 20 baadaye wameona afadhali wafanye Mabunge kama saba ili tuingie kwa undani sana kwenye mambo ya kuangalia *budget* zetu za Serikali na jinsi tunavyoweza kuwasaidia wananchi kuelewa *budget* zetu. Kwa hiyo, watakuwa na vikao na Kamati ya Uchumi na Fedha, *APNAC* na wengine ambao wako kwenye ratiba.

We also welcomes you to our Parliament, it has been nice you come when the session is going on, we will have a session on budget but we are trying to modify our system so that we can really adhear to the system of the budget control as much as we can, so you are most welcome. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tunao Wageni wa Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa William Ngeleja ambao ni Wenyeviti kumi na nne wa Kata ya CCM, Jimbo la Sengerema, Katibu wa Mbunge anaitwa Peter Ngelela. Katibu wa Mbunge na Wenyeviti wote wasimame, karibuni sana, jana bahati mbaya nadhani walikosea kutaja majina yenu, naomba mjisikie mpo nyumbani. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge tuna wageni wa Mheshimiwa Profesa Mwalyosi, Mbunge wa Ludewa, ni Mheshimiwa Diwani wa Kata ya Iwela na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Ludewa Joakim Lukuwi, Mheshimiwa Elfrida Kizota, Diwani wa Kata ya Manda, Diwani pekee mwanamke katika Halmashauri yao, tunakupongeza sana na tunaomba uhakikishe unashika hatamu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Mheshimiwa Damas Nakei na Mheshimiwa Omar Kwaangw' ambao ni Wenyeviti wawili wa Wazee na Wazazi Babati vijijini, naomba wasimame na Makatibu Tarafa wawili wa Babati Vijijini karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Babati Vijijini na Wajumbe wa UWT Mkutano Mkuu wa Mkoa wa Manyara, ahsanteni sana na karibuni sana katika Bunge letu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Mheshimiwa Charles Mwera kutoka *Central High School* ambao ni Ndugu Denis Samo, Ndugu Samweli Mwita, Ndugu Dionis Godfrey, Ndugu Abrahim Mtama na Marwa Gasero ambaye ndiye Mwenyekiti wa Mtaa wa Yangeyange, Kata ya Msongola Ukonga Dar Es Salaam, kumbe hawa ni wa Dar es salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni kumi na tano wa Mheshimiwa Godfrey Zambi ambao ni Walimu Wakuu wa Kata ya Vwawa, wakiongozwa na Afisa Elimu Msaidizi wa Wilaya ya Mbozi, Ndugu Jeremiah Senyagwa, naomba msimame mlipo, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao Jumuiya ya Walimu wa Madrasa Dodoma wapo kumi na nne, wamekuja kulitembelea Bunge wakiongozwa na Ustaadh ndugu Abubakary Yahya, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye ndugu Stewart Meta, ni Mtumishi wa Serikali katika Wizara ya Afya Kitengo cha Damu Salama, karibu, Waheshimiwa Wabunge mkitakiwa kutoa damu mnakaribishwa. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi hamsini kutoka Shule ya Sekondari ya Dodoma, naomba msimame mlipo karibuni sana, ninyi mnaruhusiwa kuja hapa mkipata nafasi. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi hamsini na tatu kutoka Chuo Kikuu cha Ardhi Dar es Salaam, nadhani wapo kule *basement,* karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hii ndiyo idadi ya wageni niliyoletewa hapa Mezani.

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Nyongeza wa Mwaka 2010 (The Supplementary Appropriation Bill, 2010)

(Kusomwa kwa Mara ya Pili)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Muswada huu tunao, lakini tumeona kwanza uende kwenye Kamati inayohusika ili kusudi waweze kutolea maoni na pia Kambi ya Upinzani nao waweze kupata nafasi ya kutolea maoni, kwa hiyo, kesho ndiyo utakuja rasmi kwa kufanyiwa kazi.

HOJA ZA SERIKALI

Mapendekezo ya Mwongozo wa Utayarishaji wa Mpango wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla ya sijamwita mtoa hoja, nitamwomba Mheshimiwa Jenista Mhagama aje anipokee nafasi hii. Halafu naomba wajumbe wa Kamati ya Uongozi tukutane katika ofisi ya Spika, tukaangalie ratiba baada ya kukubaliana kwamba Muswada wa *Security* unarudi tena.

Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita mtoa hoja, ninaomba nitoe taarifa kwamba hoja hii inazingatia Kanuni ya 94, Toleo la mwaka 2007 na kwa kuwa shughuli ni ya Kikanuni, tutaendelea kuifanya tukiwa ndani ya ukumbi huu na

hivyo itatuchukua kwa takribani siku mbili, leo na kesho. Baada ya kutoa maelezo hayo, naomba kumwita mtoa hoja aweze kutoa maelezo yake.

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na kwa kuzingatia Kanuni ya 94 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, baada ya Bunge lako Tukufu kukaa kama Kamati ya Mipango, napenda kuwasilisha maelezo kuhusu Mwongozo wa Kutayarisha Mpango na Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha muda wa kati (2010/2011 – 2012/2013). Aidha, napenda kuishukuru Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omari Kigoda (MB), kwa kupitia maeneo mbalimbali ya vipaumbele yatakayotekelezwa na kutoa maoni na mapendekezo ambayo yameboresha Mwongozo huu. Vile vile, napenda kuitumia fursa hii, kuwashukuru wadau katika ngazi mbalimbali walioshiriki katika mchakato wa uandaaji wa Mwongozo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo huu unawasilishwa katika Kamati hii ili uweze kujadiliwa kwa kina na hatimaye kupata maoni ambayo yatauboresha na hivyo kuwezesha Wizara, Idara za Serikali zinazojitegemea, Mikoa na Serikali za Mitaa, kuandaa Mipango na Bajeti zao kwa mwaka wa fedha 2010/11 – 2012/13. Mpango huu umetayarishwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Malengo ya Maendeleo ya Milenia 2015, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005, malengo ya KILIMO KWANZA na taarifa za utekelezaji wa Sera, Mipango na Mikakati ya Wizara, Taasisi, Mikoa na Serikali za Mitaa. Vile vile, Mwongozo umezingatia mwenendo wa uchumi duniani ambao umekumbwa na msukosuko tangu mwaka 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo makuu katika maeneo yaliyozingatiwa katika mwongozo huu ni haya yafuatayo:-

Malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025:-

- Maisha bora na mazuri;
- Uchumi imara na wenye kuhimili ushindani;
- Utawala na uongozi bora;
- Jamii iliyoelimika na inayopenda kujifunza zaidi; na
- Amani, Utulivu na Umoja.

Malengo ya Maendeleo ya Milenia:-

- Kuondoa kabisa umaskini uliokithiri na njaa;
- Kufikia elimu ya kumudu maisha kwa wote;
- Kukuza usawa wa jinsia na kuwawezesha wanawake;
- Kupunguza kiwango cha vifo vya watoto;
- Kuboresha afya ya uzazi;
- Kukabili UKIMWI, Malaria na magonjwa mengine;
- Kuwezesha utunzaji na uendelevu wa mazingira; na
- Kukuza mahusiano ya kidunia katika maendeleo.

Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005:-

- Kulinda mafanikio ya kiuchumi na kijamii yaliyokwishapatikana;
- Kujenga msingi wa uchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea;
- Kuboresha sekta za uzalishaji mali;
- Kuimarisha sekta za miundombinu na huduma za kiuchumi;
- Kuendeleza Sera ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi; na
- Kuboresha sekta ya huduma za jamii;

Mheshimiwa Mwenyekiti, MKUKUTA una nguzo tatu (3) za matokeo zinazolenga kutekeleza Dira ya Taifa ya Mwaka 2025, Malengo ya Milenia *(MDGs)* na Ilani ya CCM ya mwaka 2005. Nguzo hizo ni:-

- Ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini wa kipato;
- Uboreshaji wa hali ya maisha na huduma za jamii; na
- Utawala bora na Uwajibikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo huu pia umezingatia maoni na mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge yaliyotolewa wakati Bunge lilipokaa kama Kamati ya Mipango kupokea na kujadili Mwongozo wa Mpango na Bajeti wa mwaka 2009/10. Miongoni mwa maoni na mapendekezo yaliyotolewa, yalikuwa ni kuishauri Serikali kutekeleza yafuatayo: Kuimarisha miundombinu ya barabara, reli, bandari na viwanja vya ndege; Kupunguza msongamano katika bandari ya Dar es Salaam; Kuanzisha Benki ya Kilimo; Kudhibiti misamaha ya kodi; na Kuendelea kutekeleza mikakati ya kuimarisha ukusanyaji wa mapato. Maoni na mapendekezo haya yamezingatiwa katika vipaumbele vya Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya Mwenendo wa Uchumi na Bajeti kwa mwaka 2009/2010. Mpango na Bajeti ya mwaka 2009/10 vimelenga kutekeleza Sera za Uchumi jumla na inatarajiwa kuwa Pato la Taifa litakua kwa asilimia 5.0 mwaka 2009 ikilinganishwa na ukuaji halisi wa asilimia 7.4 mwaka 2008. Kushuka kwa ukuaji wa Pato la Taifa kumesababishwa na athari za msukosuko wa uchumi duniani na ukame uliojitokeza katika msimu wa 2008/09. Hata hivyo, kasi ya ukuaji wa uchumi inatarajiwa kuongezeka mwaka 2010 kufikia asilimia 6.1. Aidha, mapato ya ndani yanatarajiwa kufikia asilimia 16.4 ya Pato la Taifa mwaka 2009/10 na kasi ya upandaji wa bei isiyozidi asilimia 10 ifikapo Juni 2010. Kadhalika, Serikali inalenga kuwa na akiba ya fedha za kigeni yenye uwezo wa kuagiza bidhaa na huduma kwa kipindi kisichopungua miezi mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pato la Taifa Takwimu za Pato la Taifa kwa robo mwaka zinaonesha kuwa, katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka (Januari – Machi 2009) uchumi wa Taifa ulikua kwa asilimia 5.61 ikilinganishwa na asilimia 6.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2008. Aidha, ukuaji wa uchumi katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka (Aprili – Juni 2009) ulikuwa asilimia 5.21 ikilinganishwa na asilimia 7.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2008. Kulingana na mwenendo huu, matarajio ya kukua kwa uchumi kwa mwaka 2009 ni kufikia zaidi kidogo ya makisio ya awali ya

asilimia 5.0. Kiambatisho A (Jedwali Na. I & II) kinaonesha mwenendo wa ukuaji wa Pato la Taifa kwa mwaka na kwa Robo mbili za mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha utoaji wa takwimu za mwenendo wa uchumi, kwa mara ya kwanza, taarifa za ukuaji wa uchumi zimeanza kutolewa kwa vipindi vya robo mwaka kama nilivyoeleza. Serikali inaendelea kuboresha mchakato wa utoaji wa takwimu hizi ili taarifa za ukuaji uchumi za robo mwaka zitoke mapema kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumuko wa bei ulifikia asilimia 12.2 mwezi Desemba 2009 ikilinganishwa na asilimia 13.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2008. Hali hii imetokana na uhaba wa chakula nchini na katika baadhi ya nchi jirani kutokana na ukame. Itakumbukwa kwamba, chakula huchangia asilimia 55.9 katika matumizi yote ya kaya, na hivyo upatikanaji wa chakula nchini ni muhimu ili kusaidia kushusha mfumuko wa bei. Hata hivyo, kuanzia mwezi Oktoba 2009, kasi ya upandaji bei ya chakula imeanza kushuka, kutoka ongezeko la asilimia 18.1 hadi asilimia 14.5 mwezi Desemba 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matarajio ya Serikali kwamba, mvua zinazoendelea kunyesha katika baadhi ya maeneo, zitasaidia katika uzalishaji wa chakula zaidi. Serikali itaendelea kuboresha na kukarabati miundombinu ya usafiri ikiwemo ile iliyoharibiwa na mvua hizo, ili kurahisisha usafirishaji wa chakula kutoka sehemu zenye ziada kwenda sehemu zenye upungufu. Aidha, Serikali iko katika mchakato wa kuangalia uwezekano wa kutumia Hifadhi ya Taifa ya Chakula katika kuleta utengamano wa bei. Hivyo, mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kushuka kufuatia hali nzuri ya uzalishaji wa chakula nchini na katika nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) ulikua kwa asilimia 20.8 ikilinganishwa na asilimia 24.4 mwaka 2008. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3)2 ulikua kwa 18.4 mwaka 2009 ikilinganishwa na asilimia 22.7 mwaka 2008. Kasi ndogo ya ongezeko la ujazi wa fedha ilitokana na ongezeko dogo la utoaji mikopo kwa sekta binafsi kutokana na tahadhari iliyochukuliwa na benki kufuatia hali ya mtikisiko wa masoko ya fedha na mitaji duniani. Kasi ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ilipungua kutoka wastani wa asilimia 35.8 katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita hadi wastani wa asilimia 27.9 mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka ya hivi karibuni, viwango vya riba vimeonesha mwelekeo mzuri hasa kuanzia mwaka wa fedha 2006/07, ambapo riba kwenye amana za akiba zimekuwa zikiongezeka, wakati riba zinazotozwa kwenye mikopo zimekuwa zikipungua. Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2009/10, wastani wa viwango vya riba kwa amana za akiba za muda mfupi (hadi mwaka mmoja) ulikuwa asilimia 8.92 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 5.21 katika mwaka wa fedha 2003/04. Katika kipindi hicho, wastani wa viwango vya riba vilivyotozwa na benki za biashara kwa mikopo ya mwaka mmoja ulipungua hadi asilimia 13.93 kutoka asilimia 15.75. Kutokana na mwelekeo huo wa riba, tofauti kati ya viwango vya riba kwenye amana za mwaka mmoja na viwango vya riba kwenye mikopo ya mwaka mmoja ilishuka

kutoka asilimia 10.54 mwaka 2003/04 hadi asilimia 5.01 mwaka 2009/10, sawa na kushuka kwa asilimia 47.50. Jedwali Na. 1 hapo chini inaonesha mwenendo wa riba kwa kipindi cha mwaka 2003/04 hadi 2009/10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupungua kwa tofauti kati ya viwango vya riba kwenye amana za mwaka mmoja na viwango vya riba kwenye mikopo ya mwaka mmoja kulitokana na: ushindani uliosababishwa na ongezeko la benki zinazotoa huduma; kupungua kwa riba kwenye dhamana za Serikali; pamoja na kupungua kwa viwango vya riba inayotozwa na Benki Kuu kwa Benki za Biashara zinapochukua mikopo (kutoka wastani wa asilimia 18.34 mwaka 2006/07 hadi wastani wa asilimia 4.61 katika nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2009/10).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kwamba viwango vya riba vinavyotozwa sasa bado viko juu ikilinganishwa na viwango vya riba vinavyowekwa kwa wakopaji wakubwa (Jedwali 1). Kukosekana kwa taarifa sahihi za wakopaji na kutokuwepo kwa Taasisi ya Kuhakiki ukweli wa Taarifa za Waombaji Mikopo *(Credit Reference Bureau)* nchini, zimechangia kwa kiasi kikubwa tofauti hizo katika viwango vya riba. Serikali itaimarisha soko la dhamana za Serikali ili kufikia viwango halisi vya riba vinavyotokana na nguvu za soko na visivyobadilika mara kwa mara. Aidha, Serikali inaendelea na mchakato wa kutekeleza Awamu ya Pili ya Mageuzi katika Sekta ya Fedha kwa nia ya, pamoja na mambo mengine, kuimarisha mazingira ya ushindani katika sekta hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, thamani ya shilingi ya Tanzania ilishuka kutoka wastani wa shilingi 1,195.75 kwa dola mwaka 2008 hadi wastani wa shilingi 1,318.71 kwa dola mwaka 2009, sawa na kushuka kwa wastani wa asilimia 10.3. Kushuka kwa thamani ya shilingi kulitokana hasa na msukosuko wa fedha duniani uliowafanya wafanyabiashara kuamini kuwa fedha za kigeni zingeadimika na hivyo kutafuta dola za ziada kwa lengo la kuhodhi. Hali hiyo ya kuhodhi fedha za kigeni inadhihirika katika ongezeko kubwa la rasilimali za fedha za kigeni *(foreign assets)* na amana za fedha za kigeni katika benki za hapa nchini. Katika kipindi hicho, rasilimali za fedha za kigeni ziliongezeka kwa asilimia 51.2 hadi dola za Kimarekani milioni 985.8 mwezi Desemba 2009, kutoka dola milioni 652.0 mwaka 2008; hili ni ongezeko kubwa ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2008, ambapo rasilimali za fedha za kigeni zilipungua kwa asilimia 21.8 sawa na upungufu wa dola za Kimarekani milioni 162.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matarajio ya Serikali kwamba, thamani ya shilingi itaimarika kadri athari za msukosuko wa uchumi zinavyopungua. Serikali inaendelea kutekeleza sera ya soko huria, ambapo thamani ya shilingi hutegemea mahitaji na upatikanaji wa fedha za kigeni katika soko la jumla la fedha hizo. Hali kadhalika, Serikali inaendelea kutekeleza sera zinazolenga kuongeza mauzo nje ya nchi, ikiwa ni pamoja na kuhamasisha uwekezaji katika sekta hiyo ili kuongeza mapato katika fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapenda kusisitiza kwamba, njia bora ya kuhakikisha uimara wa shilingi yetu ni kuongeza uzalishaji wa bidhaa kwa ajili ya kuuza nje ya nchi ili kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni na hivyo kukidhi uagizaji wa

bidhaa toka nje. Vile vile, Serikali inachukua hatua kuimarisha usimamizi na udhibiti wa maduka ya fedha za kigeni kwa kuzingatia Sheria na taratibu zilizowekwa ili kuimarisha thamani ya shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mauzo ya bidhaa na huduma nje yaliongezeka hadi dola za Kimarekani milioni 4,693.6 mwaka 2009 kutoka dola za Kimarekani milioni 4,687.7 mwaka 2008. Ongezeko hilo lilitokana na mauzo nje ya huduma, dhahabu na bidhaa asilia, wakati ambapo mauzo nje ya bidhaa za viwandani yalipungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msukosuko wa fedha uliozikumba nchi nyingi duniani uliendelea kuwa na athari kwenye bidhaa za Tanzania zinazouzwa nje; bei zote za bidhaa asilia, isipokuwa bei ya chai na tumbaku, zilishuka mwaka 2009 ikilinganishwa na mwaka 2008. Hata hivyo, kuongezeka kwa kiasi kilichouzwa nje, kulisaidia kupunguza makali ya kushuka kwa bei za bidhaa asilia. Kutokana na hali hiyo, mauzo ya bidhaa asilia nje ya nchi yaliongezeka kwa asilimia 12.5, kutoka dola za Kimarekani milioni 418.4 mwaka 2008 hadi dola milioni 470 mwaka 2009. Mauzo ya dhahabu nje yaliongezeka kwa asilimia 15.4 hadi dola milioni 1,076.1 kutokana na kuongezeka kwa kiasi cha dhahabu kilichouzwa nje pamoja na ongezeko kidogo katika bei ya dhahabu. Bei ya dhahabu iliyouzwa nje iliongezeka kwa asilimia 11.6 hadi dola 972.7 kwa *troy once*. Aidha, mauzo ya bidhaa za viwandani yalipungua kutoka dola milioni 662.4 mwaka 2008 hadi dola milioni 497.6 mwaka 2009, sawa na upungufu wa asilimia 24.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mauzo ya huduma nje yaliongezeka kwa asilimia 3.0 hadi dola za Kimarekani milioni 2,059.6 mwaka 2009 ikilinganishwa na dola milioni 1,998.8 mwaka 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje *(fob)* ilipungua kwa asilimia 7.1 mwaka 2009 kufikia dola za Kimarekani milioni 7,514.0, kutoka dola milioni 8,089.2 mwaka 2008. Hii ilitokana hasa na kupungua kwa thamani katika uagizaji wa mafuta kutoka nje. Thamani ya mafuta yaliyoagizwa kutoka nje ilipungua kutoka dola milioni 1,838.6 hadi dola za Kimarekani milioni 1,307.5 licha ya kiasi kilichoagizwa kuongezeka kutoka tani 2,316,481 hadi tani 2,916,484. Kwa upande mwingine, thamani ya huduma zilizoagizwa kutoka nje iliongezeka kutoka dola milioni 1,605.8 hadi dola milioni 1,738.3.

Aidha, katika kupunguza urasimu na uvujaji wa mapato ya Serikali kutokana na mafuta, Serikali imeimarisha *flow meters* katika kudhibiti uingizaji wa bidhaa za petroli na mafuta ya kula kwa kushirikiana na wadau wengine kama Mamlaka ya Bandari na Usalama wa Taifa. Kwa sasa *'flow meters'* kumi na sita (16) zilizofungwa Dar es Salaam zote zinafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa muda wa utoaji mizigo bandarini unapunguzwa, Mamlaka ya Mapato Tanzania itatekeleza Mkakati wa *Customs Modernisation Strategy and Action Plan 2009/10 – 2012/13*. Mambo yatakayozingatiwa katika Mpango huo ni pamoja na:-

(i) Kuanzishwa kwa maeneo ya kuhifadhi makasha nje ya bandari *(Inland Container Depots-ICD);*

(ii) Kuunganishwa kwa Idara ya Forodha na TISCAN (ASY-SCAN) kupitia mtandao wa ASYCUDA ++; na

(iii) Kutekeleza Mpango wa Wafanyabiashara Waadilifu *(Compliant Traders Scheme)* kwa mizigo yao kuidhinishwa kutolewa ndani ya saa 24 bandarini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na juhudi nilizozieleza hapo juu, utafiti uliofanywa na *TRA* mwaka 2009 juu ya muda unaotumika katika kuondosha mizigo bandarini umebaini kuwa muda umepungua kutoka siku saba hadi siku mbili na nusu katika mwaka 2009. Pamoja na juhudi hizo, kuna njia mbadala zinazopendekezwa na wadau kukabiliana na changamoto katika kufikia malengo ambazo ni:-

(i) Utekelezaji wa *Port Master Plan* na mpango wa kuendeleza utendaji katika kitengo cha makasha bandari ya Dar es Salaam;

(ii) Aidha, wadau wakuu wengine bandarini yaani *TICTS* na *ICDs* nao wapo katika hatua za kuwekeza kwenye maeneo yao;

(iii) Utaratibu wa kuwa na teknolojia ya pamoja ya kuwasiliana kati ya wadau wakuu wa bandari ni moja ya mpango uliopo sasa;

(iv) Kutekeleza mpango wa kupunguza muda wa makasha kukaa bandarini hadi kufikia lengo la siku 5 la muda wa makasha kukaa bandarini kabla ya kuondolewa;

(v) Kujenga uelewa zaidi wa taratibu za kuondolea bidhaa bandarini hasa kwa wadau wa bandari ambao ni waagizaji bidhaa *(importers)* na wafanya biashara wengine; na

(vi) Kutokana na mpango uliopo wa utekelezaji wa masuala ya forodha katika Jumuiya ya Afrika Mashariki *(East African Customs Union),* Serikali inashauriwa kuondoa malipo ya thamani *(Custom bonding)* ambayo yameonyesha kuwa ya juu kwa bidhaa ziendazo nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeyapokea mapendekezo haya na inayafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akiba ya fedha za kigeni hadi Desemba 2009: Akiba ya fedha za kigeni ilifikia Dola za Kimarekani milioni 3,551.3 ikilinganishwa na dola za Kimarekani milioni 2,872.6 mwezi Desemba, 2008. Kiasi hiki ni sawa na uwezo wa uagizaji wa bidhaa na huduma kwa miezi 5.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenendo wa Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali Julai-Desemba 2009; Mapato ya Ndani: Mwenendo wa mapato ya ndani kwa kipindi cha Julai – Desemba 2009 umeonesha kuwa chini ya malengo yaliyokusudiwa, hii imechangiwa

zaidi na athari zitokanazo na msukosuko wa kiuchumi, pamoja na kupungua kwa kasi ya uagizaji bidhaa za malighafi na kupungua kwa thamani ya mauzo nje ya nchi, pamoja na ukame kwa baadhi ya maeneo nchini ambao umeathiri jitihada za ukusanyaji mapato. Katika kipindi hiki, jumla ya shilingi milioni 2,291,155 zilikusanywa, sawa na asilimia 90 ya lengo la kukusanya shilingi milioni 2,540,769.7, sawa na upungufu wa shilingi milioni 249,614.7 Hali hiyo imetokana na baadhi ya vyanzo vya kodi kutofanya vizuri. Maeneo ambayo hayakufanya vizuri ni pamoja na: Ushuru wa Forodha; Ushuru wa Bidhaa za ndani na kutoka nje; Kodi ya Ongezeko la Thamani pamoja na Mapato Yasiyo ya Kodi. Aidha, katika kipindi hicho, misamaha ya kodi iliyotolewa ilifikia kiasi cha shilingi bilioni 324.14.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya misaada na mikopo ya bajeti *(GBS)* katika kipindi hiki ilikuwa shilingi milioni 785,324.4 ambazo ni asilimia 78.7 ya makadirio ya shilingi milioni 997,264 katika kipindi hicho. Kiwango hiki ni asilimia 66 ya malengo ya mwaka 2009/10. Wafadhili waliokwishatoa misaada yao ya bajeti hadi Oktoba ni Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)*, Uingereza, Sweden, Norway, Ireland, Switzerland, Denmark, Canada na Finland. Wafadhili ambao hawajatoa fedha zao hadi Desemba, 2009 ni, Japan na Ujerumani. Hata hivyo, baadhi ya wafadhili wameamua kupunguza au kuondoa kabisa misaada waliyokuwa wameahidi hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafadhili waliopunguza fedha zao ni Serikali ya Uingereza ambayo imepunguza paundi za Uingereza milioni 10 (shilingi bilioni 20) na Benki ya Dunia ilipunguza dola za Kimarekani milioni 10 ya ahadi yao. Hii ni kutokana na wahisani hao kutoridhishwa na mafanikio ya juhudi zetu katika kuboresha mazingira ya kufanya biashara Tanzania *(Doing Business)*. Aidha, mwanzoni mwa mwaka huu Serikali ya Uholanzi ilisitisha msaada wake wa *GBS* wa dola za kimarekani 40 milioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine, misaada na mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo (ikijumuisha Mfuko wa *Basket*) ilifikia shilingi milioni 847,197.7 sawa na asilimia 86 ya makadirio katika kipindi hicho. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 178,973 ni misaada na mikopo ya *Basket* ikilinganishwa na makadirio ya shilingi milioni 310,613.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai – Desemba 2009, jumla ya matumizi halisi yalikuwa shilingi milioni 4,283,601 sawa na asilimia 88 ya makadirio ya shilingi milioni 4,866,669. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 3,036,661 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi milioni 1,246,940 ni matumizi ya maendeleo. Malipo ya mishahara ya watumishi wa Serikali kwa kipindi cha Julai – Desemba 2009 yalikuwa shilingi milioni 840,854 sawa na asilimia 96 ya makadirio ya shilingi milioni 875,427.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo ya riba kwa madeni ya ndani yalifikia shilingi 92,931 milioni katika kipindi cha Julai-Desemba 2009 sawa na asilimia 69 ya lengo la kulipa shilingi 134,987 milioni katika kipindi hicho. Kwa upande wa madeni ya nje, jumla ya shilingi 18,269.7 milioni zilitumika kulipia riba ikilinganishwa na makadirio ya shilingi 25,177 milioni, na shilingi 345,255 milioni zililipa deni halisi. Aidha, malipo

kwa ajili ya madeni mengine yalikuwa shilingi 169,301 milioni sawa na asilimia 70 ya makadirio ya shilingi 237,253 milioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi mengineyo katika Wizara, Idara, Taasisi za Serikali, Mikoa na Halmashauri katika kipindi cha Julai-Desemba 2009 yalifikia shilingi milioni 1,762,136 ikiwa ni asilimia moja zaidi ya makadirio katika kipindi hicho. Mwenendo huu umechangiwa na malipo kwa ajili ya kusambaza chakula kutoka Mikoa yenye ziada kwenda Mikoa yenye uhaba, malipo ya madai ya Walimu na malipo kwa ajili ya tatizo la umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya matumizi ya maendeleo kwa kipindi cha Julai - Desemba 2009 yalikuwa shilingi 1,246,940 milioni sawa na asilimia 85 ya makadirio ya shilingi 1,472,469 milioni. Matumizi ya maendeleo kwa fedha za ndani yalikuwa shilingi 455,712 milioni sawa na asilimia 88 ya makadirio ya shilingi 519,617 milioni. Hii inatokana na kuwahi kulipia gharama za miradi mbalimbali. Matumizi ya maendeleo fedha za nje yalikuwa shilingi 791,228 milioni sawa na asilimia 83 ya makadirio ya shilingi 952,852 milioni. Kiambatisho B kinaonesha mwenendo wa mapato na matumizi katika kipindi cha Julai – Desemba 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti katika nusu ya Kwanza ya Mwaka 2009/2010 ni kama ifuatavyo:-

(a) Nishati: -

Ili kukabiliana na upungufu wa umeme nchini ambao ulisababishwa na ukame, Serikali ilitumia shilingi 28 bilioni kukabiliana na hali hiyo. Baadhi ya shughuli muhimu zilizofanyika katika kipindi hiki ni pamoja na;

(i) Mitambo ya *IPTL* iliwezeshwa kuzalisha umeme ili kukabiliana na tatizo la upungufu wa nishati ya umeme. Hivi sasa mitambo 8 kati ya 10 inazalisha umeme. Kiasi cha unit za umeme MWh 36,472 zimeingizwa katika gridi ya Taifa na hivyo kuondoa mgao wa umeme uliokumba Taifa;

(ii) Mradi wa upelekaji umeme Makao Makuu ya wilaya za Kilolo na Bahi umekamilika. Aidha, upelekaji umeme Wilaya za Uyui na Kilindi upo kwenye hatua za mwisho;

(iii) Kuendelea kukamilisha majadiliano ili kutekeleza mradi wa gesi wa Mnazi Bay;

(iv) Serikali imeendelea na ukaguzi wa madini kwenye migodi mikubwa; na

(v) Kukamilisha tafiti mbalimbali kuhusu vyanzo vingine vya nishati ya umeme inayotokana na jua na upepo nchini.

(b) Miundombinu: -

Barabara kuu na za mikoa zenye urefu wa km 90 ziliwekwa lami. Aidha, jumla ya kilometa 13,482 za barabara za wilaya zimetengenezwa. Katika kazi hiyo, Serikali ilitumia kiasi cha shilingi bilioni 118.8.

(c) Kilimo:-

Wakulima wameendelea kunufaika na ruzuku ya pembejeo za kilimo. Jumla ya vocha 4,501,100 za ruzuku (1,500,000 ni za mbolea aina ya *phosphate* na 1,501,100 ni za aina ya UREA, 1,250,000 ni za mbegu bora ya mahindi, 220,000 ni za mahindi na 30,000 ni za mpunga) za pembejeo zimeuzwa kwa wakulima katika mikoa 11:-

(i) Uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara umeendelea katika maeneo mbalimbali hasa ambayo yamepata mvua za vuli za kutosha. Ni matarajio ya Serikali kwamba msimu wa mavuno utawezesha kupatikana mazao ya chakula na biashara kama mpunga, mahindi, maharage, pamba, korosho, chai kahawa, n.k katika kiwango cha kuridhisha;

(ii) Tani 64,546 za mahindi na tani 271 za mtama zilinunuliwa na Serikali kwa ajili ya kuongeza akiba ya chakula. Aidha, tani 84,057 za nafaka zilisambazwa kwa wananchi wenye upungufu mkubwa wa chakula;

(iii) Eneo la kilimo cha umwagiliaji liliongezeka kutoka hekta 289,245 mwaka 2007 hadi hekta 310,745 Juni, 2009;

(iv) Matrekta makubwa 472, madogo *(power tillers)* 495 na majembe 62,194 ya kukokotwa na ng'ombe yaliingizwa nchini kwa ajili ya kuchochea uzalishaji katika kilimo, Kwa kupitia miradi ya *DADPs*, baadhi ya Halmashauri zimewanufaisha wakulima kuchangia gharama za upatikananji wa matrekta 49, *power tillers* 166 na majembe 81 ya kukokotwa na ng'ombe,

(v) Uzalishaji wa chakula ulifikia tani millioni 10.87 mwaka 2008 ikilinganishwa na mahitaji ya Taifa ya tani millioni 10.33;

(vi) Wakulima 230,155 na wafugaji 47,284 walipatiwa mafunzo yaliyohusisha uundaji wa vikundi, uundaji na uendeshaji wa *SACCOS* na utunzaji wa kumbukumbu;

(vii) Katika kipindi cha Julai – Desemba, tani 172.72 za mbegu bora zilizalishwa kwenye taasisi za utafiti, na aina 39 za mbegu zilizoboreshwa zilisambazwa. Aidha, tani 488 zilinunuliwa kutoka mashamba ya Jeshi la Kujenga Taifa na Magereza.

(d) Umwagiliaji:-

(i) Uchimbaji wa visima na ufungaji wa pampu ulikamilika katika Wilaya za Same, Kiteto, Maswa, Magu, Bunda na Tarime; na

(ii) Ujenzi wa mabwawa katika maeneo ya Nyashitanda, Salama Kati, Bulenya, Masuguru, na Nyambele umefikia wastani wa asilimia 57.

(e) Programu ya Maji Safi na Majitaka Mijini:-

(i) Katika kuboresha huduma za maji Jijini Dar es salaam mabomba ya urefu wa km 210 kati ya km 290 yamelazwa katika maeneo ya Kibaha na mabomba ya urefu wa km 241 yamelazwa na wateja 12,158 wameunganishiwa maji katika maeneo ya Changanyikeni, Makongo, Ubungo, Kimara Baruti, Temboni, Kwa Msuguri, Stopover na Kimara;

(ii) Ujenzi wa mradi wa Mpwapwa na Utete unaendelea na umekamilika kwa asilimia 70; na

(iii) Wateja 6,100 wameunganishwa kwenye mfumo mpya wa maji katika mji wa Kahama na wateja 7,650 wameunganishwa, katika mji wa Shinyanga.

(f) Elimu:-

(i) Kuongezeka kwa kiwango halisi cha uandikishaji wa wanafunzi katika Shule ya Msingi kutoka 96.1 mwaka 2006 hadi asilimia 97.2 mwaka 2008. Kiwango cha ukatishaji masomo kilishuka kutoka asilimia 3.4 mwaka 2006 hadi asilimia 3.1 mwaka 2008. Aidha, kiwango halisi cha uandikishaji kidato cha kwanza hadi cha nne pia kilipanda kutoka asilimia 13.4 mwaka 2006 hadi 20.7 mwaka 2007;

(ii) Kuongezeka kwa wanafunzi wanaojiunga na Shule za Awali kutoka wanafunzi 795,011 (kati yao wasichana ni 438,025) mwaka 2008 hadi 896,146 mwaka 2009 (kati yao wasichana ni 450,279);

(iii) Kuongezeka kwa wanafunzi wanaojiunga na Shule za Msingi kutoka 8,410,094 (kati yao wasichana ni 4,148,263) mwaka 2008 hadi 8,441,553 (kati yao wasichana ni 4,192,789) mwaka 2009;

(iv) Kuongezeka kwa wanafunzi wanaojiunga na Shule za Sekondari kutoka 438,901 (wavulana 252,116 na wasichana 186,785) mwaka 2008 hadi 524,784 (wavulana 290,696 na wasichana 234,088) mwaka 2009 sawa na ongezeko la asilimia 19.6;

(v) Wanafunzi wanaojiunga na Vyuo vya Ualimu waliongezeka kutoka 16,700 (kati yao wanawake ni 7,491) mwaka 2008 hadi 21,709 (kati yao wanawake ni 9,300) mwaka 2009;

(vi) Idadi ya wanafunzi wanaofadhiliwa na Serikali iliongezeka kutoka 174,946 mwaka 2008 hadi 215,643 mwaka 2009; na

(vii) Idadi ya wanafunzi wanaojiunga na Vyuo Vikuu iliongezeka kutoka 82,508 kipindi cha 2007/08 hadi wanafunzi 95,525 kipindi cha 2008/09. Katika ongezeko

hilo, asilimia 34 walikuwa wanawake na imesababishwa na ongezeko la udahili wa wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Dodoma.

(g) Afya:

(i) Kupungua kwa vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano kutoka watoto 112 kati ya 1000 waliozaliwa hai mwaka 2004/05 hadi kuifikia 91 kati ya 1000 waliozaliwa hai mwaka 2008. Vifo vya watoto wachanga chini ya mwaka mmoja vimepungua kutoka 68 kati ya watoto 1,000 waliozaliwa hai mwaka 2004/05 kufikia 58 kati ya watoto 1,000 mwaka 2008;

(ii) Kupungua kwa maambukizi ya virusi vya ukimwi kutoka asilimia 7.0 mwaka 2006 hadi asilimia 5.7 mwaka 2008. Aidha, maambukizi mapya kwa vijana wenye umri kati ya miaka 15-24 yanaonesha kupungua kutoka asilimia 3.5 mwaka 2007 hadi asilimia 2.4 mwaka 2008;

(iii) Idadi ya vituo vya afya imeongezeka kutoka 4,984 mwaka 2008 hadi 5,422 mwaka 2009;

(iv) Vifaa vya kisasa kama vile *Magnetic Resonance Imaging (MRI), CT Scan* na vifaa vya kutoa huduma za upasuaji wa moyo zinapatikana katika Hospitali ya Taifa Muhimbili;

(v) Idadi ya wanafunzi wanaojiunga na masomo katika Taasisi za Afya imeongezeka kutoka 3,831 mwaka 2008 hadi 4,147 mwaka 2009;

(vi) Ajira katika sekta ya afya imeongezeka kwa wafanyakazi 3,100 tangu mwaka 2008 hadi 2009; na

(vii) Chanjo zifuatazo zilitolewa: 1,378,404 (ikiwa ni asiliimia 88% ya malengo) kwa *Diptheria Pertusis Tetanus Hepatitis B (DPTHB)* na 1,368,700 (88%) kwa surua.

(h) Ajira:

Hadi kufikia Desemba 2008, jumla ya ajira mpya 1,271,923 zilianzishwa katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa MKUKUTA, Mwezi Juni, 2010 ni mwisho wa utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya MKUKUTA. Katika awamu hiyo, taarifa za utekelezaji zimekuwa zikitolewa ikiwa ni pamoja na Taarifa ya kila Mwaka ya Utekelezaji wa MKUKUTA *(MKUKUTA Annual Implementation Report –MAIR)* na Ripoti ya Umaskini na Maendeleo ya Watu *(Poverty and Human Development Report –*

PHDR) itolewayo kila baada ya miaka miwili. Taarifa hizi zimekuwa msingi wa majadiliano na wadau mbalimbali na kutoa maoni yanayolenga kuleta ufanisi na kufikia malengo yanayotarajiwa.

Pamoja na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya MKUKUTA, mafanikio mbalimbali yamepatikana. Nachukua fursa hii kutoa muhtasari wa mafanikio na changamoto zilizojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni kama ifuatavyo:-

(i) Ukuaji wa Pato la Taifa kwa wastani ulikuwa asilimia 7.2 kwa mwaka,

(ii) Ongezeko la mapato ya ndani kwa wastani wa shilingi 177.1 bilioni kwa mwezi, mwaka 2005/06 hadi shilingi 357.8 bilioni mwaka 2008/09;

(iii) Kuboreka kwa hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kutoka asilimia 73.0 mwaka 2006/07 hadi asilimia 83 mwaka 2008/09. Upatikanaji wa maji safi vijijini umeongezeka kutoka asilimia 53.7 mwaka 2006/07 na kufikia asilimia 58.3 mwaka 2008/09. Aidha, upatikanaji wa maji safi na salama kwa mkoa wa Dar es Salaam umeongezeka kutoka asilimia 50 mwaka 2005 hadi asilimia 68 mwaka 2008;

(iv) Kuongezeka idadi ya wanawake katika ngazi za maamuzi hadi asilimia 29 kwa mwaka 2008;

(v) Kuongezeka kwa uwajibikaji katika usimamizi wa fedha za umma na kuongezeka kwa uwazi katika ugawaji wa rasilimali katika Mikoa na Halmashauri;

(vi) Kukua kwa demokrasia kwa kuendesha chaguzi mbalimbali zikiwemo za mamlaka za Serikali za Mitaa kwa amani, utulivu na kwa kuzingatia vipindi kwa mujibu wa sheria; na

(vii) Kuimarisha uhuru wa maoni ya wananchi na kuzingatia utawala wa sheria kwa kutoingilia uhuru wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya MKUKUTA umekabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo:-

(I) Uboreshaji wa uzalishaji katika sekta ya kilimo na kusindika mazao;

(iI) Uboreshaji na upatikanaji wa huduma za mikopo ya kilimo kwa wakulima;

(iIi) Uboreshaji wa upatikanaji wa nishati ya umeme wa uhakika;

(iV) Uboreshaji wa sekta ya usafirishaji hasa barabara, reli na bandari;

(v) Kuboresha huduma za jamii (elimu, afya na maji) na uwiano sawa katika ngazi zote lengo likiwa hasa ni: kuwa na elimu bora, kupunguza vifo vya mama wajawazito na kuongeza upatikanaji wa maji safi na salama mijini na vijijini;

(vI) Kuboresha utendaji kazi kwa kuendeleza rasilimali watu katika sekta zote;

(viI) Uduni wa miundombinu muhimu kwa wasimamizi wa sheria kama vile Mahakama, Polisi na Magereza;

(viIi) Uimarishaji wa mazingira ya biashara ili kuwezesha upatikanaji wa ajira binafsi;

(iX) Upanuzi wa wigo wa mauzo ya mazao nje ili kutumia fursa zilizopo katika soko la kimataifa;

(x) Uongezaji wa thamani ya bidhaa zinazozalishwa nchini;

(xI) Kuimarisha zaidi mifumo ya usimamizi wa fedha za umma;

(xiI) Ushirikishwaji wadau binafsi na asasi za kijamii katika hatua ya kupanga mipango ya maendeleo;

(xIII) Kuboresha hali ya maisha kwa makundi maalum; na

(xiV) Uimarishaji wa mifumo ya ufuatiliaji katika ngazi zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nilizozitaja hapo juu, zimezingatiwa katika uandaaji wa Awamu ya Pili ya MKUKUTA. Awamu ya Pili ya MKUKUTA, itaendelea kuzingatia zaidi matokeo na kubaki na nguzo kuu tatu. Msukumo zaidi utakuwa katika ukuaji wa uchumi bila kuathiri huduma nyingine za kijamii. Aidha, Mkakati huu utaainisha maeneo ya kipaumbele, kuoanisha matokeo na njia za kufikia matokeo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa hatua zilizochukuliwa katika kukabili athari za msukosuko wa kiuchumi Katika Bunge la Bajeti mwezi Juni 2009, nilieleza madhara yatokanayo na msukosuko wa kiuchumi duniani kwenye uchumi wetu. Baadhi ya athari zitokanazo na msukosuko huo ni pamoja na: kupungua kwa kasi ya ukuaji wa Pato la Taifa ambapo inatarajiwa kuwa Pato la Taifa litashuka kutoka asilimia 7.4 mwaka 2008 hadi kufikia asilimia 5.0 mwaka 2009; kuongezeka kwa mfumuko wa bei hadi kufikia tarakimu mbili; kushuka kwa thamani ya shilingi kwa Dola ya Kimarekani kulikosababishwa na watu kuhodhi fedha za kigeni; kushuka kwa mapato ya Serikali kulikotokana na kupungua kwa bidhaa zilizoagizwa kutoka nje, na kupungua kwa ajira katika baadhi ya shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kuwa niliainisha hatua ambazo Serikali ilikusudia kuchukua kukabiliana na athari za msukosuko huo ikiwemo uandaaji wa mpango wa dharura, na wa muda wa kati ambao unajumuisha:-

(i) kufidia hasara waliyopata wanunuzi wa mazao msimu wa 2008/09;

(ii) kutoa udhamini wa kuahirisha ulipaji wa mikopo ya waathirika wa msukosuko;

(iii) kutoa mitaji ya uendeshaji *(working capital)* kwa riba nafuu;

(iv) Kuboresha Mifuko ya Dhamana;

(v) kuhakikisha upatikanaji wa chakula;

(vi) kulinda uwekezaji muhimu hasa katika miundombinu ili kuendeleza ukuaji wa uchumi na Malengo ya *Milenia*; na

(vii) kutoa ruzuku kwenye bei ya mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tahadhari ambazo Serikali ilichukua zimesaidia kupunguza athari mbaya ambazo zingeweza kujitokeza endapo hatua hizo zisingechukuliwa. Ni matumaini ya Serikali kwamba hatua za muda wa kati zinatuweka katika nafasi nzuri ya kuimarisha uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hatua zilizochukuliwa, naomba kutoa taarifa ya utekelezaji kwa baadhi ya maeneo hadi kufikia mwezi Desemba 2009 kama ifuatavyo:-

(i) Kiasi cha shilingi bilioni 19.9 kililipwa kama fidia kwa wanunuzi wa pamba ikilinganishwa na lengo la shilingi 21.9 bilioni. Mchakato unaendelea kulipa kiasi kilichosalia;

(ii) Jumla ya shilingi bilioni 15.8 zilitolewa kama dhamana kwa mabenki kwa ajili ya kuwawezesha wakopaji kurudisha mikopo. Lengo la hatua hii ni kuwawezesha wakopaji kupata mikopo mipya kwa ajili ya shughuli za ununuzi wa mazao kwa msimu wa 2009/10;

(iii) Ruzuku ya jumla ya shilingi bilioni 20.0 ilitolewa kuboresha bei ya pamba kwa wastani wa shilingi 80 kwa kilo moja;

(iv) Jumla ya shilingi bilioni 12.4 zilitolewa kwa lengo la kuboresha mifuko ya dhamana (*Export Credit Guarantee Scheme* na *SMEs*);

(v) Jumla ya shilingi bilioni 10.0 zilitolewa kwa kampuni ya *ARTUMAS* kwa ajili ya kugharamia usambazaji wa umeme katika mikoa ya Lindi na Mtwara kama mkopo kupitia Benki ya Rasilimali Tanzania- *TIB*;

(vi) Serikali ilitoa ruzuku ya pembejeo kwa wakati kwa kushirikisha Mikoa yenye uwezo wa kuzalisha chakula kwa wingi, kuongeza wataalamu wa ugani na kusambaza chakula kutoka maeneo yenye ziada kwenda kwenye maeneo yenye uhaba;

(vii) Serikali imeendelea kusimamia na kufuatilia kwa karibu utendaji wa benki na taasisi za kifedha, ili kuhakikisha Sekta ya fedha haitetereki. Aidha, benki na taasisi za fedha zinahimizwa kuendelea kukopesha wazalishaji; na

(viii) Serikali ilipokea dola za Kimarekani milioni 245 kutoka IMF kupitia mpango wa *"Exogenous Shock Facility"* Juni, 2009 ili kusaidia mizania na malipo ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza hapo awali, kuna kila dalili kwamba uchumi katika nchi mbalimbali ikiwemo Tanzania umeanza kuonyesha mwelekeo mzuri. Kwa upande wetu ukuaji wa Pato la Taifa kwa robo ya kwanza na ya pili ya mwaka 2009 unaonesha kuzidi asilimia 5, kiwango ambacho kinategemewa kwa mwaka huo. Uzalishaji katika sekta chache ikiwemo ya viwanda umeanza kuongezeka japo kwa viwango vidogo. Aidha, ukuaji wa sekta ya huduma za mawasiliano na uchukuzi, kilimo, huduma za fedha nazo zimeonyesha dalili nzuri katika ukuaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na dalili hizo njema za kuimarika kwa uchumi, bado kuna maeneo ambayo yanakabiliwa na matatizo yaliyotokana na msukosuko wa kiuchumi duniani. Serikali itaendelea kutekeleza baadhi ya hatua zilizochukuliwa na Serikali chini ya Mpango wa Kunusuru uchumi katika mwaka ujao wa fedha. Baadhi ya hatua hizo ni pamoja na zifuatazo:-

(i) Kuharakisha uanzishwaji wa Benki za Rasilimali na Kilimo zitakazotoa mikopo ya muda mrefu na kwa riba nafuu**.** Tayari mchakato wa kuanzisha vyombo hivi viwili uko katika ngazi ya uamuzi na kutafuta washiriki hasa *China Development Bank.* Dirisha la kilimo tayari limefunguiliwa katika Benki ya Rasilimali na kwamba taratibu za uendeshaji wa dirisha umeandaliwa.

(ii) Benki Kuu kuruhusu kuongezeka kwa Ukwasi, Benki kuu kuendelea kuruhusu kuongezeka kwa ukwasi katika uchumi ili mikopo iweze kutolewa kwa riba nafuu kwa:

· Kupunguza riba katika dhamana za serikali kwa kupunguza mauzo ya dhamana jambo ambalo limesababisha kushuka kwa riba za dhamana za Serikali kutoka asilimia 13.3 mwezi Machi 2009 hadi asilimia 9.7 katika wiki ya pili ya Mei 2009; na

· Kupunguza riba ya kukopesha mabenki kwa muda mfupi (kila siku) na kipindi cha miezi mitatu.

(iii) Kukamilisha Sera ya "*Public Private Partinership - PPP"*, Kuharakisha ukamilishaji wa Sera ya *PPP* na kanuni zake ili ianze kutumika. Aidha, itabidi kuchagua miradi michache inayoweza kugharimiwa kwa ushirikiano baina ya serikali na sekta binafsi *(PPP projects)* kwenye miundombinu.

(iv) Kulinda uwekezaji muhimu hasa katika miundombinu ili kuendeleza ukuaji wa uchumi na malengo ya milenia, katika eneo hili kuna malengo makuu mawili: (i) kuepuka kusitisha mipango ya uwekezaji inayolenga kutumia nafasi nzuri ya Tanzania kimaliasili na kijiografia hususan miundombinu na kilimo; (ii) kulinda mafanikio tuliyopata kwenye kufikia malengo ya milenia ya ustawi wa jamii katika elimu na afya na kuhakikisha kuwepo kwa uwekezaji fanisi na wa kutosha katika miundombinu ya sekta hizi na fedha za kutosha za uendeshaji.

(v) Kulinda mipango ya kijamii, kuendeleza mipango ya kijamii kulingana na malengo yake ya awali. Hii inajumuisha mipango ya:-

· Utoaji wa ruzuku kwa dawa za kurefusha maisha kwa wagonjwa wa UKIMWI, vyandarua vya kuzuia malaria, programu za kifua kikuu na magonjwa ya milipuko;

· Kuendeleza programu za vijana ili kuhakikisha utulivu wa kijamii na kujenga uwezo wa siku za baadaye; na

· Kuendeleza programu maalumu za kulinda watu walio katika makundi tete – yaani programu za ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zilizochukuliwa kukabiliana na mabadiliko ya Tabia Nchi. Katika kipindi cha hivi karibuni, nchi yetu imekabiliwa na mabadiliko ya Tabia nchi ambayo yamesababisha ukame na mafuriko yaliyoleta maafa kwa binadamu na mali zao, wanyama na mimea katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** tumeshuhudia wananchi wakipoteza maisha, kupoteza mali zao ikiwemo uharibifu wa nyumba, na hivyo kushindwa kujikimu. Tumeshuhudia uharibifu wa mashamba na miundombinu mbalimbali ikiwemo madaraja, barabara na reli. Aidha, katika baadhi ya wilaya kumejitokeza tatizo la njaa ambalo linahitaji hatua za haraka ili kuweza kuwanusuru wananchi waliokabiliwa na tatizo hilo. Serikali imeanza kuchukua hatua za dharura kukabiliana na maafa hayo. Baadhi ya hatua zilizochukuliwa ni pamoja na:-

(i) Kutafuta fedha za kukarabati miundombinu iliyoathirika ya reli, barabara na madaraja, kazi ambayo itatekelezwa kwa ushirikiano na vikosi vya ulinzi na usalama. Nia ya Serikali ni kuhakikisha ukarabati wa miundombinu hiyo unafanyika kwa manufaa ya uchumi wetu na wa nchi jirani;

(ii) Kununua mazao ya chakula na kuyasambaza katika maeneo yaliyoathirika na matokeo ya tabia nchi; na

(iii) Kuhamasisha wananchi, wahisani na makundi mbalimbali ya jamii kusaidia kwa hali na mali walioathirika. Kwa kipindi kifupi tumeshuhudia matokeo ya kuridhisha kwa namna Taasisi zinavyojitokeza kutoa misaada ya aina mbalimbali. Kwa niaba ya Serikali nachukua nafasi hii kushukuru Taasisi zote na wahisani na vikundi mbalimbali vya kijamii kwa misaada yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya mpango wa muda wa kati wa 2010/11 – 2012/13 yamegawanyika katika maeneo makuu yafuatayo: -

- Shabaha na malengo ya uchumi-jumla;
- Utambuzi wa maeneo ya vipaumbele; na
- Mwelekeo wa mapato na matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo ya uchumi jumla kwa kipindi cha 2010/11-2012/13 ni kama ifuatavyo:-

(i) Kasi ya ukuaji wa Pato halisi la Taifa itaongezeka kutoka matarajio ya asilimia 5.0 mwaka 2009 hadi asilimia 6.1 mwaka 2010, asilimia 6.6 mwaka 2011, asilimia 7.1 mwaka 2012 na asilimia 7.6 ifikapo mwaka 2013 kutokana na baadhi ya sekta kuanza kufanya vizuri;

(ii) Kuwa na kiwango cha kasi ya upandaji bei chini ya asilimia 10 ifikapo mwezi Juni 2011;

(iii) Mapato ya ndani yanatarajiwa kuwa asilimia 15.5 ya Pato la Taifa mwaka 2010/11, asilimia 15.9 mwaka 2011/12 na kufikia asilimia 16.1 mwaka 2012/13;

(iv) Kudhibiti ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) kwa kiwango kisichozidi asilimia 23.9 ambacho kitawiana na malengo ya ukuaji wa uchumi na kupunguza kasi ya upandaji bei; na

(v) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya vipaumbele katika mpango na Bajeti 2010/11 – 2012/13. Wakati ninawasilisha Mwongozo wa Mpango na Bajeti wa mwaka 2009/10 – 2011/12, Waheshimiwa Wabunge walipendekeza Serikali iainishe vipaumbele vichache na kuvitengea fedha za kutosha badala ya kutawanya fedha kidogo kwenye maeneo mengi. Kwa kuzingatia ushauri huo, Serikali imeainisha maeneo machache ya vipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya kipaumbele katika mwongozo wa Mpango na Bajeti yataendelea kutekelezwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005; Malengo ya Milenia; Mpango wa Muda wa Kati wa Uwekezaji wa Umma (MKUU) na MKUKUTA chini ya kaulimbiu ya KILIMO KWANZA. Maeneo ya vipaumbele ni yafuatayo:-

I. Kilimo na Maendeleo ya Mifugo

· Maeneo yatakayohusika ni umwagiliaji, uvuvi, kilimo na mifugo

II. Miundombinu

· Maeneo yatakayohusika ni barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege na nishati

III. Huduma za jamii

· Maeneo yatakayohusika ni Elimu, Maji na Afya

IV. Ardhi

· Kuanzisha vituo vya kitaifa vitakavyosaidia upimaji wa ardhi na uchoraji ramani;

· Utekelezaji wa mipango ya kitaifa ya matumizi bora ya ardhi ikijumuisha Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi katika wilaya na programu nyinginezo; na

· Kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika miji ili kukabiliana na changamoto za ukuaji wa miji nchini.

V. Viwanda

· Kuendeleza wajasiriamali wadogo na wa kati;

· Kuendeleza na kuhamasisha matumizi ya teknolojia rahisi na sahihi ya viwanda inayolinda mazingira;

· Kuendeleza viwanda mama ikiwa ni pamoja na mradi wa chuma Liganga na mradi wa Makaa ya Mawe wa Mchuchuma; na

· Kuendeleza Kanda Maalumu za Uzalishaji kwa ajili ya kuuza nje *(Export Processing Zones)* kwa kushirikisha sekta ya umma na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha miradi ya miundombinu inatekelezwa, Serikali inaendelea na maandalizi ya kukopa kutoka katika masoko ya mitaji nje na ndani ya nchi. Katika kufanikisha azma hii, Serikali inatarajia kukopa kupitia mpango wa *"Sovereign/ State bond"* ambao kwa sasa umeonesha dalili nzuri ya kutengamaa kwa riba

katika masokoya mitaji. Hii itasaidia kupunguza utegemezi kutoka kwa washirika wetu wa maendeleo. Ieleweke kuwa fedha zinazotafutwa ni kwa ajili ya miradi ya miundombinu hasa barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege na nishati

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza maeneo ya vipaumbele vya kitaifa yaliyotajwa hapo juu, Wizara, Idara zinazojitegemea, Mikoa na Serikali za Mitaa zitaainisha vipaumbele kulingana na majukumu yao ili kuandaa mipango na bajeti ya mwaka 2010/11 – 2012/13.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** mwaka huu ni mwaka wa Uchaguzi Mkuu ambao utafanyika mwezi Oktoba 2010. Ili kuhakikisha uchaguzi huo unafanyika kwa amani na utulivu, Serikali itatenga fedha za kutosha kufanikisha uchaguzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** mwelekeo wa Bajeti ya Serikali katika kipindi cha 2010/11 – 2012/13 utazingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika kipindi cha muda wa kati pamoja na malengo ya Awamu ya Pili ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania. Aidha, mwelekeo huu umezingatia umuhimu wa kuharakisha mapinduzi ya kijani kwa kutekeleza nguzo kuu za KILIMO KWANZA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapato, Sera za Mapato, Serikali itaendeleza ukusanyaji wa mapato katika mwaka 2010/11 kwa kuzingatia sera kama ilivyokuwa kwa mwaka 2009/10. Aidha, vianzio vipya vya mapato vitabuniwa katika maeneo ya kodi na yasiyo ya kodi. Serikali imeshatoa tangazo la kuzitaka Taasisi mbalimbali na sekta binafsi kuwasilisha mapendekezo yao ya Sera za Kodi kwa mwaka 2010/11. Kikosi Kazi cha Maboresho ya Kodi *(Task Force on Tax Reform)* kitaanza kushughulikia mapendekezo hayo na kuishauri Serikali ipasavyo kuanzia mwezi Machi, 2010. Hatua mbalimbali zitaendelea kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na kupunguza mianya ya ukwepaji kodi, kudhibiti misamaha ya kodi na kuimarisha usimamizi wa mizigo inayopita hapa nchini kwenda nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia Sera za Mapato kama ilivyoelezwa hapo juu, Serikali inategemea kukusanya mapato ya ndani ya asilimia 15.5 ya Pato la Taifa mwaka 2010/11 kulingana na kasi ya ukuaji wa uchumi. Misaada inatarajiwa kuwa asilimia 5.8 mwaka 2010/11 na Mikopo kutoka kwa wahisani inatarajiwa kuwa asilimia 4.6. Serikali inatarajia kukopa kutoka vyanzo vya ndani na nje ya nchi ili kuziba pengo la mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera za Matumizi zitalenga kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele vilivyoainishwa katika Mwongozo. Aidha, Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba matumizi yanakuwa ya tija na tunatumia kile tulichokusanya katika mwaka 2010/11 kwa kuzingatia sera ilivyokuwa kwa mwaka 2009/10. Katika mwaka 2010/11 mambo yafuatayo yatazingatiwa katika kutekeleza sera za matumizi:-

(i) Kuhakikisha kuwa Maafisa Masuhuli wote wanatenga fedha za kutosha katika majukumu yao ya msingi ikiwa ni pamoja na huduma muhimu kama vile maji,

umeme na simu na hivyo kuepuka maombi nje ya bajeti iliyoidhinishwa kwenye mafungu yao;

(ii) Maafisa Masuuli wazingatie sheria, kanuni na taratibu mbalimbali za kiutumishi na kifedha ili kuepuka kuzalisha hoja za ukaguzi na madeni;

(iii) Kuhakikisha kuwa bajeti iliyopitishwa na Bunge inatekelezwa kama ilivyopangwa ili kuepuka uhamisho wa fedha katika vifungu;

(iv) Wizara, Mikoa na Serikali za Mitaa kuendelea kudhibiti matumizi ya fedha zilizoidhinishwa, ili kutoa huduma kwa ufanisi;

(v) Kudhibiti matumizi yasiyo na tija na kutoa kipaumbele katika kulipa madeni kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za ununuzi wa umma; na

(vi) Kuendelea kuimarisha taratibu za kufuatilia utekelezaji wa mpango na bajeti *(Monitoring of Plan and Budget Execution).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgao wa fedha unaopendekezwa kwa mwaka 2010/11 ni kama ifuatavyo:-

(i) Matumizi ya kawaida yatakuwa asilimia 69; na

(ii) Matumizi ya Maendeleo yatakuwa asilimia 31.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa utayarishaji wa Mpango na Bajeti wa mwaka 2010/11-2012/13, unaelekeza upangaji wa mipango uzingatie rasilimali chache tulizonazo na kuzielekeza katika vipaumbele vichache ili kuchochea ukuaji wa uchumi na hivyo kupunguza umaskini. Kwa kuzingatia hayo, watekelezaji wanaagizwa kuzingatia yafuatayo wakati wa kuandaa Mpango na Bajeti ijayo:-

(i) Kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kugharamia kwa kiwango kikubwa zaidi utekelezaji wa mipango ya Serikali;

(iii) Kuhakikisha MKUKUTA II unazingatiwa ipasavyo katika mipango na bajeti;

(iv) Kuzingatia vipaumbele vya mpango na bajeti kama vilivyoainishwa katika Mwongozo huu;

(v)Kuhakikisha Uchaguzi Mkuu wa mwezi Oktoba 2010 unafanyika kwa amani na utulivu;

(vi) Kuharakisha utekelezaji wa mradi wa vitambulisho vya kitaifa;

(vii) Kuimarisha zaidi ushirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi *(Public Private Partnership-PPP)* ikiwa ni pamoja na kuandaa sheria ya kutekeleza sera ya *PPP*;

(viii) Kuhakikisha kuwa Maafisa Masuhuli wote wanatenga fedha za kutosha katika majukumu yao ya msingi na hivyo kuepuka maombi nje ya bajeti iliyoidhinishwa kwenye mafungu yao;

(ix) Maafisa Masuhuli wazingatie sheria, kanuni na taratibu mbalimbali za kiutumishi na kifedha ili kuepuka kuzalisha hoja za ukaguzi na madeni;

(x) Maafisa Masuhuli wanaelekezwa kulipa makato yote ya kisheria na kuwasilisha kwa wakati kwenye vyombo husika. Hii ni pamoja na michango kwa mifuko ya hifadhi ya jamii, bima, mikopo mbalimbali na kodi;

(xi) Kuendelea kutekeleza sera ya upelekaji wa madaraka kwa wananchi ili kuboresha utoaji wa huduma na kuharakisha mchakato wa maendeleo katika ngazi ya Halmashauri;

(xii) Wizara, Mikoa na Serikali za Mitaa kuendelea kudhibiti matumizi ya fedha kama zilivyoidhinishwa, ili kutoa huduma kwa ufanisi;

(xiii) Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ziendelee kubaini fursa za maendeleo zinazovutia uwekezaji wa sekta binafsi pamoja na kuwahamasisha wananchi wawekeze zaidi ili kuongeza kasi ya maendeleo;

(xiv) Serikali za Mitaa zinaagizwa kukusanya maduhuli na kuwasilisha taarifa za makusanyo kwa kila robo mwaka OWM-TAMISEMI na Hazina;

(xv) Kudhibiti matumizi yasiyo na tija na kutoa kipaumbele katika kulipa madeni kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za ununuzi wa umma;

(xvi) Ununuzi wa magari na uendeshaji wa semina na makongamano utaendelea kufanyika kwa idhini kutoka kwa Waziri Mkuu;

(xvii) Wizara zihakikishe mashirika na taasisi za umma zilizo chini yao zinakusanya maduhuli ipasavyo na kuwasilisha katika Mfuko Mkuu wa Serikali;

(xviii) Kuhakikisha ununuzi wa samani zenye ubora na imara (kipaumbele kiwe kwa samani zinazotengenezwa nchini) kulingana na thamani halisi ya fedha katika maeneo husika kwa kuzingatia kanuni na taratibu;

(xix) Kuongeza kasi ya kutekeleza Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania katika Wilaya ambazo mpango umeanza; na

(xx) Kuendelea kuimarisha taratibu za kufuatilia utekelezaji wa mpango na bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kwa kuwa Bunge na Kamati zake ni vyombo muhimu vya kuhakikisha kwamba mpango na bajeti inatekeleza sera za kitaifa, Serikali iko tayari kupokea maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge ili kuuboresha Mwongozo huu. Aidha, napenda kusisitiza kuwa huu ni mwongozo wa uandaaji wa mipango na bajeti. Mpango na Bajeti kamili kwa mwaka 2010/11 – 2012/13 vitakuwa

tayari baada ya Wizara, Mikoa na Halmashauri husika kuandaa mipango na bajeti zao kwa kuzingatia maeneo ya vipaumbele vya Mwongozo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba kumpongeza Waziri kwa kuwasilisha hoja yake lakini wakati nipo hapa Mezani, kabla sijamuita Mwenyekiti wa Kamati, nimepokea hapa maombi ya ufafanuzi kama manne yanayohusu Muswada ule wa Sheria ambao ni Muswada wa Matumizi ya Fedha ambao Mheshimiwa Naibu Spika ameuzungumzia, walioniomba nitoe ufafanuzi wote walitumia Kanuni yetu ya Bunge namba 105.

Sasa naomba nitoe taarifa rasmi kwamba Kanuni inayotumika kwa ajili ya Matumizi ya Nyongeza ya Fedha ni Kanuni namba 107 ambayo inasema:-

"Mapendekezo yoyote kwa ajili ya Matumizi ya Nyongeza ya Fedha za Serikali au kwa ajili ya kutoa fedha yoyote ya nyongeza zaidi ya Fedha za Matumizi ya Mwaka huo:-

(a) yataitwa Makadirio ya Nyongeza ya Matumizi;

(b) yatapelekwa kwenye Kamati ya Matumizi kufuatana na masharti ya Ibara ya 99 ya Katiba; na

(c) yatafuata masharti ya Kanuni zote zinazohusu Makadirio ya Mwaka ya Matumizi ya Serikali."

Ndiyo maana tumesema kwamba ni wajibu wa Kamati inayohusika na kwa kushirikiana na Serikali kuyafanyia uchambuzi na hivyo yatakapowasilishwa Bungeni, yatafuata taratibu kwa mujibu wa Kanuni zinazohusika za makadirio ya mwaka ya matumizi ya fedha za Serikali. Kwa hiyo, ninaomba kutoa taarifa hiyo Waheshimiwa Wabunge tunaifuata Kanuni namba 107.

Baada ya kusema hayo…

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo!

MWENYEKITI: Ndiyo Mheshimiwa Mbunge.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Nilitaka kuomba muongozo wakati Mheshimiwa Naibu Spika alipotoa maelekezo yake asubuhi, umerudia hayohayo ambayo yalikuwa yananisumbua na yanayowasumbua pia Waheshimiwa Wabunge. Umesema sahihi kabisa kwamba ni kifungu cha 107 sawa kabisa lakini kifungu hicho hicho

kinakurejesha kwenye kifungu cha 105, kwa sababu hii ni *supplementary*, Serikali inakuja na maombi ya nyongeza kupitia Muswada huu ambao umegawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masharti ya Kanuni hizi ambayo yanatakiwa yatumike ni yale ambayo yanahusu makadirio ya mwaka ya matumizi ya Serikali ambayo yanasimamiwa na Kanuni ya 105 kwamba Muswada huo kwanza huwa hautangazwi kwenye Gazeti la Serikali na wala haupelekwi kwenye Kamati yoyote ya Kudumu na unapoingia kwenye Kamati ya Matumizi unapelekwa katika hatua zote tatu, hasa hapo ndiyo tunahitaji muongozo sahihi, mimi katika tafsiri yangu ni kwamba Muswada huu hauhitaji kupelekwa katika Kamati ya Fedha na Uchumi, unapaswa tu uwasilishwe hapa Bungeni na twende katika Kamati ya Matumizi ili twende katika hatua zote tatu, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Chenge, ni kweli kabisa unachokisema lakini unaona kabisa unapovipitia vifungu hivi vyote viwili kile cha 105 na 107 ambacho kinatoa tafsiri halisi ya maana ya Matumizi ya Nyongeza ya fedha ndani ya Serikali. Sasa kile cha 107 ambacho kinatoa tafsiri halisi ya *Supplimentary Appropriation Bill* chenyewe bado kinabebwa na kipengele kidogo cha (c) ambacho kinataka masharti ya kanuni zinazohusu makadirio ya mwaka ya matumizi ya Serikali yafanyike sasa kwa sababu Kanuni hizi zote mbili zinabeba dhana moja, hebu tuache tuone namna nzuri ya kulishughulikia suala hili baada ya kufanya haya maamuzi na baada ya hapo kwa mujibu wa taratibu za Bunge zitafuta taratibu nzuri za kuangalia uzoefu wa maamuzi mengine yaliyokwishafanyika na shughuli itaendelea tu kufanyika bila kuwa na matatizo yoyote. Naomba Waheshimiwa Wabunge hili wala lisiwape matatizo. Kanuni tunazo, tutatekeleza tu na shughuli itafuata utaratibu kwa mujibu wa Kanuni zetu za Bunge na kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili kuweka utaratibu wa Bunge na shughuli za Bunge uende vizuri.

Baada ya kutoa Muongozo huo, sasa namwita Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda ili aweze kutoa taarifa ya Kamati kuhusu maelekezo haya ambayo yameshatolewa na mtoa hoja.

MHE. DR ABDALLAH O. KIGODA - MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 94 ya Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, inalitaka Bunge kukaa kama Kamati ya Mipango katika Mkutano wake wa Mwezi Februari ili kujadili na kushauri kuhusu mapendekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika mwaka wa fedha unaofuata.

Katika kufanya hivyo, Kamati yangu tarehe 2 Februari, 2009, ilipata fursa ya kuchambua Mwongozo wa Utayarishaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Kipindi cha 2010/11 hadi 2012/13 uliowasilishwa na Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo (MB) na Waziri wa Fedha na Uchumi, badala ya kuchambua Mpango wa Taifa kama kanuni inavyoagiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu ilipata wakati mgumu mara ilipokutana na Wizara ya Fedha na Uchumi kuhusu dhana ya Bunge kukaa kama Kamati ya Mipango kwa maana tulishindwa kuelewa sisi kama Bunge tupate maelezo gani kutoka Serikalini na sawia Serikali itoe maelezo gani Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo linalojitokeza kwa utaratibu huu, Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa mwaka wa fedha 2010/11 ambao ni wa muda mfupi na ambao ni *operational*, maandalizi yake huwa yanakamilika mwezi April baada ya Serikali kuwasilishiwa mipango mbalimbali ya Wizara na Taasisi nyingine katika mfumo wa nchi. Hali hii ni changamoto kwa azma ya Bunge kutekeleza wajibu wake wa kuwa Kamati ya Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda tuliojiwekea wa Bunge kukaa kama Kamati ya Mipango mwezi Februari maantiki inatuonyesha tufuate moja kati ya utaratibu ufuatao:

(a) Wizara ya Fedha na Uchumi au iwasilishe maelezo ya Mpango wa Mwaka unaofuatia kutokana na Mipango yetu Mikuu tuliojiwekea; kama vile Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, MKUKUTA n.k. kwa maana hatua ya utekelezaji iliyofikiwa katika mwaka husika. Maelezo haya yatatuonyesha tunatoka wapi, tuko wapi na tunaelekea wapi, baada ya muda wa kutekeleza mipango yetu mikubwa tuliyojiwekea; ama

(b) Bunge na Serikali tuelewane vizuri maana na tafsiri ya Kanuni husika tuliyoiweka. Jinsi Kanuni ilivyoandikwa inaashiria kuwa Serikali ina mpango wake wa muda wa kati na wa muda mrefu unaohitaji kutekelezwa katika mwaka unaofuatia. Au Serikali ilete mbele ya Bunge mipango inayokusudia kuutekeleza katika mwaka unaofuata ili Bunge liupitishe au la. Hii ni changamoto kubwa kwa Bunge letu, taasisi ambayo ni endelevu.

Hatua hizi mbili ni muhimu zifanyiwe kazi na kutolewa maamuzi haraka ama sivyo Kanuni ibadilishwe kwa kuiagiza Serikali ituletee Mwongozo wa Kitaifa wa kutayarisha Mpango na Bajeti ya Serikali kwa kila mwaka, kama inavyofanyika hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kuwa utaratibu wa sasa ukiendelea tatizo litakalojitokeza ni Bunge hususan, wakati wa kuwasilisha Bajeti ya Serikali, badala ya Bunge kuwa ni sehemu ya kusimamia Serikali kuona kwamba inatekelezaje Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala, (CCM), kutokana na Mipango tuliojiwekea, pamoja na vipaumbele tulivyoviweka katika program mbalimbali itakuwa ni ukumbi wa Waheshimiwa Wabunge au wa kugombania rasilimali, miradi na kadhalika au eneo la kupanga tena mipango mingine mipya ambayo haikufanyiwa kazi na Serikali. Tija na ufanisi wa hatua na malengo ya Bunge kukaa kama Kamati ya Mipango hayatafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi tunaloendelea nalo ni kuchambua Mwongozo uliowasilishwa. Kamati inashauri kuangaliwa Mwongozo huu kwa sura ya Kitaifa '*the bigger picture'*, na moja ya changamoto ni kutathmini mahitaji ya rasilimali inayohitajika katika kutekeleza mpango ujao. Bunge lazima liwe '*focused'*. Msisitizo uwe ni kuzingatia

vipaumbele tulivyokubaliana vinavyogusa maeneo machache ambayo yataibua fursa na uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu inaamini kuwa kwa hali yoyote ile mapendekezo ya Mpango wa Taifa katika kipindi kijacho ni lazima yatokane na malengo ya Dira ya Maendeleo ya Milenia 2025 na MKUKUTA. Suala la msingi ni kwa Bunge kuelewa Dira hii ina malengo na mikakati gani na MKUKUTA unaweka mkakati, malengo na vigezo gani kufikiwa. Ipo haja ya Bunge kuelewa ni kwa kiasi gani tuko ndani ya malengo husika kiutekelezaji tunapoelekea mwaka 2025. Kwa mantiki hii mapendekezo ya Mpango wa Taifa ni lazima yawe na mtazamo na sura ya Kitaifa badala ya kuwa na sura ya kieneo au kijimbo. Hali hii lazima ionyeshwe katika Mwongozo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Mwongozo unatuelekeza kwenye taratibu za utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa na moja ya changamoto itakuwa ni rasilimali za kutekeleza mipango hiyo, Bunge lihakikishe hili linazingatiwa; Bunge lizingatie vipaumbele tulivyojiwekea ili kusaidia jitihada ya Serikali ya kuibua fursa za uchumi wa nchi yetu. Tuliamua na kuainisha maeneo matano yaani: Miundombinu, Elimu, Afya, Nishati na Kilimo kuwa ndiyo yapewe umuhimu. Bunge na Serikali hatuna budi kuwa *consistent* na *persistent* katika kuyasimamia na kuyashughulikia maeneo hayo. Haitaleta tija ikiwa tutaendelea kubadili badili vipaumbele hivi kwa kila mwaka wa bajeti. Vipaumbele hivi lazima viwe vya kitaalam badala ya kuwa vya kisiasa zaidi. Vipaumbele visiwe *imposed* au *superimposed*. Kamati imetoa ushauri huu kwa Wizara baada ya kuona kuwa vipaumbele vilivyoonyeshwa vilikuwa ni vingi, hivyo kuweza kuleta tatizo la utekelezaji hasa katika kusambaza fedha chache tulizonazo katika maeneo mengi badala ya yale tunayoyajua kama *Drivers of the Economy*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa iliyowasilishwa inaonyesha kuwa pamoja na mipango tunayopanga bado kasi ya kupunguza umaskini nchini hairidhishi. Kutokana na ukweli huu ipo haja ya makusudi ya kuhakikisha kuwa Mwongozo unaelekeza Mipango yetu ya Kitaifa ijikite zaidi kwenye maeneo ya kupunguza umaskini hasa kwa kuzingatia MKUKUTA. Nguzo zote tatu za MKUKUTA zinahakikisha kuwepo kwa jitihada za kimaendeleo ambazo ni za ufanisi ulio na uwiano mzuri wenye kuhakikisha kwamba kila mtu ananufaika na matunda ya rasilimali mpya zinazoundwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kaulimbiu ya KILIMO KWANZA na malengo yake yanafikiwa, eneo la kilimo linahitaji kuangaliwa kwa umakini katika sura zifuatazo:-

- Raslimali zinazotengwa kwa ajili ya Kilimo na Mifugo, hazina budi kuwafikia walengwa (wakulima wenyewe);

- Mipango yetu ilenge kwenye kuboresha miundombinu ya kukuza sekta ya kilimo hasa barabara vijijini;

- Sheria za Ardhi zirekebishwe ili kuruhusu uwekezaji mkubwa katika kilimo; tuimarishe kilimo kikubwa cha biashara kitakachohamasisha viwanda vya usindikaji;

- Ziongezwe hifadhi za chakula na mazao kwa kujenga maghala;

- Serikali isimamie upatikanaji wa masoko na bei nzuri za mazao kwa wakulima;

- Utaratibu wa sasa wa kusambaza madawa, mbegu bora na zana za kilimo uimarishwe ikiwa pamoja na kutoa ruzuku kwa wakulima;

- Wataalamu wa Kilimo wapewe kipaumbele kwa kuzingatia fani zao; na
- Uanzishwe mpango mkubwa wa kilimo cha umwagiliaji na uhifadhi wa maji wakati wa kiangazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya fedha si pekee kwa sekta ya kilimo, bali imekuwa ni 'si rafiki' katika kutoa huduma zake hasa kwa wakulima walio wengi pamoja na wale wenye vipato vya chini au kati. Hali hii imechangia katika kudumaza juhudi za kuibua uchumi. Mwongozo ni lazima uangalie utaratibu wa kupunguza viwango vikubwa vya riba katika mabenki yetu ili huduma hii iwafikie wazalishaji wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo moja linalohusisha misingi mikuu ya (*macro economic fundamentals)* ni lile la mfumuko wa bei. Eneo hili linawaathiri sana hususan wale wananchi wenye kipato cha chini. Hivi sasa tatizo kubwa na sugu ni lile la kupanda kwa bei ya chakula na hivyo kuendelea kupandisha mfumuko wa bei katika uchumi wetu. Kamati inashauri Serikali, Mwongozo uelekeze mipango ilenge katika kujitosheleza na kuimarisha usalama wa upatikanaji wa chakula. Ingawaje hapo awali tulipata afueni kutokana na kupungua kwa bei za mafuta katika kipindi kilichopita, hivi sasa bei za mafuta zimepanda kutoka dola za Marekani 35 hadi 80 kwa pipa. Tusipokuwa makini mfumuko wa bei unaweza kufikia viwango vya juu kuliko ilivyo sasa (asilimia 12).

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna tatizo la uwekezaji mkubwa wa viwanda na biashara katika maeneo mbalimbali nchini. Hali hii inasababishwa na kutokuwa na uhakika wa upatikanaji wa umeme kwa kipindi chote cha mwaka. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha vyanzo mbadala vya umeme vinapatikana kama vile nishati ya umeme itokanayo na makaa ya mawe, jua, upepo na madini. Mwongozo uelekeze wazi nia ya nchi kuendeleza uwekezaji mkubwa katika sekta hii kwa lengo la kuwa na akiba ya umeme nchini (*reserve*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa kuwa mwezi Juni, 2010 ni mwisho wa utekelezaji wa awamu ya kwanza ya MKUKUTA, kamati inashauri tathmini ya kina ifanywe kwa kipindi chote ili tujue wapi tulipokuwa, tupo wapi na tunaelekea wapi. Hii itasaidia katika kujiandaa na utekelezaji wa awamu nyingine. Kimsingi Mwongozo uelekeze changamoto zinazojitokeza katika MKUKUTA- I; zikatumike kurekebisha utekelezaji wa MKUKUTA- II. Bado Serikali haijaonyesha gharama za kutekeleza mpango huu kwa awamu ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kuipongeza Serikali kwa kuandaa Mwongozo ambao kwa ujumla unagusa maeneo mengi yanayoendana na vipaumbele tulivyojiwekea, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kuwa mwongozo unaelekeza mpango ambao utakuwa tayari kuhimili dharura na changamoto ambazo zitajitokeza na ambazo zimeshajitokeza: majanga ya mafuriko, uharibifu wa miundombinu, tatizo la njaa na kadhalika *(preparedness of the economy).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la huduma za jamii, hususan sekta ya Elimu mahitaji yaangaliwe kwa makini. Kamati inashauri kuwa licha ya mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kuongezeka kwa shule za msingi na za Sekondari; Mwongozo uelekeze, Mipango ihakikishe kuwa msititizo unawekwa katika kuboresha elimu si wingi tu wa watoto wanaokwenda shule (*quality versus quantity*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kuwa hatutaweza kuendelea bila ya kuwa na msukumo wa hali ya juu wa Uwekezaji katika Uchumi wetu (*Investment Drive).* Moja ya eneo linalotuathiri ni kushindwa kupunguza vikwazo vya utekelezaji na hivyo kufanya gharama zetu ziwe kubwa Afrika Mashariki *(cost of doing business).* Mwongozo uzingatie maeneo yanayohitaji maboresho na marekebisho ili tuongeze kasi ya kuvutia wawekezaji wa ndani na wa nje. Kwa kushindwa kuboresha mazingira ya kufanya biashara *(doing business)* taarifa aliyoitoa Mheshimiwa Waziri imetuonesha kwamba Uingereza imepunguza paundi milioni 10, Benki ya Dunia ilipunguza dola milioni 10 na Uholanzi ilisitisha msaada wa dola 40 milioni. Urasimu, kuchelewesha au kutokutoa maamuzi pamoja na baadhi ya sheria zetu inabidi zihuishwe. Aidha, Sera ya *PPP* ikamilishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado idadi kubwa ya Watanzania hawajafaidika na utaratibu wa uwezeshaji kupitia programu mbalimbali kuzingatia hali hii ili Mipango ijielekeze katika eneo hili. Aidha, kwa sababu tayari Tanzania tumeshajiunga na Soko la Pamoja la Afrika Mashariki, Mwongozo haujatoa maelekezo yoyote jinsi tutakavyojipanga, kwa madhumuni ya kukuza uchumi wetu katika soko hili kubwa. Serikali iangalie mkakati wa kujiingiza katika soko hili kwa nguvu zote kupitia Mipango yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya sasa ya nchi yetu inaonyesha dhahiri kwamba Serikali imeshindwa au haijatumia vizuri jiografia ya nchi yetu hasa kwenye uboreshaji na uimarishaji wa miundombinu ambayo ndiyo nguzo kuu ya kukuza uchumi wetu. Kamati inashauri mipango inayotolewa sasa ijielekeze kwa dhati na kwa makusudi moja kwa moja katika kuboresha bandari zetu za Tanga, Dar es Salaam na Mtwara, kuboresha Reli ya Kati, Reli ya Tanga, Arusha hadi Musoma pamoja na viwanja vya ndege. Uboreshaji wa miundombinu hii itasaidia kuibua uchumi wetu kwa kuhudumia ndani ya nchi na nchi za jirani za Burundi, Rwanda, DRC, Uganda, Zambia na kadhalika. Kamati inaamini kuwa Mwongozo huu utazingatia haya kupitia mikakati inayowekwa katika mipango inayokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeona kutokana na uzoefu tunaoendelea nao mpaka sasa ili tuwe na Mipango madhubuti ambayo inatekelezeka sambamba na bajeti itakayotolewa; Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuwa chombo madhubuti cha kupanga mipango, yaani Wizara ya Mipango. Kamati imeona kuwa zinapounganishwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa pamoja, masuala ya Mipango yanamezwa na kupoteza umuhimu wake na hivyo Mipango muhimu itokanayo na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Malengo ya Maendeleo ya Milenia 2015, MKUKUTA na mipango mingine inakuwa dhaifu hasa katika upande wa kufanyiwa tathmini, kufuatiliwa, kubuniwa na kutekelezwa kwa misingi endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kimsingi Wizara ya Fedha inashughulikia masuala ya Bajeti ya kila mwaka na si ajabu kuona msisitizo mkubwa ukiwekwa kwenye eneo la kuboresha Sera za kifedha zaidi badala ya kuangalia yale maeneo ya uzalishaji na yatakayoongeza mapato ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatoa pendekezo kwa Bunge kuanzisha Kamati ya Bajeti ili kufanya kazi zake kwa tija na ufanisi hasa Bunge litakapotekeleza wajibu wake kama Kamati ya Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho napenda kumalizia kwa kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya na ushirikiano wao walionipa. Naomba nitumie fursa hii kuwatambua wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dkt. Abdallah O. Kigoda, Mjumbe na Mwenyekiti, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mjumbe na Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Andrew Chenge, Mjumbe; Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga, Mjumbe; Mheshimiwa Anthony M. Diallo, Mjumbe; Mheshimiwa Fatma Abdulhab Fereji, Mjumbe; Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mjumbe; Mheshimiwa Athumani Said Janguo, Mjumbe; Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mjumbe; Mheshimiwa Eustace Osler Katagira, Mjumbe; Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mjumbe; Mheshimiwa Clemence Beatus Lyamba, Mjumbe; Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, Mjumbe; Mheshimiwa Monica Ngenzi Mbega, Mjumbe; Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mjumbe; Mheshimiwa Felix C. Mrema, Mjumbe; Mheshimiwa Mossy S. Mussa, Mjumbe; Mheshimiwa Damas Pachal Nakei, Mjumbe; Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge; Mheshimiwa Dkt. Omar Mzeru Nibuka, Mbunge; Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba, Mjumbe; Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq, Mjumbe; Mheshimiwa Mzee Ngwali Zuberi, Mjumbe; Mheshimiwa Devota Mkuwa Likokola, Mjumbe; Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mjumbe na Mheshimiwa Charles Kajege, Mjumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mbunge na Makamu Mwenyekiti, kwa kunisaidia kuiongoza Kamati, Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Mbunge na Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Jeremiah Solomon Sumari, Mbunge; Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, Manaibu Waziri wa Wizara ya Fedha na Uchumi. Aidha, naomba niwashukuru Watendaji Wakuu wa Wizara, Mashirika, Taasisi na Asasi zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Uchumi chini ya Katibu Mkuu wao Ndugu Kija kwa kuandaa Mwongozo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana wewe mwenyewe binafsi na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kutupatia miongozo na maelekezo mbalimbali kwa Kamati yetu ambayo wakati wote yamefanikisha kazi za Kamati. Aidha, napenda pia kumshukuru na kumpongeza Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashililah, Makatibu wa Kamati Ndugu Lawrence Makigi na Ndugu Michael Kadebe, kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI - WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 53(6), toleo la mwaka 2007, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kuwasilisha maoni ya Kambi kuhusu mpango wa Uchumi wa Taifa letu 2010/2013. Kama ulivyowasilishwa na Waziri wa Fedha na Uchumi leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kushukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuufika mwaka mpya tukiwa katika hali ya amani na utulivu nchini kwetu. Mola azidi kutupa amani, umoja na kuvumiliana hasa mwaka huu wa uchaguzi mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi za dhati kwako na kwa wasaidizi wako. Aidha, naomba kuwashukuru Wabunge wa Kambi ya Upinzani kwa ushirikiano wao walionipa wakati wa kutayarisha hotuba hii wakiongozwa na Dr.Willibrod Slaa, Mbunge wa Karatu na Naibu Kiongozi wa Upinzani Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe shukrani na pongezi za dhati kwa Waziri wa Fedha na Uchumi Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Mbunge wa Kilosa kwa ushirikiano wao walionipa pamoja na wasaidizi wake wote kama Waziri Kivuli wa Fedha na uchumi. Ahsanteni sana muendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani za pekee nawapa Bwana Oliver Mwikila, Frank Mbumi, Mama Mahundu na Grace Samwel kwa msaada mkubwa walionipa katika kufanikisha hotuba hii. Nawashukuru sana kwa moyo wao wa kujituma wakielewa uchache wetu na wingi wa majukumu tulionayo ya kuwatumikia Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango ya maendeleo ya nchi yetu kwa mujibu wa kanuni kifungu cha 94, naomba kuinukuu: “Ili kutekeleza majukumu yaliyoainishwa katika Katiba Ibara ya 63(3)(C) ya Katiba, Bunge litakaa kama Kamati ya Mipango katika mkutano wake wa mwezi wa Februari ili kujadili na kushauri kuhusu mapendekezo ya mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika mwaka wa fedha unaofuata” mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kuwa dhana hii haijaeleweka vizuri, hivyo ni matumaini yangu kuwa wananchi wataweza kutofautisha baina ya Bajeti na Bunge kuwa

Kamati ya Mipango ambapo kazi yetu kubwa ni kuishauri Serikali katika kuainisha vipaumbele vya Mipango ya Maendeleo na maeneo mengine ya kupata mapato zaidi kwa madhumuni ya Serikali kujitegemea kimapato. Ni wajibu wa Serikali kuuchukua ushauri huu na kuufanyia kazi ili kazi ya Wabunge iwe rahisi wakati wa kujadili na kupitisha bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** hivyo ni dhahiri katika maoni ya Kambi ya Upinzani, inawezekana ukajitokeza utofauti wa vipaumbele au mpangilio wake. Aidha tutaonesha maeneo mapya ya kuongeza wigo wa kukusanya kodi ili mapato yakidhi mahitaji yetu kwa lengo la kupunguza utegemezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tathmini ya mpango uliopita (unaoishia June 2010; mpango wetu wa maendeleo ulitokana na mpango wa muda mrefu (*Vision 20*-25) ambao Malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 ni kuhakikisha kuwa ifikapo 2025, Watanzania watakuwa na maisha bora na mazuri, kuwa na uongozi bora na utawala wa kisheria na kujenga uchumi imara wenye uwezo wa kukabiliana na ushindani. Tanzania itakuwa na uchumi unaotegemea sekta nyingi na ulioendelea kwa kuwa na wastani wa viwanda vingi, uchumi mpana ulio tulivu *(macroeconomic stability)*, miundombinu imara na pato la taifa linakua kwa asilimia nane au zaidi. Tanzania ya 2025 itakuwa inamudu ushindani wa Kikanda na Kimataifa kwa kuwa na nguvukazi yenye elimu na ujuzi. (Mpango huu haueleweki vizuri kwa umma kama vile lilivyoweza kueleweka Azimio la Arusha).

Mheshimiwa Mwenyekiti, MKUKUTA ambao ni sehemu ya Dira ya Taifa, lengo lake kuu liko katika *cluster* tatu ambazo ni:-

(a) Kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato.

(b) Kuimarisha ubora wa maisha na ustawi wa jamii.

(c) Kuimarisha Utawala bora na uwajibikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukadiriaji wa gharama za MKUKUTA katika baadhi ya sekta muhimu ulikamilika mwishoni wa mwaka 2006 na gharama zake zikabainika kuwa ni kubwa mno kuliko uwezo wa Serikali. kwa hiyo MKUKUTA umeshindwa kutekelezeka kikamilifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya 2009/10 ni ya mwisho ya utekelezaji wa MKUKUTA. Waziri kaeleza kwamba Serikali inaandaa MKUKUTA namba II. MKUKUTA wa kwanza haujafanyiwa tathmini ya kina ili kujifunza kutoka mapungufu yaliyojitokeza. Ni wazi MKUKUTA wa pili hautakamilika na kuanza kutekelezwa mwaka wa bajeti wa 2010/11. Ikiwa Serikali ina lengo thabiti la kuwa na mpango wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini unaotekelezeka inastahili kujipa muda kutathmini MKUKUTA na kushirikisha wadau wote katika kuandaa mpango mbadala wa kukuza uchumi kuongeza ajira za uhakika na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina nia ya kuelezea mafanikio na mapungufu katika maeneo hayo kwani mnaelewa namna Serikali yetu inavyofanya maamuzi yake, kwa mfano imechukua miaka nane kuanzisha utaratibu wa kuishirikisha sekta binafsi katika miradi mikubwa PPP, imetuchukua miaka 47 kufikia hekta laki 3.5 kati ya hekta 2.9 milioni ambazo ni nzuri kwa umwagiliaji ili tujitosheleze kwa chakula. Hadi leo tumeshindwa kuwa na umeme wa uhakika kwa matumizi yetu, pamoja na kuwa na vianzio visivyopungua saba vya uhakika ambavyo vingetuwezesha kuuza umeme nje ya nchi na kujipatia fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kugusia maeneo machache tu na hasa lile nililowahi kuliuliza katika Bunge lako Tukufu na nikajibiwa la ughali wa uchumi wetu au kwa lugha rahisi gharama za kufanya biashara Tanzania ambazo huchangia ughali wa uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tarehe 16 Februari 2006, niliuliza swali hili hapa Bungeni: Kwa kuwa Serikali katika vipindi vya bajeti ya 2003/2004 na 2004/2005 iliahidi kulifanyia kazi tatizo la ughali wa uchumi wetu:-

(a) Je, nini matokeo ya utafiti huo?

(b) Je, ni hatua gani zilizochukuliwa kupunguza ughali huo wa uchumi?

Serikali ilijibu kama ifuatavyo, naomba kunukuu: “Serikali haioni umuhimu wa kufanya utafiti huo kwa vile hali halisi ya ughali huo ilishaonyesha dhahiri kutokana na malalamiko ya wananchi wa kawaida na wawekezaji.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa, ili kufikia malengo ya nchi yetu kushinda maadui kama ambayo ilianishwa katika misingi mikuu ya Azimio la Arusha yaani, Maradhi, Ujinga na Umasikini utafiti wa kujua hali halisi ya mazingira yanayotuzunguka kama vile rasilimali za aina zote, wingi wake na mgawanyo wake ni muhimu. Hapo ndipo tutakapoweza kupanga uchumi wetu vizuri na kufanikiwa kushinda wale maadui wakuu kama ilivyobainishwa katika azimio la Arusha ambalo pamoja na kwamba limekufa lakini maudhui yake yanatumika hasa katika MKUKUTA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa mtazamo huo vituo vingi vya utafiti vilikufa na vilivyopo havipewi fedha za kutosha, matokeo yake Taifa ambalo uchumi wake kwa kiwango kikubwa unategemea Kilimo hata mbegu (bora) za kutosha halina. Tofauti ya wenye kipato na wasionacho kila uchao inaongezeka, kinyume na matarajio ya AZIMIO la Arusha au MKUKUTA. Mipango yetu kwa bahati mbaya sio endelevu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano malengo ya kukusanya mapato ya ndani kwa mwaka 2008/2009 yalikuwa ni 18.5% ya pato la Taifa, mwaka 2009/2010 yalikuwa ni 16.4% ya pato la Taifa, mwaka 2010/2011 ni 15.5% ya pato la Taifa, shabaha ni kufikia 16.1% kwa mwaka 2012/2013. Je lile lengo la awali limesahauliwa au limeonekana halitekelezeki? Ni kitendawili labda Waziri atatusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika mapendekezo ya Mpango uliowasilishwa, Serikali Kuu, Mikoa na Halmashauri zinatakiwa katika kipindi cha miaka mitatu kiweke kipaumbele katika mambo 10, lakini nitataja moja tu nalo ni (ii) kuhakikisha kuwa rasilimali (fedha) zinaelekezwa kwenye utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi (2005) MDGS, MKUKUTA II, KILIMO KWANZA na vile vile mambo ya mtambuka kama vile *HIV* Na *AIDS*, maboresho, jinsia na mazingira. Kambi ya Upinzani inataka kujua hivi Kilimo Kwanza ni Mpango tafauti na ule wa MKUKUTA, MKURABITA (ambao sasa hautajwi) na *MDGS*? Hii si kujirudia rudia kwa *programs over lapping*? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaashiria kuwa kuna mapungufu makubwa katika mipango yetu, kwani nchi yetu ina kila kitu kinachotakiwa kwa maendeleo ya wananchi wake. Japokuwa kuna sababu wanazozitoa za hali ya hewa na mtikisiko wa uchumi wa dunia lakini bado Kambi ya Upinzani, inaona udhaifu wa mipango yetu upo pale pale na ndio maana bado tunaendelea kushauri kuwa ni vyema Kamisheni ya Mipango ikawekwa ndani ya Katiba ili isiwe inaundwa na kuvunjwa kila wakati. Tuwe na Kamisheni ya Mipango ya Kudumu ili iweze kuratibu vyema mipango yetu na ifanye kazi zake kwa utaalam bila kuingiliwa na Siasa kama ilivyotokea hapo nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndio tathmini fupi ya mipango yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtazamo na mpango wa uchumi wa Kambi ya Upinzani utajikita katika sekta zifuatazo ili kutengeneza mazingira yatakayotoa fursa sawa kwa Watanzania katika kunufaika na uchumi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo, ni ukweli ulio wazi kuwa tatizo kubwa linalosababisha hali ya maisha ya Mtanzania wa kawaida kuwa mbaya ni mfumuko wa bei. Mfumuko wa bei unasababishwa na upandaji wa bei za vyakula na hivyo kusababisha kudhoofika kwa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa ili kujikwamua haraka na hali hii mbaya ya uchumi, hatuna budi kuwekeza kwenye sekta ambayo itabadilisha hali hiyo kwa haraka nayo ni kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ni eneo pana na kwa madhumuni ya angalau kuondokana kabisa na suala la njaa, Kambi ya Upinzani inashauri kati ya hekta 2.3 milioni ambazo ni *High Potential* kwenye kilimo cha umwagiliaji ambazo zimegawanyika katika maeneo ya mabonde mbalimbali ya nchi yetu angalau tujipangie katika miaka hii mitatu tuzalishe mpunga na mahindi kwa wastani wa tani milioni tano mbali na uzalishaji unaoendelea. Mahitaji ya mchele kwa Tanzania ni tani karibu 600,000 tu kwa mwaka. Lakini kila mwaka nchi inakuwa na uhaba wa mchele wa karibu tani 150,000. Hivyo basi kati ya hekta 2.3 milioni tutachukua hekta 500,000 tu. Uzalishaji kwa hekta ni tani tano wakati gharama za uzalishaji kwa hekta ni Tshs.10 milioni. Kwa mpango huo tutakuwa tumezalisha mchele tani 2.5 milioni kwa gharama za Tshs.5 bilioni ambazo mwaka unaofuata zitapungua. Aidha, zoezi kama hili litahusu pia kwa zao la mahindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri huu wa Kambi ya Upinzani utaisaidia Serikali kujitosheleza kwa chakula na pia tutapata ziada ya kuuza nchi za jirani (soko la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki). Kwa mujibu wa takwimu zinazotolewa na taasisi ya biashara ya mazao ya kilimo katika eneo hili la Afrika (*Regional Agricultural Trade Intelligence Network-RATIN*) bei ya tani moja ya mchele Kampala ni USD 892 sawa na Tshs. 1,159,600/= na kwa mahindi ni USD 174 sawa na Tshs. 226,200/=. Kama tukiuza tani milioni moja za mchele tutapata Jumla ya Tshs. 1,159,600,000,000/=. Tukumbuke kwamba bei katika soko la Afrika Mashariki zinatofautiana kulingana na miji husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetoa takwimu hizo katika kuonyesha umakini katika mipango, kama kweli Serikali ingekuwa makini fedha zote za *ASDP* pamoja na za Mfuko wa JK zingetosha kubadilisha na au kumaliza tatizo la aibu la kuwa nchi yetu inakumbwa na balaa la njaa kila muda fulani. Tatizo la msingi hapa ni kukosekana kwa utashi wa kisiasa, kutafuta umaarufu kwa mipango isiyoandaliwa kwa umakini na au kudharau ushauri wa kitaalam na kufanya maamuzi yanayogusa maisha ya binadamu kwa msingi wa kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upotevu wa Mazao Kabla na Baada ya Mavuno (*Post and Storage Harvest Loss);* Upotevu wa mavuno kwa mazao ya chakula na yale ya biashara ni tatizo ambalo limekuwa ni sugu kwa nchi zinazoendelea na kwetu limekuwa na linaendelea kuwa tatizo kubwa sana. Upotevu huu unaweza kuwa ni kupungua kwa ubora halisi na kiwango kwa mazao (*quality and quantity*) au uharibifu mwingine kama kuoza kwa mazao kuliwa na wanyama pamoja na wadudu waharibifu wa mazao na kadhalika, uhifadhi duni na ukosefu wa masoko pindi mazao yanapovunwa toka mashambani ndio chanzo kikubwa cha upotevu wa mavuno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa tafiti zilizofanywa na Shirika la Chakula na Kilimo (*FAO*) kwa nchi 15 zinazoendelea upotevu ni kati ya 15% na 100% kwa kutegemeana na aina ya zao. Tanzania na Brazil kama nchi zingine ni kwamba kwa zao la mahindi upotevu wa uzito baada ya kuhifadhiwa ni kati ya 20%-45% kwa Tanzania na Brazil ni kati ya 15%-40%. Lakini kwa mujibu wa takwimu za Serikali ya Tanzania upotevu ni kati ya 30%-40% ya mavuno yote ya mazao. Kwa nchi ya India upotevu wa mazao kabla ya mavuno Kamati maalum ya Serikali ilikisia kuwa kwa ujumla upotevu ni 9.33% ya uzalishaji mzima wa nafaka nchini humo. Kati ya asilimia hizo, 70% inatokana na uhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana nzima ya kutoa takwimu hizo ni kuuliza kuwa kama nchi ya India ambayo ni mfano wetu kwa uzalishaji na teknolojia iliyonayo lakini bado kuna upotevu kiasi hicho. Je, hapa kwetu Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha wakulima hawapati hasara hiyo ya *post and storage losses*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa kama Serikali haijaweka mkakati mahsusi wa kupambana na upotevu wa mazao (nafaka na matunda) basi dhana nzima ya KILIMO KWANZA haitakuwa na maana kwa wakulima

wenyewe na kwa Serikali, hivyo ni wajibu wa Serikali katika mipango yake kuweka mkazo kuhakikisha kuwa upotevu hasa utokeao katika kadhia nzima ya uhifadhi wa mazao unapatiwa ufumbuzi wa kudumu jambo ambalo litazidi kuwatia moyo wakulima kuendelea kuzalisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashauri Serikali iagize mashine za kukaushia mazao *(HYGREX MACHINE)* ili kupunguza upotevu wa mazao na itasaidia kupatikana kwa masoko ya kuuza mazao yaliokaushwa, teknolojia hii inapatikana Canada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Viwanda vya Uzalishaji katika Kilimo; Sera ya Kilimo ya mwaka 1997, *ASDP* ambacho ni chombo au programu ya kutekeleza malengo ya mkatakati wa kuendeleza sekta ya kilimo (*ASDS*) pamoja na kauli mbiu zingine zinazotolewa katika sekta ya KILIMO kama vile KILIMO KWANZA. Dhana kuu ni kukiwezesha kilimo kiwe cha kisasa, cha kibiashara, kilicho na tija, kinacholeta faida, kinachozingatia matumizi endelevu ya rasilimali na kinachochochea maendeleo ya sekta nyingine. Hivyo basi, ili kufikia malengo hayo hayo nishati ya umeme ndio kichocheo kikubwa ili kilimo chetu kiwe ndio daraja la kutuvusha na kufikisha pale tulipokusudia kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli ulio wazi kuwa ili kilimo kiwe cha kisasa, kilicho endelevu na chenye tija, tunahitaji kuwa na viwanda vyetu vya uzalishaji wa pembejeo hasa mbolea na miundombinu ya uhakika ya umwagiliaji mashamba yetu. Kwa kuwa Tanzania kwa kiasi kikubwa inategemea kilimo hasa cha wakulima wadogo ambao wanaishi vijijini na kwa takwimu zilizopo inaonesha kuwa, Watanzania wanaopata umeme wa Grid ya Taifa ni chini ya 10% huko vijijini. Kambi ya Upinzani inarudia tena kuwa Nishati Umeme ndiyo kichocheo hasa kitakacholifanya Taifa letu kuwa Taifa lenye fursa sawa na hivyo kuwafanya Watanzania na nchi yao kuondokana na umaskini uliokithiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo kwa maoni yetu linahitaji kupewa kipaumbele ni la Nishati ya Umeme. Kwani ni aibu kwa nchi yetu, yenye vyanzo vya kutosha vya kuzalisha umeme, lakini hadi leo tuna programu za zimamoto za kukabiliana na tatizo hili na hatimaye kujitokeza vitendo vya kifisadi ndani yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu kubwa za upungufu wa uzalishaji umeme zinazotajwa siku zote ni ukame (kuchelewa kunyesha mvua), jambo ambalo linajulikana mara zote na mapema kutokana na utabiri wa hali ya hewa na pia vituo vinavyofuatilia mwenendo wa maji vya *Hydrological Instruments* vya *TANESCO*. Sababu hiyo hiyo ya ukame ndio hutumika na Serikali pale inapotokea njaa katika nchi kwamba, ukame ndio uliosababisha njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo nchi nyingi duniani ambazo hazizalishi umeme kwa kutokuwa na vyanzo vya maji wala hazitumii kilimo kwa chakula na nchi hizo na baadhi ya hizo nchi, hazina hata ardhi ya kulima, lakini hawatoi sababu za kukosa umeme kwa ajili ya mvua wala chakula, kwa sababu ya ukame. Hii ni kwa sababu ya mipango

kabambe ya nchi hizo tena inayotekelezwa kwa vitendo bila ya kubakia katika makabrasha ya mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kauli ya Serikali iliyotolewa hapa Bungeni tarehe 4 Novemba, 2009, Serikali imeahidi kusimamia na kutekeleza miradi ifuatayo:-

(1) Kuwa na kituo cha MW 100 kitakachojengwa Ubungo na kutumia gesi asilia na kuanza uzalishaji mwaka 2011.

(2) Kuwa na kituo cha MW 60 cha mafuta mazito (HFO) katika Jiji la Mwanza na kukamilika mwaka 2011.

(3) Kituo cha MW 50 kwa nishati ya upepo Mkoa wa Singida, ambacho kitatumia upepo, kitajengwa na wawekezaji binafsi na kuanza uzalishaji mwaka 2011.

(4) Kituo cha MW 240 cha kutumia nishati ya gesi cha Kinyerezi kwa mfumo wa PPP kitakachojengwa na kuanza kuzalisha ifikapo mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na mipango hiyo ya Serikali tuliyoelezwa hapa Bungeni, pia imetolewa taarifa kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi kuhusu hali ya umeme na ukuaji wa uchumi tarehe 20 Januari 2010 na hapa napenda ninukuu ukurasa wa 9 na 10 wa taarifa hiyo ya Serikali:-

"Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba, dhima ya nchi ni kuwa kitovu cha kutoa umeme Afrika Mashariki, kwa maana hiyo itakuwa muhimu kuendeleza mapema zaidi miradi miwili; yaani Mchuchuma (MW 400) na ule wa *Stieglers' Gorge* (MW 1200) ili umeme utakaotokana na miradi hii uweze kupatikana mapema zaidi kuanzia mwaka 2015. Ili kuruhusu kuanza kwa ujenzi wa miradi hii mapema ni vyema kufanyika kwa tafiti na pembuzi yakinifu, pamoja na tathmini ya athari za mazingira zitakazoendana na miradi hii itatekelezwa. Tafiti hizi yafaa zifanyike mapema kuanzia sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya ili niikumbushe Serikali na Bunge lako Tukufu kwamba, mipango iliyopo ni mingi sana, lakini haina uwiano (*consistency*), haina vipaumbele (*priority*), wala haijaandaliwa katika misingi ya gharama halisi *(realistic cost conscious)* na hivyo kufanya sehemu kubwa ya miradi kutokutekelezeka. Kwa kubaini hilo, napenda tujikumbushe mipango mingine iliyopangwa na Serikali kupitia *TANESCO* katika Mpango wa Ufufuaji, pamoja na *Power System Master Plan (PSMP)* na Wazalishaji Binafsi *(IPP).* Mipango hiyo ni *Financial Recovery Plan and Power System Master Plan 2009 - 2031* iliyowasilishwa kwa Kamati ya Nishati na Madini, baadaye Semina ya Bunge Zima, pamoja na Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Umeme 2009 – 2033 *(2009 PSMP UPDATE).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa FRP wa TANESCO umetengenezwa kwa dhana ifuatayo: Usambazaji umeme vijijini kuunganisha wateja wapatao laki moja kwa

mwaka; makampuni ya madini kukubali kutumia umeme wa gridi; Serikali itatoa fedha kugharimia mitambo ya kuzalisha MW 60 Mwanza na kuanza kufanya kazi 2009; Serikali itatoa fedha kujenga mtambo mwingine wa MW 100 Ubungo na kuweza kufanya kazi mwaka 2011 *(PSMP – Kiwira 2010);* Mnazi Bay iwe tayari kuzalisha MW 300 mwaka 2013 *(PSMP – Mnazibay 2021)*; *ZTK Interconnector* iwe tayari mwaka 2014; na Mradi wa Kuzalisha Gesi wa Songosongo uweze kuzalisha 1000 bcf na ipatikane PSM *(billion cubic feet).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa tufanye uchambuzi wa hayo yote niliyoyataja hapo juu, yanayotokana na Taarifa kwa Kamati ya Fedha na Uchumi, Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini, pamoja na ile Semina ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Bunge zima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa tufanye uchambuzi wa hayo:-

Kwanza, *Financial Recovery Plan And Power System,* inazungumzia kuzalisha umeme wa Kinyerezi I kwa kutumia HFO kwa MW 150 mwaka 2010 na Kinyerezi II kutumia gesi kwa MW 100 mwaka 2013, ambapo *Power System Master Plan* imepangwa Kinyerezi I kutumia gesi na kuzalisha MW 100 na kuwa tayari mwishoni mwa 2009 na Kinyerezi II kutumia gesi na kuwa tayari Januari 2010. Mpango upi ndio wa uhakika hapa? Je, hiyo gesi ya Songosongo ya 1000 bcf itakuwa tayari mwaka gani?

Je, bomba la gesi lililopo hivi sasa ambalo halina tena uwezo wa kutoa gesi ya kutosha hata kwa huo mtambo wa MW 100 katika mwaka wa 2010 itatoka wapi ikiwa Serikali haikujenga bomba lingine hivi sasa? *(Makofi*)

Kamati ya Fedha na Uchumi haijaelezwa mpango wa ujenzi wa bomba jipya la gesi kutoka Songosongo, pamoja na mtambo mpya wa kusafisha gesi ambao ni lazima kwa vile uliopo hivi sasa hauna uwezo tena.

Kukosekana kwa mipango au fedha za kutekeleza ujenzi wa mtambo mpya wa kusafisha gesi na bomba jipya kutoka Songosongo na Dar es Salaam, hakuna uwezekano wa kutekeleza miradi hii. Hivyo, inaonekana wazi kuwa, bado Serikali haina uwiano katika mipango yake. Taarifa tunazopewa kwenye Kamati mbili ni tofauti na utekelezaji wake ni tofauti.

(a) Inaonekana FRP kwa umeme wa Kiwira ni mwaka 2011, PSMP ni mwaka 2010, Kauli ya Serikali 2013; tushike lipi? Mipango ya kifedha iko wapi? Tunaomba Serikali ilieleze Bunge lako kauli moja ambayo haina utata. Si vema Taifa likajazwa matumaini ambayo hayakujengwa katika msingi imara wa mipango madhubuti.

(b) Katika mipango ya usafirishaji umeme katika PSMP Mtwara – Dar es Salaam au Mtwara na kwingineko haijatajwa na haimo katika mpango. Gesi ya uhakika ya Mnazi Bay inafahamika, tena nyingi mno, wakati huo huo kauli ya Serikali inazungumzia Kituo cha MW 300 Mnazi Bay mwaka 2013; sasa huo umeme utasafirishwa wakati mabomba hakuna? *(Makofi)*

Hapa mipango ya Serikali inakatisha tamaa na kuonekana porojo tupu. Tunaomba kauli sahihi ya Serikali pamoja na *Mtwara Corridor Program* imefikia wapi? *(Makofi)*

(c) Je, Serikali iliiwezesha vipi na kwa kiasi gani FRP ya *TANESCO* na ina mipango gani ya kuiwezesha PSMP ili itekelezeke?

(d) Wakati Serikali inazungumzia mipango ya kuwa na umeme kwa kutumia nishati ya upepo huko Singida wa MW 50 hapo mwaka 2011, *Power Pool East Africa Ltd (IPP),* Singida mipango yao ni kuzalisha MW 15 za kuingiza katika gridi kwa majaribio ifikapo Agosti, 2010 na mipango ya kuzalisha MW 210 mwaka 2013. Hii ni dhahiri kwamba, Serikali inakosa *Coordination* baina yao na hawa IPP na kukosekana usahihi wa mipango yake. Je, Serikali itatatua vipi mipango ya namna hii na kuamini wanachosema?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine, hebu tuangalie gharama inazoingia Serikali katika *IPTL*. Kamati ya Fedha na Uchumi ilielezwa kwamba, gharama za *IPTL* kwa mwaka ni dola milioni 180 wakati Kamati ya Nishati na Madini ilielezwa kwamba ni dola 190. Yote ni kuonesha kwamba, takwimu zetu zinazowasilishwa kwenye Kamati zetu za Bunge zinatofautiana kila wakati na kwa hiyo mipango yetu ina matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa, kipindi hiki cha mpango tumalize tatizo la umiliki wa IPTL, tuwekeze nguvu zetu katika miradi itakayotupa umeme usiopungua MW 1000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya uchambuzi tulioufanya, naomba tulithibitishie Bunge lako Tukufu kwamba, pasipo na takwimu sahihi hapatakuwa na mipango sahihi ya kiuchumi. Hili linathibitika pale Kamati zako za Kudumu za Bunge ambazo ni ya Fedha na Uchumi na ile ya Nishati na Madini, zinapopewa taarifa ya jambo moja lenye takwimu tofauti. Mfano:

Katika mikakati ya dharura, maamuzi yaliyofanywa na Serikali kuruhusu kutumia mitambo ya IPTL ni kama ifuatavyo:-

Mafuta (HFO) tani 14125		U$D 10,425,024
Vipuri na vilainishi mitambo	U$D	743,174
Gharama za *fixed cost (capacity charge)*	U$D	1,600,000
Jumla ndogo		12,768,198
VAT 18%		2,298,275
Jumla Kuu		15,066,474
Exchange rate 1330 = TShs.		20,038,410,493

Kwa mwaka gharama hizi ni $180,796,690, (U$D)

Kwa upande wa Kamati ya Nishati na Madini, gharama za mafuta kwa mwezi ni tani 15000, ambazo Serikali inalipa TShs.600,000,000 kwa siku, sawa na TShs.18,000,000,000 kwa mwezi = USD 13,533,835.

Mafuta (HFO) tani 15000	-	U$D 13,533,835
Vipuri na vilainishi	-	U$D 743,174
Gharama za *capacity charge*	-	U$D 1,600,000
Jumla Ndogo		U$D 15,877,009
Vat 18%		2,857,861.60
Jumla Kuu		18,734,871,60

Exchange rate 1330 TSh. 24,917,379,000

Kwa mwaka ni USD 190,524,110

Mheshimiwa Mwenyekiti, nukuu na maelezo yote haya niliyoyatoa, hayana nia ya kuisema vibaya Serikali ila najaribu kuonesha udhaifu na kasoro nyingi zilizopo katika mipango yetu katika Sekta ya Nishati hasa umeme ili tuwe na mipango sahihi ya kukabiliana na tatizo hili na hatimaye tuwe na umeme wa uhakika na wa kuweza kuuza nje ya nchi yetu. Kambi ya Upinzani inashauri kwa kipindi hiki cha Mpango, tumalize tatizo la umiliki wa IPTL, tuwekeze nguvu zetu katika miradi itakayotupa umeme usiopungua 1000 MW.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kukua kwa teknolojia ulimwenguni, Kambi ya Upinzani, inashauri Serikali itumie teknolojia ya *mapping* ili kujua kwa kina, rasilimali zote zilizoko nchini na namna tunavyoweza kuzitumia. Teknolojia hii inapatikana hata *Spain*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa Serikali imeshindwa kujua wingi wa madini tulionao nchini, lakini baya zaidi hata kuzigawa kwa kufuata umuhimu wake imeshindikana. Hakuna nchi duniani *Uranium* inaweza kutolewa kiholela au mkaa wa mawe, shaba, chuma, nikel na kadhalika *(Industrial Minerals)* isipokua Tanzania. Sababu kubwa; hatujui thamani, wingi na mahali zilipo na kwa kiasi gani zitasaidia uchumi wetu. Huku ni kukosa mipango mizuri na endelevu na kutokutumia vema rasilimali watu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inashauri utafutwe utaalamu haraka sana, kabla hatujaingia katika Shirikisho la Kisiasa la Jumuiya ya Afrika Mashariki ili Watanzania wajue rasilimali zao kikamilifu ili kuepuka migongano ya kijamii baadaye. Aidha, kwa Taasisi ya Uwekezaji *(Tanzania Investment Centre)*, watakuwa wanatoa vibali kwa wawekezaji kulingana na rasilimali zilizopo, wakijua mazingira halisi ya uwekezaji; hii itasaidia Serikali kukusanya kodi kulingana na uzalishaji na rasiliamali zilizopo, badala ya kutoa vibali kwa Wawekezaji bila kuzingatia maliasili zilizopo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi ni mojawapo ya rasilimali na nyenzo muhimu katika kukuza uchumi na kupambana na umasikini, kwani ndiyo inayotoa ajira kwa wastani wa asilimia 75 ya Watanzania. Watanzania bado hawajanufaika na rasilimali hii ambayo ina ukubwa wa kilomita za mraba 885,200, kwani kutokana na taarifa ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; ni viwanja 18,641 na mashamba 734 katika mikoa 21 ambavyo vimepimwa na wahusika kupewa Hati. Viwanja 56,743 vilipimwa Dar es Salaam, Mradi wa Kupima Viwanja 20,000 kuanzia mwaka 2002/2003 hadi Juni 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukizingatia umuhimu wa rasilimali hii katika siyo tu kumwendeleza Mtanzania kiuchumi, bali kumpa urithi wa asili, ni kwa vipi kwa mwenendo huu wa kutoa viwanja kidogo kama hivi; Watanzania wasiopungua milioni 25 wataweza kurithishwa rasilimali hii ambayo ndio utajiri wao wa asili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, utambuzi wa ardhi ni mojawapo ya chanzo kikuu cha mapato kwa Serikali kupitia kodi ya ardhi na kodi hii haiwezi kulipwa kwa wamiliki wa ardhi wasiokuwa na hati. Mfano, Wizara ya Ardhi ilikusanya kodi ya ardhi ya shilingi 586,998,900 kwa Mkoa wa Dar es Salaam, baada ya kusajili nyumba 217,407 tu. Zoezi hili la kusajili na kutoa hati kwa ardhi za nyumba likiendeleza, Serikali itakuwa imepata mapato ya kutosha.

Kambi ya Upinzani ilitegemea kwa umuhimu wa pekee na kwa kuzingatia ushirikiano wa Afrika Mashariki, mipango ingelikuwa wazi zaidi katika kumilikisha viwanja na mashamba kwa Watanzania, pia ichukuliwe kuwa inaongeza mapato ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo la kuwa na takwimu sahihi za rasilimali watu wanaotoa huduma katika Sekta za Umma hapa kwetu. Kwa mfano, Sekta ya Afya na Elimu zina upungufu mkubwa wa watumishi na ukiangalia mipango yetu hasa katika nyanja ya sayansi, mahitaji ni makubwa kuliko uzalishaji wa wataalamu wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa, iwekwe mipango madhubuti ya kujua idadi ya wataalamu wetu katika kila fani, upungufu na mipango ya kujaza upungufu huo kwa kutumia watu au teknolojia ya mawasiliano hasa katika elimu na huduma za afya*(Distance Learning and Tele Medicine).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango mizuri ya rasilimali huleta maendeleo ya nchi na huchangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la Pato la Taifa. Nchi nyingi duniani, Pato lao la Taifa limeongezeka kutokana na Raia wao wanaofanya kazi nje ya nchi kutuma fedha kwa ndugu zao nyumbani na hizo pesa zinachangia katika Pato la Taifa; mfano, nchi kama Phillipines, Israel, India na nchi nyingine nyingi zimepata mapato makubwa. Aidha, katika mwaka 2007, jumla ya Dola za Kimarekani 337 bilioni zilitumwa na wafanyakazi mbalimbali duniani. Katika nchi zetu za Afrika ilikuwa Dola za Kimarekani 251 bilioni, zilitumwa kwenye nchi zinazoendelea kutokana na wananchi wao kufanya kazi nje ya nchi na zinachangia kwenye Pato la Taifa *(GDP)* kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa yake, Shirika la *International Organization for Immigration (IOI),* lilieleza kuwa, kwa miaka 20 iliyopita, fedha zilizotumwa na wafanyakazi wa nje kwenda nchini kwao, zilizidi fedha za misaada, pamoja na fedha za uwekezaji wa moja kwa moja *(Direct Foreign Investment).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Taarifa ya Shirika la Maendeleo ya Binadamu *(Human Development Report 2009),* Watanzania wote, wanaofanya kazi nje ya nchi, wanachangia katika Pato la Taifa dola milioni 14 katika suala zima la maendeleo. Wakati nchi kama Nigeria ni bilioni tisa, Somalia dola bilioni mbili, pamoja na kuwa wako katika vita, Kenya dola milioni mia saba na Uganda dola milioni mia sita.

Ukilinganisha Tanzania na nchi nyingine, utaona kwamba, kuna tatizo la kutojua taarifa sahihi za idadi ya Watanzania wanaoishi nje ya nchi na kipato wanachotuma kwa ndugu na jamaa zao; jambo hili linaikosesha nchi kujua fedha halisi kutoka nje ili kuzielekeza katika mipango ya maendeleo. Serikali inatakiwa kuweka utaratibu mzuri wa kujua Watanzania wanaoishi nje ya nchi na fedha wanazotuma makwao ili kuziingiza katika Pato la Taifa *(GDP).* Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali ifanye utaratibu wa kuweza kuwaratibu watu hawa na kuingiza katika bajeti yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali ianzishe haraka utaratibu wa kuwajua na kuwaratibu Watanzania walioko nje na ambao wana mapenzi na nchi yao, aidha, uanzishwe utaratibu wa *Diaspora Bonds;* India na Israel wameweza kukusanya wastani wa USD 35 - 45 billion kwa kutumia *diaspora bond (World Bank Development Finance via Diaspora Bonds).* Hapa ndio umuhimu wa uraia wa nchi mbili unapoonekana, jambo ambalo Serikali yetu imekuwa ikilipuuzia kwa muda mrefu sasa.

Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali iharakakishe mchakato na utaratibu wa *Dual Citizenship* ili Taifa letu lisiendelee kupoteza faida na manufaa ya kuwa na uraia wa nchi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri huu ukitekelezwa, Serikali itakuwa imepanua wigo wa mapato na kupunguza matumizi yetu ya fedha za kigeni kwa kutegemea mapato yatokanayo na mauzo ya nje; hivyo, urari wetu wa biashara kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakisi ni eneo jipya kabisa kwa Serikali. Tumekuwa tukitoa visingizio vingi juu ya kutokufikia malengo ya kukusanya mapato, japokuwa tunaambiwa tumepanua wigo wa kukusanya kodi. Ukiangalia takwimu zilizotolewa katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri, inonesha kuwa katika kipindi cha miezi sita tu, Serikali imetoa misamaha ya kodi inayofikia Tshs. 324.14 bilioni. Tungeomba sana, ili kuondokana na bajeti tegemezi, angalau asilimia 50 ya misamaha hii iondolewe ili nakisi katika bajeti iweze kuondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misamaha hii ya kodi ndicho chanzo kikuu cha kuleta nakisi (*deficit*) katika bajeti yetu. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inatarajia misamaha

hiyo ambayo kwa takwimu za Serikali ni asilimia 30 ya makusanyo yote ya kodi au 3.5 ya pato la nchi, ipungue angalau iwe sawa na wenzetu wa Kenya au Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linawezekana kama kweli tutakuwa makini katika kusimamia mipango yetu; jambo ambalo limekuwa ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, manunuzi ya jumla *(Bulk Procurement),* tumelisema sana ndani ya Bunge lako Tukufu; tunaomba Serikali iangalie namna gani tunaweza kupunguza manunuzi kwa kuwa na *bulk procurement.* Manunuzi ya Halmashauri na Serikali ni asilimia kama 70, tunaiomba Serikali iangalie ili kupunguza ukwasi katika bajeti yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato yanayotokana na madini hasa dhahabu na almasi bado hayaridhishi. Tunaelewa kuwa, Serikali inaleta Sheria Bungeni, lakini maeneo mawili yanahitaji mipango ya muda mrefu. Kwanza, upatikanaji wa mitaji ya uchimbaji madini. Makampuni mengi hayakopi hapa nchini na kwa maana hiyo, fedha nyingi wanakopa nje na hatuwezi kujua ni kiasi gani cha fedha ambacho wamekopa na kila siku wanaendelea kusema kwamba wanadaiwa. Ni vema mabenki yetu sasa yaweke utaratibu wa kuwakopesha watu wetu.

Pili, mapato makubwa hupatikana kutokana na huduma zinazopelekwa kwenye makampuni hayo; kwa mfano, mitambo wanayonunua, bidhaa wanazonunua, lakini mpaka sasa hivi Serikali haijaandaa utaratibu mzuri wa bidhaa na *supplies* kwenda kwenye migodi. Kwa hiyo, uhaulishaji wa fedha unakuwa mkubwa. Tunaiomba Serikali iandae utaratibu wa kuangalia viwanda gani vinaweza kuhudumia makampuni haya ya madini na hasa huduma gani zinazohitajika ili tupunguze tatizo la kuhaulisha fedha kwa kisingizio kwamba, wananunua huduma nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda ni bidhaa muhimu, pindi ikishapita basi haipatikani tena. Tanzania katika mipango yake ya maendeleo, suala la muda limekuwa halitiliwi maanani au halipewi kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, baada ya kufanya tafiti, imegundua kuwa, muda unaopotezwa na watumishi wa umma au wajasiriamali kwa kujua au kutokujua ni mwingi mno. Maeneo yafuatayo ndiyo yamekuwa yakikwaza katika shughuli za maendeleo; kwanza ni kwenye mabenki yetu, ambapo utakuta msululu mkubwa wa wananchi wanangojea huduma, hospitali na sehemu nyingine nyingi. Tumefanya utafiti tumeona saa nne kwa siku, watu wanapoteza bila ya kufanya kazi. Kutokana na hali hiyo, tungeomba Serikali iweke utaratibu wa kwamba, anayeingia kazini, muda anaoingia na muda anaotoka ujulikane. Vile vile mfanyakazi huyo lazima alipwe vizuri ili aweze kujihudumia kutokana na mshahara anaopata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kubuni sera nzuri ni mwanzo tu; Sera zinazopaswa kuwekwa katika mipango ya utekelezaji na kutekelezwa kwa umakini wa hali ya juu ni jambo lingine. Utekelezaji na matokeo yake ufanyiwe tathmini ya mara kwa mara ili makosa yagunduliwe na kurekebishwa. Kujenga utumishi bora, wenye

ujuzi, usioyumbishwa na rushwa ndani ya Serikali ni changamoto muhimu. Utumishi mzuri ulio imara haujengwi siku moja. Viongozi wa kisiasa ni wepesi kuhujumu kuwepo kwa utendaji mzuri Serikalini, ikiwa watawatumia watendaji wa Serikali kufanikisha malengo ya kisiasa ya kubaki madarakani kwa kuiba kura ama kwa jambo lingine lolote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inawajibika kuwavutia watumishi wenye uwezo na ari ya kufanya kazi. Ni muhimu mishahara ya wafanyakazi Serikalini iwe inavutia, lakini utumishi Serikalini uzingatie uwezo na siyo mtoto wa nani au wa jamaa fulani. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kila sekta ambayo tumeiongelea maana yake kuna faida inayopatikana na kuna fedha zitakazopatikana. Tunaomba ziada yote ya fedha ipelekwe kwenye miradi ya miundombinu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, orodha ya wachangiaji ipo tayari na mpaka sasa tuna wachangiaji 22, lakini mchangiaji wetu wa kwanza ambaye anaweza akatumia dakika hizi tulizonazo sasa ni Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa na mimi kama ilivyo ada, nianze kwa kuwatakia heri ya mwaka mpya, wapiga kura wangu wa Kasulu Mashariki na Wilaya yote ya Kasulu na Watanzania wote. Kwa wale wa Kasulu Mashariki, niseme huu mwaka ni mwaka wa majukumu makubwa na hasa Uchaguzi Mkuu tunaokwenda nao mwezi Oktoba; kwa hiyo tutakiane kila la heri tukutane huko tukiwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, moja kwa moja nianze kwa kuchangia katika maeneo matatu, manne hivi; nitaanza na msingi wa bajeti, halafu nitagusia kipaumbele halafu nitagusia matumizi ya Serikali. Matumizi makubwa ya Serikali na vyanzo vya mapato ambavyo kwa maoni yangu, nafikiri vinapaswa viwe vyanzo ambavyo wenzetu wa Wizara ya Fedha wangejielekeza kutafuta pesa zaidi katika uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijachangia, nianze moja kwa moja kukubaliana mia kwa mia na Taarifa hii ya Kamati ya Fedha; kwenye *document* hii Wajumbe wametoa kitu kizuri na niombe Bunge lako Tukufu na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba, mengi yaliyozungumzwa humu ndani ni ya msingi sana hasa maeneo ya nchi, kuitizama kama *unit* moja na siyo kuitazama vipande vipande au vijimbo jimbo hivi au vieneo; kuitizama nchi kimkakati kama *unit* moja na kuangalia zile fursa za kijiografia. *Paper* hii imenigusa na ningekuomba Mheshimiwa Waziri uichukue hii kama *working document* katika taratibu zenu kwani imekaa vizuri. *(Makofi)*

Wenzetu wa Kambi ya Upinzani, naona wao wamehama wakaja kwenye utekelezaji na utendaji zaidi, pengine na hili litam-*guide* Mheshimiwa katika bajeti katika baadhi ya mambo ambayo wameyatekeleza. Lengo la leo, Mheshimiwa Hamad Rashid,

lilikuwa ni kuzungumzia mwongozo, kujiingiza kwenye dhana zaidi kuliko utendaji, lakini bado uliyoyachangia kwenye utendaji ni dhahiri Mheshimiwa Waziri atayazingatia katika bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na hili la jumla; tukiangalia kwenye kitabu chetu ambacho Mheshimiwa Waziri ametupitisha, amezungumzia msingi wa bajeti au msingi wa kupanga mipango akizingatia Dira ya Taifa 2025, Malengo ya Milenia, Ilani ya Uchanguzi ya CCM, Malengo ya Kilimo Kwanza na Malengo ya Mikoa, Wilaya na Halmashauri zetu. Kwa tafsiri yangu tu ni kwamba, yote haya ni ndio chimbuko la mipango yetu.

Niseme tu kwamba, ndiyo msingi wa bajeti yetu na kwa sentensi moja, iwe Dira ya Taifa 2025, Malengo ya Milenia, Ilani ya Uchanguzi ya CCM, Malengo ya Kilimo Kwanza; kwa sentensi moja ni kupunguza umaskini. Lengo ni hilo tu, watu wetu ni maskini na mipango yote hii au msingi wa bajeti lazima ujielekeze kupunguza umaskini na nikubaliane na Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi na nadhani kuna tathmini kwa kina ni kwa nini mipango yote hii ambayo imegharimu fedha nyingi hizi lakini umaskini wetu haupungui, uchumi unaongezeka; sasa tunaambiwa unakua kwa asilimia takribani 6; matarijio yetu ni 6.1, lakini umaskini unazidi kuwa mkubwa katika maeneo ya vijijini. (*Makofi*)

Nadhani kuna mahali mambo hayako sawa sawa na ningefikiri sasa wenzetu kile Kitengo cha Mipango, kingejikita zaidi katika kufanya tathmini ni wapi tumekosea, maana haiwezekani kuwekeza fedha nyingi katika Dira ya Taifa 2025, Malengo ya Milenia, Ilani ya Uchaguzi ya CCM, ambayo Wabunge wote tunashiriki kuitekeleza, Malengo ya Kilimo Kwanza, lakini bado umaskini ni mkubwa kiasi hicho. Nafikiri kuna mahali ambapo tufanye tathmini ya kina na kwa sababu tunaingia kwenye MKUKUTA Phase Two, basi tujiekeleze katika kufanya tathmini ni wapi tumekosea ili MKUKUTA Phase Two pengine uweze kuwa na maana zaidi; vinginevyo, tutakuwa na tatizo, tutawekeza fedha nyingi katika mipango, lakini bado tatizo la umaskini lenyewe halitapungua wakati ndio malengo yetu ya kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye *paper* hii, ukiangalia zile sekta ambazo Mheshimiwa Waziri amezitamka kwenye ukurasa wa 32 wa kitabu hiki, vipaumbele viko kama kumi au kumi na tatu; ametaja barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege, nishati, elimu, afya, maji ya kunywa, ardhi na viwanda. Ukihesabu zile *subsectors* ni karibu kumi na mbili; sasa nachelea kuamini kwamba, tunaweza kuwa na vipaumbele 12; nafikiri hatujajielekeza sawasawa. Vipaumbele kwa tafsiri yangu lazima viwe vichache, ambavyo tutawekeza kwa nguvu zetu zote kwa rasilimali fedha na rasilimali watu. Hiyo haina tafsiri kwamba, sekta nyingine zitaachwa ziendelee lakini tutajielekeza zaidi kwa maana ya kwamba, *focus* yetu itakuwa katika maeneo hayo machache na ni dhahiri hayawezi kuwa yote haya; nafikiri kosa tunaanzia hapo. Kwa hiyo, ile dhana ambayo Mheshimiwa Waziri ameitaja ukurasa wa 36, nafikiri kwamba tunatapanya rasilimali zetu; kwa tafsiri hii ya 32 ,tunatapanya rasilimali hizi kwa sababu vipaumbele ni vingi sana, huwezi kuwa na vipaumbele kumi na tatu ukasema una vipaumbele; haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri tatizo linaanzia hapo, kwa hiyo, tuwaombe wataalam kule Hazina wakae chini tujielekeze kwa kuzingatia hii *document* ya wenzetu wa Kamati wa Fedha; hivi vipaumbele vya taifa ni vipi na vipaumbele vya taifa huwezi ukavi-*define* bila kuangalia matatizo ya taifa. Matatizo ya taifa ndiyo yanakuja baadaye, ku-*define* vipaumbele vya taifa na hili ndiyo litakalotuondoa katika kufika mahali tunakuwa na fedha, lakini tunazitumia katika mambo ambayo mengine ni ya ovyo ovyo, hayaendi sambasamba na vipaumbele vyetu na hayaendi sambamba na kupunguza umaskini wa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka, mtoa hoja anazungumzia habari ya umwagiliaji, uvuvi, kilimo na mifugo. Bila ku-*define* hivi kwenye umwagiliaji tuna maana gani; Kiongozi wa Kambi ya Upinzani amelizungumza kidogo hili upande wa chakula; hivi tukizungumzia umwagiliaji maana yake nini hasa? Hivi scheme ndogo ndogo maana yake nini? Umwagiliaji maana yake nini? Kimkakati tukizungumzia masuala ya umwagiliaji *(Irrigation Schemes),* tunataka kutafsiri kitu gani? Lazima tuwe na tafsiri pana ambayo ni ya kimkakati. Uje kwenye miundombinu, barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege na nishati; hivi kipaumbele chetu ni nini; na kama ni barabara ni barabara zipi hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka ubishi uliokuwepo bajeti iliyopita, nadhani hoja aliibua ndugu yangu Mheshimiwa Diallo pale, ambayo kila mmoja alimuunga mkono kwamba ,tumezungumza barabara kama kipaumbele lakini barabara zipi? Tumechukua barabara za ovyo ovyo tu kwamba ndiyo kipaumbele chetu, lakini barabara za kimkakati, barabara za kiuchumi, ambazo zitatusaidia kutengeneza fedha tujenge barabara nyingine tumeziacha. Sasa hakuna nchi duniani ambayo imekwenda katika mtazamo huu ambao tunakwenda nao sisi haiwezekani.

Ukizungumzia barabara lazima uwe *clear,* unazungumzia barabara zipi? Bajeti iliyopita mimi nilizungumzia kuhusu barabara nikasema, nchi hii tuna barabara kubwa tatu ambazo tunazihitaji kimkakati; barabara ya kwanza ni ya Tunduma – Sumbawanga – Mpanda – Kanyani; barabara ya pili ni Kigoma – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi, ambayo inakwenda mpaka Muhutu mpaka Uganda; barabara ya tatu ni hii ya Itigi – Tabora – Kigoma – Malagarasi Bridge unakwenda mpaka Kongo, DRC.

Mheshimiwa Mkulo, huko DRC kuna mzigo ambao unahitaji kwenda Ulaya kupitia Bandari ya Dar es Salaam wa trilioni 2.3, upo DRC ya Mashariki. Sasa jana nimeshtuka kusikia Waziri anazungumza habari ya eti hizo ndoto za kuanzisha Reli ya TAZARA itoke Lubumbash - Kapilimposhi - Dar es Salaam, njia ya mkato ni hii ya Kigoma; sasa huo mzigo wa Kongo umekaa hauna jinsi ya kwenda Bandari ya Atlantic ni mbali zaidi, wanahitaji kupitia njia ya Dar es Salaam na huwezi kukarabati na kupanua na kuboresha Bandari ya Dar es Salaam bila kuboresha reli na barabara; hivi vitu vinakwenda pamoja na uzuri tuna Mheshimiwa Rais, ambaye dunia anaifahamu, anapita duniani anaomba mikopo na misaada; tujikite katika mambo ya msingi.

Mheshimiwa Mkulo trilioni 2.3 zipo Kongo DRC na hizo lazima tuwekeze katika Reli yetu ya Kati na barabara hii ya kwenda Kigoma - Tabora - Malagarasi Bridge hadi kwenda Kigoma. Hayo ni mambo muhimu sana na bila hayo tutabaki tunacheza ngoma tu, lazima ule ili uliwe. Sasa hatuwekezi tunazungumza tu na urari hatuna, lazima uliwe kwanza ndio ule; kuna mzee mmoja alisema maneno hayo, sasa ningeshauri sana Mheshimiwa Mkulo tujielekeze katika eneo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni matumizi ya Serikali; tunamshukuru Mheshimiwa Waziri amekuwa akizungumzia matumizi ya kiSerikali, magari ya kifahari na matumizi mengine yasiyokuwa na maana Serikalini na kwenye vyombo vyetu. Mimi nilikuwa nafikiri kupitia mwongozo huu, tumwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu, akaze kamba; nchi hii tuna shinda tunanunua magari ya kifahari ili iweje? Tunashindana kununa VX ili iweje; ndio tunapunguza umaskini wa watu wetu?

Yapo mambo ambayo tunaweza tukayafanya bila hata kuhitaji Wazungu. Fedha zetu za ndani tuzitumie vizuri, tu-*behave* kama watu maskini, nchi yetu hii bado ni maskini, lakini ni dhahiri kwamba, sasa Mawizara yanashindana kununua magari ya kifahari kana kwamba ndio kupunguza umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu, nafikiri tumwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu, aendelee na juhudi alizozianza za kupunguza matumizi Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni vyanzo vipya; mimi nilidhani wenzetu wa Wizara ya Fedha na Uchumi, wangejielekeza kwenye *new sources of revenue*, maeneo mapya ya kupata fedha ambayo ni pamoja na Sekta ya Umeme na Gesi. Mimi nipo kwenye Kamati ya Nishati na Madini, tumekwenda Songosongo, pale kuna visima sita lakini kinachotumika ni kimoja, vingine viwili ile gesi haina jinsi ya kufika Dar es Salaam; wale Wazungu tumefika pale Songosongo wanatushangaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ninakushukuru sana Mheshimiwa Nsanzugwanko kwa mchango wako. Waheshimiwa Wabunge, mjadala umeanza kushika kasi na kama nilivyosema, idadi inazidi kuongezeka na sasa tumefika 27; niwataje watakaoanza kuchangia tutakaporudi saa kumi na moja; Mheshimiwa John Momose Cheyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwanne Ismail Mchemba.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuwataja hawa, naomba sasa nisitishe shughuli hizi mpaka saa kumi na moja jioni.

(Saa 07.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tuketi. Tunaendelea na hoja yetu. Kama nilivyosema, tutakaporudi saa kumi na moja tutaendelea na mchango wa jumla

kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na Mwongozo wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2010/2011 na kama nilivyokuwa nimesema, mchangiaji wetu wa kwanza kwa jioni hii ya leo atakuwa Mheshimiwa John Momose Cheyo, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Mwanne Ismail Mchemba, Mheshimiwa Peter Serukamba ajiandae na kama Mheshimiwa Job atakuwa ameingia atafuatia.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia katika hoja hii muhimu. Awali ya yote, napenda kutoa pongezi nyingi sana kwa wapiga kura wangu walioko Gambasingu na Kisesa, kwa kupata daraja; na hapa tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa kutimiza ahadi yake. Sasa wanaopata matatizo shauri yao, lakini sisi tumepata daraja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema hivi; yale tuliyoletewa na Waziri wa Fedha ni mwanzo tu wa mchakato mrefu wa kuhakikisha kwamba, Bunge hili linashiriki katika kutengeneza Bajeti ya Serikali. Hatujafika, lakini tuko njiani na mwanzo ni mzuri na kwa hili, nataka kumpongeza Waziri pamoja na Wafanyakazi, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya ya kuleta mbele ya Bunge lako.

Bajeti Shirikishi ndiyo mtindo wa siku hizi wa Mabunge yote Duniani na wengi tunapotembea na kwenda kwenye *forum* mbalimbali za Mikutano ya Mabunge tunaulizwa; je, ninyi Wabunge mnashiriki vipi? Je, ninyi Wabunge mnaweza mkageuza hata takwimu kwenye bajeti ya Serikali? Jibu kusema kweli kila wakati inakuwa ni kumung'unyamung'unya tu, lakini ukweli ni kwamba, dhana ya kupanga Bajeti ya Serikali imekuwa ni shughuli ya Serikali peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, huu ni mwanzo mzuri na lazima tuuendeleze, lakini kuna vitu vya kufanya na sitaki kurudia; mambo mengi yamezungumzwa lakini la kwanza, kuwepo na Tume ya Mipango ni jambo ambalo ni la lazima kabisa. Tunachozungumza hapa ni ushiriki wa Bunge, kwa hiyo, pamoja na kuiimarisha Tume ya Mipango, basi Bunge pia liimarishe Ofisi ya Bajeti na ndani yake pawepo na *Budget Committee*, siyo *Budget Committee* tu bali ofisi ya bajeti. Halafu na mipango yenyewe au bajeti yenyewe kama walivyofanya Uganda, bajeti ya mwaka 2011/2012 ndiyo iko kwenye Ofisi ya Bunge inajadiliwa, inaangaliwa kipengele kwa kipengele, tutakapofika kwa mwaka unaohusika ni kujazajaza namba tu na kugeuza, lakini tayari mpango umeshakuwa tayari na pia Wabunge wameshiriki kwenye bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naona changamoto kwa Bunge ni kuweza kuweka Ofisi na Kamati ya Bajeti. Jambo lingine, sioni kwa nini kwa miaka yote bajeti yetu inaanza mwezi wa Juni, mwisho wa bajeti ndiyo mwanzo wa kuijadili bajeti.

Mtindo huu umepitwa na wakati, bajeti inazungumzwa kabla ya mwisho, hakuna uchawi wowote unaozuia bajeti kuanza kuzungumzwa mwezi wa Aprili, tunapofika Juni tumeshamaliza kuidhinisha *vote* zote halafu bajeti inaanza kutoka Julai Mosi. Sasa hivi bajeti yetu tunamaliza kuzungumza mwezi wa August, hakuna hela inayotoka na zaidi ya maendeleo, tunakwenda Krismas watu ndiyo wanaanza kutafuta hela, hakuna hela

inayoondoka. Kwa hiyo, kusema ukweli hatuna bajeti ya miezi kumi na mbili, tuna bajeti sana sana ya miezi sita; jambo ambalo kwa maoni yangu haliridhishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya vipaumbele; nimeangalia vipaumbele hapa, lakini nafikiri kipaumbele *number one* ni ukusanyaji wa mapato. Kwa sababu tunazungumza hapa matumizi na Bunge lako, kwa mtindo tulionao tunakaa karibu miezi miwili hapa, tunanyang'anyana, nipe hiki, nipe kile, ni mara chache sana tunatumia muda kuzungumza hiyo fedha inatoka wapi. Mimi naona hii ni sehemu mojawapo ambayo hata Kitabu cha Nne ambacho kinazungumzia juu ya vyanzo vya mapato huwa kinakuja Bungeni kwa kusuasua na hakiangaliwi, tunaangalia vitabu vya matumizi peke yake. Kwa hiyo, hili Bunge linadhihirisha matumizi, lakini hatuweki mkazo sana juu ya fedha hizi zinakotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri katika miaka inayokuja, Bunge litahadharishwe kuzungumzia zaidi juu ya mapato yanayotoka ili tuhakikishe kwamba, kweli tuna fedha ya kutosha ili kuweza kutumia vipaumbele mbalimbali. Kipaumbele cha ukusanyaji wa mapato, nataka kusema kwamba, misamaha ni mingi mno. Ukiangalia CAG, kwa mfano, amefanya utafiti wa 2007/2008, jumla la fedha yote ambayo ilisamehewa mwaka huu ni bilioni mia saba na thelathini na tatu na ushee kidogo na wengi waliosamehewa ambao ni zaidi ya asilimia hamsini na tisa, waliochukua bilioni 47 ni makampuni binafsi. Wewe unapiga kelele sana juu ya Mashirika ya Dini, ambayo hata bilioni mbili hazijafika; ni asilimia moja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna changamoto hapa. Tunategemea makampuni yale yatulipe fedha, lakini kama tunawapa pesa nyingi hizo kwa ajili ya misamaha ya kodi, ndiyo kusema kwamba, hatubakiwi na hela ya kutosha kwa ajili ya matumizi ambayo tunayahitaji. Tunahitaji pia katika TRA pawepo na *Research Unity* kabisa ya kushughulikia vyanzo vipya kutoka misitu, nyama; mnaidharau nyama ya ng'ombe nayo inaweza kuwa chanzo kikubwa sana cha mapato ya Serikali.

Tungependa pia kuona pawepo na utafiti juu ya vyanzo vya Halmashauri, maana sasa hivi Halmashauri ni tegemezi sana kwa Serikali Kuu na vyanzo vyao vyote viko kwenye Serikali. Basi tutafute njia ya kuimarisha pia mapato ambayo tunaweza kukokotoa kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele ambacho kimetajwa kuwa *number one* ni kilimo. Mimi nakubali, lazima tusaidie kilimo na kwa yote yale ambayo yamezungumzwa, baada ya kupata matatizo haya ya kiuchumi kiulimwengu, naunga mkono na tunashukuru sana sisi ambao tunalima pamba, kupata shilingi themanini kwa kilo. Rais alipokuwa kule nilimwambia bwana angalia hii kitu kiendelee hata mwaka ujao. Ninasema hivyo kwa sababu kama unavyofahamu, tabia nchi haiwasaidii wakulima; wakulima leo hawajui majira, hawajui kama mvua inakuwa nyingi au inakuwa chache sana, kilimo chenyewe cha pamba kwa mfano, mara ukichanganya mahindi na pamba unawekwa ndani, huna uhakika wa bei! Kwa hiyo, wale wakulima ambao wanalima pamba wanahitaji hii motisha ili waendelee kulima pamba, tupate fedha za nje.

Kwa hiyo, katika mpango wa mwaka huu, isiwe dharura tena, themanini ile iwe katika bajeti kabisa ili tuhakikishe kwamba tunaendelea na mtindo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaridhika Serikali ilivyoweza hata kutukumbuka sisi watu wa pamba kwamba, sasa pembejeo za madawa tunapata kwa nusu bei na vocha imeanza kutumika. Tuendelee hivyo kwa sababu tusifike mahali ambapo tunapendelea chakula tu au tunapendelea sehemu moja tu, hii fedha ni ya Watanzania wote, tunasema panapowezekana kusukuma pesa kama hivyo kusaidia upande kwa pembejeo, tuendelee. Tusiwe na woga, hawa Wazungu wanatuambia ninyi msiweke *subsidy*, lakini kwao wanafanya. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba, jambo hili Waziri wa Fedha aliwekee fedha kabisa ili kuhakikisha kwamba, tunaendelea na mtindo wa kuweza kuwasaidia hawa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wetu nimeangalia katika Ripoti yako, unazungumza juu ya matrekta mia nne, unazungumza juu ya *power tiller;* kwa maoni yangu, kusema kweli Serikali haipaswi kununua *power tillers*, Serikali inapaswa kutengeneza utaratibu wa watu wanaotaka kununua *power tillers* kukopa. Bariadi ukitununulia *power tillers* ishirini au thelathini zitatusaidia kitu gani na utazigawa vipi? Huu ni mtindo ambao umeendelea na sioni kama ni matumizi mazuri sana ya fedha ya Serikali. Sisi tuna *power tillers* zetu, ng'ombe, sasa tusaidieni tupate mikopo ya kunua *plough* na maksai wazuri zaidi; hiyo ndiyo *power tiller* yetu na ndiyo maana tunalima vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kushauri kwamba, sasa hivi kwa upande wa kilimo, ardhi imekuwa ni tatizo; watu wengi sana wanashindwa kupanua kilimo chao kwa sababu ya uhaba wa ardhi. Mimi naona hapa kuna changamoto ya Serikali, tujaribu kuangalia kati ya kuhifadhi na pia kuweza kutoa ardhi watu waweze kuitumia na pia tuweze kuangalia ni maeneo gani nchini tuwaambie watu waliobanana sehemu fulani wahamie huko wakafanye kilimo endelevu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya kipaumbele nishati; kwanza, nasikitika kwamba, kila siku tunazungumzia juu ya nishati, lakini historia ya fedha tunayotoa kwa nishati, haiendani na maneno tunayopewa na zaidi tunapoweka umuhimu zaidi kwa kutegemea fedha za nje. Kwa mfano, kwa Wizara ya Nishati, mwaka 2007/2008, bajeti ile kwa upande wa fedha inayotoka nje ni asilimia 7.6 tu ndiyo iliyotolewa. Mwaka 2008/2009 ni asilimia 11 tu, mpaka hivi sasa mwezi wa Juni kwa upande wa nishati ni asilimia 0.23 ya bajeti yote ndiyo imetolewa kwa hivi sasa kwa fedha za kutoka nje hata za ndani ni bilioni 13 tu. Sasa kama hii ndiyo historia na tutaendelea nayo ni wazi tu kwamba, *we are not serious*, yaani hatuweki umakini katika kuhakikisha kwamba, tuna nishati itakayowakilisha uendelevu wa viwanda na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa hili jambo liwekewe kipaumbele na fedha za kigeni na za wafadhili ziwekwe hapa, tuweke fedha zetu za ndani kwa sababu wameonesha ukiangalia kwenye park fedha za ndani zinafanya vizuri. *The current budget is an excellent performance*. Hata hela inayowekwa kwa *development* ya *local* inapatikana. Sasa tuwekeze sisi *locally* kuliko kutegemea wafadhili. Miundombinu hivyo

hivyo; ukiangalia 2007/2008, tuliahidiwa asilimia 15 tu ya fedha ya nje, afadhali 2008/2009, fedha ya nje tuliyoahidiwa ilipatikana, karibia asilimia 89. Mwaka 2009/2010, sasa hivi ni 1.3 ndiyo imepatikana. Kwa hiyo, hapa ningeshauri kwamba, basi maneno yetu na matendo yetu yafanane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kwa miundombinu; nasisitiza Reli ya Kati ni muhimu sana kwa uchumi wetu. Hapa tusiende kona kona, kama Mkataba wa *RITES* haufai ufutwe mara moja na Serikali iwekeze mara moja siyo tena mara tungoje sijui upembuzi yakinifu, sijui kitu gani; tunataka hiyo reli. Hi ndiyo reli ya wanyonge, itahakikisha kwamba, bidhaa zinakwenda Kanda ya Kati na bidhaa itakuwa nafuu, lakini kwa hali tunayokwenda nayo, mimi siridhiki na naomba hiyo habari ifike Serikalini. Sisi tunaotoka Kanda ya Ziwa, tunaotegemea Reli ya Kati, haturidhiki hata kidogo na hatua ambayo Serikali inachukua katika kuiimarisha sehemu hii. Kipaumbele hiki kifanyiwe kazi.

Ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuzungumza. *(Makofi)*

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi jioni hii niwe mchangiaji wa pili katika mpango wa vipaumbele vya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2010/2011. Awali ya yote, nichukue nafasi hii ya pekee kutoa salamu za rambirambi kwa familia ya Marehemu Mzee Kawawa; nawapa pole hasa ukizingatia kwamba, Marehemu alioa kutoka Tabora. Nampa pole sana mkewe na kwamba, tuko pamoja katika majonzi hayo yaliyomfika. Mwenyezi Mungu, aiweke roho yake mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kuipongeza Serikali kwa kusikia vilio vya Wabunge, imeelewa malalamiko yao, sasa inatushirikisha kwa haya yafuatayo:-

Inatushirikisha katika mpango, tutoe mawazo yetu ingawa mipango imepangwa lakini waende kuiboresha. Kwa hiyo, tunachofanya hapa ni kuongeza tu kabla vitabu vya mahesabu havijapitishwa rasmi na kuletwa kwenye Bunge la Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa niende kwenye taarifa ya mapendekezo ya vipaumbele. Vipaumbele vilivyooneshwa humu ndani, bado nataka niviboreshe ili itakapofika wakati wa bajeti twende sambamba. Kwa kuwa bajeti hii au mpango huu unaandaliwa na wataalamu, lakini wale wataalamu hawapo kwenye maeneo yetu. Nataka kuzungumzia kero kubwa tunazozipata sisi wanasiasa kama alivyozungumzia Mheshimiwa Cheyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kuhusu reli, ningependa niishauri Serikali iangalie jiografia ya Tanzania na umaskini uliokithiri kwenye maeneo mbalimbali, halafu ndiyo wapitishe bajeti ya miundombinu. Nitakwenda haraka kwa sababu muda wenyewe hautoshi. Upande wa Kanda ya Ziwa, suala zima la reli ni kero. Ungeniuliza sasa hivi ningesema huo mkataba ufutwe usiwepo, kwa sababu Serikali iliweka mkataba kwa nia nzuri, wakichukulia kwamba, hawa wenzetu wataibeba Serikali

kwa yale waliyonayo; wameshindwa au hawataweza kibiashara, lakini matokeo yake huyu tuliyempa ndiyo adhabu yake tunayoipata hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo yaliyotokea Godegode, Kilosa ni kama mtazamo tu wa Mwenyezi Mungu, anatuonesha madhara tunayoyapata. Kwa sababu tatizo lile lilipotokea, la kusitishwa reli na reli kuharibika miundombinu, maana yake Watu wa Tabora, Kigoma na Mwanza walibaki Dar es Salaam. Watu wa Mwanza walibaki Mwanza, ambao wanategemea kwenda Dar es Salaam, hawana uwezo wa kupanda mabasi. Mabasi yalisitisha safari zote; inasikitisha sana, lakini nimpongeze Waziri Mkuu, leo asubuhi amezungumza, amefafanua angalau hata *pressure* imetulia kwa sababu tunaamini kwamba, Serikali itafanya nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kungekuwa na treni inaanzia hapa, angalau watu wangesafiri wangefika Kigoma na Tabora; tungekuwa tuko kwenye neema. Nimesema jiografia kwa sababu Tabora hatuna barabara ya aina yoyote ya lami ambayo inaweza kutuunganisha; endapo tungekuwa na barabara kama vile Songea, Dar es Salaam au Arusha, masuala ya reli yangekuwepo lakini yasingekuwa kero; tungesema Serikali ijipange.

Ninaomba katika kipaumbele cha reli, Serikali ifanye mambo mawili; iendelee kuikarabati na kuisimamia Reli ya Kati kuhakikisha inafanya kazi, kwa sababu kwa hivi sasa ninavyokueleza, Watu wa Kigoma hawaendi wapo Tabora wamekaa; watakwenda na nini? Hakuna mabasi wala hakuna njia, inasikitisha sana. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Waziri kwa sababu sasa unakwenda kwenye bajeti, sitaki kwenda kwenye takwimu za asilimia. Uliweka wataalamu wako, walipe kipaumbele suala zima la reli ili bajeti hii izingatie hili ninalolisema leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwenye barabara; sasa hivi barabara ya kutoka Dodoma kwenda Tabora mpaka Kigoma, haipitiki; mimi mwenyewe nilikwama njiani, ikinyesha mvua ni tatizo. Kwa hiyo, umeona ni jinsi gani tulivyokuwa kisiwani. Tabora na Kigoma tuna matatizo makubwa; mimi kila nikizungumzia Tabora nazungumzia na Kigoma, watu wanakwenda na nini Kigoma? Wamekwama, kwa sababu hakuna njia ya kuwafikisha Kigoma. Kwa hiyo, nadhani ifike mahali sasa kwa Serikali iangalie jinsi gani fedha zitapelekwa Ukanda huu wa Magharibi hususan barabara na reli ili angalau tusitegemee asilimia kubwa ya wafadhili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba nijazilizie hapo ili Serikali iweze kuona ni jinsi gani Watu wa Tabora na Kigoma tunavyohangaika. Vifaa vimepanda, tunafanya kazi katika mazingira magumu, umaskini umekisiri kwa sababu hatujui tushike wapi na twende wapi.

Tatizo lingine linalotukabili ni maji. Nimeona hapa, siyatoi kichwani. Wamesema, vipaumbele kuna kilimo, miundombinu, huduma za jamii; katika huduma za jamii wamesema elimu, maji na afya. Mimi nachukua maji, kuna Mpango Mkakati wa *World Bank* kwa ajili ya kuandaa mfumo mzima wa maji, lakini hivi karibuni nakwambia Watu wa Tabora siku tano hatuna maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Manispaa ya Tabora hakuna maji kabisa kutokana na tatizo la mfumo mzima wa miundombinu, Bwawa la Igombe limejaa tope kiasi ambacho hata mitambo inashindwa kuvuta; Kazima imekauka; hivi hawa wananchi wanaishije? Kazima ikijaa maji na ikiwekewa miundombinu itapita kwenye Kata nyingi sana, kwa hiyo, tatizo la maji halitakuwepo. Ukija Igombe, itainywesha maji Tumbi, Misha, Tabora na kadhalika. Kwa hiyo, hatutakuwa na tatizo la maji. Mimi ninaiomba Serikali ihakikishe mabwawa haya mawili yanakarabatiwa iwezekanavyo kwa fedha ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu sasa hivi Tabora tuna hali ngumu sana ya maji; maji, hakuna maji, yaliyopo ni machafu na hayafiki kwa watu na bili tunapata, lakini hayo tuyaache; ni jinsi gani utendaji na utekelezaji utakavyokuwa kwenye bajeti? Ombi langu kwa Mheshimwia Waziri na Wataalamu wake, bado nasisitiza waangalie jiografia, waangalie maeneo yalikokuwa nyuma, waangalie ni jinsi gani wanaweza kuisaidia Tabora ili angalau nayo iweze kuonekana kwamba ni mtoto wa Tanzania, maana sasa inaonekana kama tuko Burundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonekana kama siyo Tanzania, kwa jinsi watu wanavyopata shida. Kwa hiyo, hilo nilitaka nilizungumzie ieleweke kwamba, mimi naboresha tu ili huko wanakokwenda wataalamu wakafanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la kilimo na pembejeo. Kwa kuwa tuna kilimo kwanza ni vizuri sasa tukaanza kuainisha takwimu halisi za wakulima wetu na mahitaji yao kila Mkoa na kila eneo.

Kwa mfano, sasa hivi hizi pembejeo za mbolea zinapokwenda, Manispaa ya Tabora haiunganishwi na Tabora ni Manispaa. Manispaa ina Kata ishirini na moja; Kata nane ni za wakulima lakini hawapati ruzuku, wala mbolea; wanaondolewa kabisa kwenye bajeti kwamba, mbolea inayoenda huko iende kwa walengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mwaka huu mbolea imepungua sana hasa kwenye tumbaku. Watu wengi wameng'oa tumbaku, wameziondoa kwa sababu ya takwimu. Kwa hiyo, nilichokuwa nasemea ni kwamba, kwa kuwa si sehemu ya bajeti *as such*, niombe tu Wizara inapochukua takwimu zake za kilimo, basi iangalie kwamba, Tabora Manispaa katika bajeti zao ina Kata nane ambazo ziko nje ya Manispaa. Kwa hiyo, Kata hizo pia ziangaliwe wanapogawa fungu kubwa la pembejeo. Suala lingine ambalo ningependa nilijazie ni kwamba, bajeti kama bajeti inapokuja, basi iangalie sehemu kubwa ya mjadala wa Wabunge kuhusu tatizo zima la mahitaji na matakwa ya maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni upande wa afya. Ningeshauri wataalamu wetu wangalie suala la afya, wanapopanga bajeti yao, bajeti izingatie pia maeneo hayo ambayo nimeyataja kwamba, sasa hivi tuna matatizo makubwa mno kutokana na bajeti ufinyu wa maeneo ya jiografia ya Magharibi kwa sababu huu Ukanda una matatizo; kwa mfano, sasa hivi kuna zahanati nyingi ambazo zina upungufu mkubwa wa wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nilikuwa naomba bajeti hii pia izingatie madai ya watumishi wote kwa ujumla kwa nchi nzima, watu wenye madai yawe yamekwisha hususan walimu, polisi, watumishi wa afya na maeneo mengine ili tunapokwenda kwenye uchaguzi kusiwe na malalamiko na chuki ndani ya Chama cha Mapinduzi au ndani ya Serikali kuonekana kwamba haiwajali watumishi wake.

Kwa hiyo, nilitaka nijazilizie hilo na kwa sababu muda wangu unanitosha, nakukushukuru sana ya kwangu yalikuwa ni hayo. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwanne Isumaily Mchemba. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Sasa namwita Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba na Mheshimiwa Job Yustino Ndugai ajiandae.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie Mwongozo wa Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2010 kwenda 2011. Nami nianze kwa kuwatakia kila la kheri wapiga kura wangu na wananchi wangu wa Kigoma Mjini na kuwahakikishia kuwa, tunaendelea kuifanya ile kazi ambayo tuliwaahidi na tutaifanya kwa nguvu ile ile tuliyoanza nayo mpaka mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nimemsikiliza sana Waziri wa Fedha; tunalo tatizo la Kanuni, tumelishaliongelea vya kutosha, nadhani sasa ni muhimu tujadili hili ambalo lipo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejiuliza sana nikaamua kufanya *hypothetical*, nikasema Waziri wa Fedha ni kama kwenye *co-operate world;* ni *director* wa *operation* wa nchi hii. Waziri wa Fedha akiamua mambo yatokee nchi hii yatatokea, akiamua yasitokee pia hatatokea. Kwa hiyo, jukumu lipo mikononi mwa Waziri wa Fedha aamue tu. Mimi naamini akiamua yeye yatatokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nchi hii Chama cha Mapinduzi na Serikali zake zote, moja ya mambo makubwa yaliyofanyika ni kuhakikisha nchi hii kuna amani na utulivu. Mungu naye kwa sababu zake anazozijua yeye, akaiweka Tanzania hapa ilipo leo tunazungukwa na nchi nane; tuna bahari, mito, maziwa, mbuga za wanyama, madini na tuna kila kitu ambacho kila mtu angekitamani kuwepo kwenye nchi yake. Sasa ukianza kujiuliza haya makubwa mawili; tunayaweka kwenye mzania wa kuleta maendeleo ambayo mimi naamini kasi yetu ya maendeleo inatakiwa kuwa kubwa zaidi kuliko iliyopo sasa kwa sababu ya hizo sababu mbili kubwa nilizozisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nianze na vipaumbele, *with due respect to the Minister;* vipaumbele hivi ni vingi sana. Hatuna uwezo wa kuvitekeleza ingawa tunaweza kuamua tugawane kidogo kidogo sungura mdogo, lakini hakuna *impact.* Kwa hiyo, matokeo yake tutakwenda kila mwaka tunaongeza vipaumbele hivyo hivyo kwa sababu hatujaamua kwamba hili tulimalize.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najaribu kuviangalia vipaumbele halafu naviwekea pesa, tunahitaji shilingi ngapi na uangalie kwenye jedwali la pesa, mwaka huu tunafikiria kwenda karibu 9.5 trilioni ndiyo itakuwa bajeti nzima ya Serikali. Ukiangalia hivi vipaumbele kama kweli tunataka kutoka hapa tulipo, sioni kama hivi tunaviweza. Mheshimiwa Waziri, ametuambia jana na leo kuwa, *development budget* ya nchi hii ni *31 percent.*

Matumizi ya kawaida ni asilimia 69. Wachumi wanasema, angalau ili muweze kwenda kasi kubwa ya maendeleo, lazima *devopment budget* iwe 20% ya *GDP*. Ukichukua *GDP* ya Tanzania uki-*calculate 20%,* maana yake ilitakiwa *6 trillio*n ziwe ndiyo za maendeleo. Kinyume chake, siyo hivyo; sasa tunafanyaje kutoka hapa?

Kwa hiyo, la kwanza, nilitaka kusema suala la vipaumbele ni vingi sana. Ukiangalia matatizo tuliyonayo ya barabara peke yake *in the country*, kwanza, tuna madeni zaidi ya bilioni 230 ambayo inatakiwa tuyalipe. Kwa hiyo, inawezekana bajeti hii inakuja kulipa madeni wala siyo *project* mpya. Tukiamua kuweka *project* mpya maana yake ni nini? Ukichukua idadi ya kilomita inayotakiwa kujengwa, zidisha kwa bilioni moja unajikuta unahitaji karibuni trilioni moja kwa ajili ya barabara peke yake. Hatujajenga reli, bandari, viwanja vya ndege, miundombinu ya maji, skimu za *irrigation* wala kilimo. Kupanga ni kuchagua, Mwalimu alituambia lazima tuamue tunataka kufanya nini, lakini tuiangalie nchi yetu.

Wanasema *economic drivers* ndiyo zitupeleke kwenye kupanga vipaumbele. Nikijenga barabara itaniletea pesa, kama haitaniletea pesa nitaachana nayo nitakwenda kwenye kitu kingine ambacho nikikifanya nitapata pesa. Kwa hiyo, nawaomba wachumi wakubwa wa nchi hii, watusaidie kwenye vipaumbele hivi. Haiwezekani, dunia ya leo haitusubiri, nenda ukaone *investment* inayofanyika leo Mombasa ya kuipanua bandari ya Mombasa, sasa hivi wameanza kujenga bomba la mafuta kutoka Mombasa kwenda Eldoreti, wanakwenda Uganda watafika Rwanda mpaka Burundi. Wameanza kupanua treni kwenda kwenye geji 120 kutoka Mombasa Kenya kwenda Uganda mpaka Rwanda. Wameanza kujenga barabara *double line* kutoka *port* kwenda mpaka Uganda na Rwanda; maana yake Tanzania tunaachwa pembeni. *(Makofi)*

Mimi najiuliza; *economic intelligence* yetu inafanya nini? Huhitaji digrii kuyajua haya kwamba, tukiwaacha wenzetu wakamaliza sisi tutakuwa *feeder road* ya Mombasa. Tuamue, tunajua kusema na tumeandika vizuri sana; haya tuliyoyaandika yanatosha, tuyapeleke kwenye *implementation, it is high time, we can't say* Mjerumani alijenga reli miaka 100 iliyopita, bado ni ile ile; hatuitendei haki nchi hii. Wenzangu wamesema, tuwafukuze *RITES, problem* siyo *RITES*, hii reli ni ya kwetu kwani *RITES* tukianza kujenga reli watatukatalia leo? Reli hii tunaihitaji ili tuweze kupunguza gharama za kufanya biashara, hatuwezi kila siku kufanya kazi ya kulalamika tatizo letu ni fulani, tatizo ni letu wenyewe. Tunahitaji kwenda Kigoma, tunahitaji kwenda kuchukua mzigo Congo, tunahitaji kwenda Rwanda ili tuweze kuwa *competitive.* Kama mmeamua tuendelee kusema, tutafute mtu wa kumpelekea lawama tuendelee. Mimi nasema tuache, umefika wakati tutekeleze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasema, tuulizane vizuri, moja ya *area* ambayo na mimi nitasema leo kama kuna jambo nikienda Kanisani namwomba Mungu litokee nchi hii, wafadhili wakatae kutupa mikopo nchi hii ndiyo itaendelea. Ninaomba Mungu wafadhili wakatae kutupa mikopo nchi hii ndiyo itaendelea. Nasema leo mtanisamehe, kwa sababu mikopo hii imetufanya sasa hatutaki kufikiria tena. Matokeo kila siku tunakuja tunasema unajua hatujatekeleza kwa sababu wahisani hawajaleta pesa. Wahisani namna gani, tunazo hela kwenye *Other Charges* tupunguze, kama tunataka tule milo mitatu, tuifanye iwe miwili. Hata nyumbani kwako ukitaka kuleta maendeleo lazima unajifunga. Hatuwezi kuendelea huku tunakula kuku, haiwezekani. Tufikirie familia zetu, hivi wakati unajenga kibanda chako hufanyi *saving* kweli; hujinyimi kweli? Sisi tunataka nchi hii iendelee wakati hatutaki kujinyima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Obama anatangaza bajeti ya mwaka huu ya Nchi ya Marekani, nchi kubwa iliyoendelea, amepunguza matumizi *by 1.5 trillion dollars,* hii ni nchi kubwa iliyoendelea. Sisi hatutaki kupunguza matumizi, hatuwezi kuendelea kama hatutapunguza matumizi na nitawaambia vitu ambavyo viko kwa upande wa matumizi. Angalieni mfano mdogo sana; najua kuna watu watachukia, tumekuja Bungeni tumeweka machuma yale yanaongeza *value* gani kwenye hili jingo? Hii ni kwa sababu tuna *access money;* mfano huu unakwenda mpaka kwenye *Council* na kwenye Mawizara yetu. Serikali hii nenda ukaone leo tunavyopeleka mamilioni ya pesa, lakini jiulize *how much we are getting from Swaziland;* kila Wizara zetu watu kusoma Swaziland! Mimi nimekwenda; *there is nothing;* watu wanakwenda pale, wameandaliwa *trip* za kwenda Johannesburg na Durban wanakaa mwezi mmoja wanarudi! *This country* hatuwezi kuendelea.

Namwomba Waziri wetu wa Fedha, ndiyo maana nimemwambia yeye ni *Director* wa *Operation*, aamue wale Watendaji wakileta bajeti, wewe sema mwaka huu napunguza *Other Charges by 30%,* uone kama nchi hii itaacha kwenda. Ukipunguza *by 30%, you almost have one trillion,* amua mwaka huu hii *one trillion* naipeleka kutatua matatizo ya maji tu *in the country*, matatizo ya maji yatakuwa historia. Au unasema hii *Other Charges* nimekata *one trillion* napeleka kwenye barabara, *you have one thousand kilometers*, hivi ndiyo tutakavyoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunaamua hatutaki kupunguza matumizi, leo hii ni *fashion* na magari yakitoka baada ya miezi mitatu yamejaa kwenye Mawizara. *What is this?* Wabunge tulikopa magari *five years ago* mpaka leo tunayatumia, ni machakavu *fine*, lakini yanaendelea na kazi inakwenda. Kwa hiyo ni kujinyima, kupanga ni kuchagua. Tukishamaliza mambo muhimu tuanze kula kuku. *We have no problem.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo kazi ya Serikali. Lazima tuandae mazingira ambayo tuta-*create environment* ya watu kufanya biashara ili waje ku-*invest* Tanzania. Ili biashara ya ndani iweze kufanyika, kuna mambo lazima yafanyike; lazima tuangalie *policy issues* zetu zinasemaje, *legal and regulatory frame work* zetu zinasemaje; *fiscal infrastructure* yetu iko sawa; haya ndiyo ya kufanya ili mambo mengine yaende. Haya tunayosema tuandae mazingira, *market condition* zetu zinasemaje, *is it favorable for* watu

kufanya biashara. Tuna maeneo leo Kigoma Kusini watu wanalima, lakini hawawezi kufika kwenye masoko; mtu huyu hawezi kuendelea hata siku moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo lazima tuamue leo, lakini kwa *style* hii ya kuleta kila kitu, haitakiwi. La mwisho, niongelee *cost business in Tanzania*; jamani wenzetu huko hawatusemi vizuri, kufanya biashara Tanzania ni gharama. Angalia unatoka *Port* ya Dar es Salaam unakwenda Tunduma utasimamishwa kwenye malori karibu vituo 40; wapi kwenye dunia ipi? Ukitoka Kenya baada ya kukaguliwa pale Mombasa, utakaguliwa tena nje ya mpaka karibu na Uganda. Sisi unatoka Dar es Salaam unakwenda Tunduma, unakwenda Kigoma, utasimamishwa kila baada ya kilometa 50. Hauwezi kushindana duniani, lakini *above all* tumeamua kuweka na matuta. Mimi naamini wenzangu mmetembea duniani, niambieni ni *high way* gani ambazo zina matuta kama za kwetu? Tukubaliane *cost of doing business in Tanzania* ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mmeweka hapa kwenye majedwali, kuna nchi zimeacha kutupa misaada kwa sababu gharama za kufanya biashara Tanzania zimekuwa kubwa. Mfanyabiashara wa Kigoma ataendeleaje kama hana reli hii? Ataendeleaje kama leo anachukua kontena Dar es Salaam analifikisha Kigoma baada ya siku 30? Hawezi kuendelea huyu, hawezi ku-*compete* kwenye dunia ya leo. Tunakwenda kwenye *East Africa,* tusipokuwa tayari wenzetu watatuacha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, mimi narudia tena, wenzetu wa Serikalini wakakae, vipaumbele ni vingi; tuchague vichache tuweke pesa nyingi na wenzetu watatuelewa. Haiwezekani, toka uhuru tunajadili bado matatizo ya maji, ukienda pale Kigoma maji yapo nusu kilomita, halafu mita 100 eti Mji wa Kigoma hauna maji, sababu ni bajeti. Mwaka huu pelekeni milioni 400; kesho pelekeni; watatatuaje haya matatizo? *We could decide* kwamba, leo tuna-*slash* hizi *OC by 30%,* hela tunayopata yote tunatatua matatizo ya maji, baada ya miaka miwili Waziri wa Maji hana kazi, tunaendelea na jambo lingine. Ndiyo nchi hii itaweza kuendelea. Lazima tuamue leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru Mheshimiwa Serukamba. Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa nimwite Mheshimiwa Job Yustino Ndugai.

MHE. JOB Y. NDUGAI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kidogo katika suala lililo mbele yetu, linalohusiana na masuala ya Mwongozo wa Mpango wa Bajeti yetu inayotarajia kuja ya mwaka 2010/2011. Tunapojielekeza kwenye bajeti maana yake ni kwamba, tunafikiria kupanga kutumia *re-distribution* na hii huwa ni *emphasis* kubwa ya nchi za kijamaa. Alisema Mzee Cheyo mwanzoni kama nilimpata vizuri, wenzetu Magharibi wanakazania sana kwenye kukusanya; sisi hujikita kwenye kutumia na tunatumia muda wetu mwingi sana katika eneo hilo na ni sifa ya kila Mbunge, kasungura haka umechukua kiasi gani kupeleka jimboni kwako na ukipata nafasi ya kuwa kwenye meza ya mbele basi unakata kanyama kakubwa zaidi unapeleka kwako. Sisi tunajikita sana katika kugawana

kasungura. Lazima tuangalie suala la ukusanyaji nalo lipate wakati wake tulijadili vizuri, maana huwezi kugawana wakati hujakusanya. *(Makofi)*

Sasa tunaongelea habari ya mwongozo utakaopelekea kupata mpango na mpango mahali popote unapanga kwa sababu rasilimali zako ni chache, kama rasilimali ni nyingi huna haja ya kupanga, unatumia tu. Kwa kuwa zako ni chache, lazima uwe na vipaumbele ili kuangalia unafanyaje katika chache hizi, ndiyo maana tuliwahi kuwa na msemo unasema kupanga ni kuchagua. Kwa hiyo, unapanga unachagua, ukiwa na rasilimali chache kama za kwetu hapa Tanzania, utapata tabu sana. Kila atakayesimama, atasema Mheshimiwa Waziri wa Fedha tuwe na vipaumbele vichache na kadhalika, maana uwezo ni mdogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa chuoni nikisoma *resource economics*, niliwahi kuuliza swali darasani, nalikumbuka leo na Profesa wetu aliuliza kwamba, ungekuwa ni Waziri wa Fedha wa nchi yako ungepangaje vipaumbele vya bajeti ya nchi yako? Lilitupa shida sana swali hilo. Ukienda vijijini, ukaenda kule Kongwa au mahali pengine, ukawauliza wananchi wa kawaida kwamba; jamani vipaumbele vyenu ni nini? Kama ni kule Kongwa watakwambia kwanza maji; pili, afya halafu tatu elimu. Kwa utaratibu huo huo, kwanza tupate maji halafu zahanati, halafu ile habari ya watoto kwenda shule itafuata baadaye, ndiyo itafuata barabara, haya yatakuwa mengine mengine kwa maana ya wananchi.

Kwa maana ya swali lile nililokuwa na-*refer* hapa la Profesa wangu, una *option* mbili tu; *option* ya kwanza kuna vitu vinavyoitwa huduma za uchumi upande mmoja, upande wa pili kuna kitu kinaitwa huduma za jamii. Kwa sehemu kubwa, utakachochagua ni kati ya maeneo hayo mawili, unatanguliza nini, huduma za uchumi au huduma za jamii. Huduma za jamii ndiyo hii maji, elimu na afya. Sasa kwa Mbunge yeyote kwa maana ya kazi yetu ya Ubunge, lazima uwe unaelewa wananchi wanataka nini. Wanachokitaka wananchi ndicho na wewe unapaswa ukitake. Mtu mmoja aliwahi kuuliza akasema hivi unapokuwa kiongozi unafanyaje, unawaongoza watu wako yale unayotaka wewe au unawaongoza watu wako kwa kujiunga nao kwa yale wanayotaka wao.

Sasa kama unataka yale wanayotaka wao, utatanguliza huduma za jamii, maji, afya na elimu. Maji kwanza, lakini ukweli ni kwamba, kwa nchi, maana hapa tunaongelea habari ya nchi sasa, ili nchi isonge mbele ni lazima katika mipango yako kipaumbele cha kwanza kiwe ni huduma za kiuchumi. Uchumi wako ukikua, wananchi wako watamudu zaidi kugharamia huduma zao za jamii, wataweza kuwalipia watoto wao huduma za afya, wataweza kuwalipia ada za shule na mambo mengine, huduma za jamii kama uchumi ni nzuri. Kwa hiyo jenga uchumi, uchumi *automatically* utakuza hizi huduma za jamii. Kwa maana ya bandari, ninaposema huduma za kiuchumi, reli, barabara, viwanda, kilimo, uvuvi, mifugo, utalii na kadhalika.

Lazima uanze na huduma za kiuchumi, lakini haimaanishi kwamba hizi huduma za kijamii ziwe mbali sana na hapo, kwa nchi iliyochelewa kama ya kwetu katika hatua za kimaendeleo. Lazima ifuate hapo kwa karibu.

Mwaka jana kipaumbele kilikuwa elimu. Mwaka huu tumesema Kilimo Kwanza. Sina tatizo, maana ndiyo zile huduma za kiuchumi, lakini kwenye kilimo hebu tuchukue makabrasha ya kila Halmashauri ya Wilaya nchi hii tuangalie mipango ya kilimo ya mwaka huu fedha zilielekezwa wapi; ni fedha kiasi gani zimeelekezwa zinazomfikia mwananchi ili kuboresha kilimo chake? Bajeti nyingi katika Wilaya nyingi zifanana. Mwaka huu wamenunua pikipiki nyingi sawa, utasema inamuwezesha *Extension Officer* afike kijijini, lakini kwanza hawa *Extension Officers* walio wengi wako ndani ya Kata moja ile ile.

Vijiji vyetu vilivyo vingi viko karibu karibu tu. Hata kama angepewa baiskeli au tukanunua pikipiki kiasi, mwakani kiasi na mwaka keshokutwa kiasi, bado tungefika tu. Kongwa peke yake karibu pikipiki 40, kilomita za mraba 4,000. Kompyuta kibao, sijui kwa nchi nzima tumenunua ngapi? Magari, hela za mashamba darasa, kila mahala shamba darasa. Hoja yangu ni kwamba, kilimo sawa lakini bado kabisa. Hebu tujielekeze kuweka fedha mwananchi ng'ombe bora, yeye mwenyewe amkamate ng'ombe huyo. Tumpe mbuzi bora, tumpe jogoo wa kisasa arekebishe hali pale, tumpe jembe la plau moja kwa moja, tujitahidi bajeti ya kilimo iwe inalenga wananchi moja kwa moja *plus* fedha nyingine kutoka vyombo vingine vitakavyosaidiana. *(Makofi)*

Tukiendelea hivi tutakuwa na bajeti kubwa ya kilimo, lakini ukifanya tathmini hutaona kama kilimo chako kimesogea sana. Kwenye eneo la huduma za jamii kama nilivyosema, halipaswi kukaa mbali sana na kwenye eneo hili; tatizo siyo mipango, tatizo ni utekelezaji. Nimefikiri sana kabla sijalizungumzia eneo hili, nimepata tabu sana nilizungumzieje, nikaamua nichague mkoa mmoja kama mfano, kwa watani zangu najua hawatakasirika, wakikasirisa shauri yao kwa sababu mimi ni baba yao. *(Kicheko)*

Nimechagua Mkoa wa Shinyanga. Mkoa wa Shinyanga ni mmoja ya mikoa ambayo ni *highly populated Tanzania*. Mikoa yenye watu wengi sana na ongezeko la idadi ya watu ni kubwa, ukienda Kahama, Bukombe, Shinyanga Vijijini, Meatu, Maswa au Bariadi, kote ongezeko la watu ni kubwa. Mkoa huu ni moja ya mikoa mizito katika nchi. Kwa hiyo, mkoa kama ule kama hali yake ya kiuchumi ikitetereka, lazima nchi nzima inatikisika. Kwa hiyo ni moja ya mikoa muhimu. Natoa mfano tu kama mkoa; Mkoa wa Shinyanga ni wa mwisho katika matokeo ya darasa la saba; kwa miaka miwili au mitatu mfululizo mkoa huu ambao ni wenye watu wengi sana na si wote wamefika darasa la saba, walio-*drop out* ni wengi na hao waliofika darasa la saba huu ndiyo mkoa wa mwisho.

Sasa lazima ujiulize kwa nini jambo hili na kama hali ni mbaya namna hiyo; unategemeaje mauaji ya albino yapungue katika maeneo kama Shinyanga? Unategemeaje mauaji ya vikongwe na haki za akinama tunazozungumza hapa kwamba zitaweza kuchukua nafasi katika maeneo ambayo hatujafikisha elimu mahali pake inavyotakiwa? Mkoa kama wa Shinyanga usipo-*perform* unategemea nini na inapotokea kukosekana kwa maendeleo muhimu kama ya elimu namna hiyo kwa miaka mfululizo Mkoa haujafanya vizuri? Mimi najiuliza ni hatua gani zimechukuliwa na Serikali? Ni

mambo gani ya makusudi ambayo tumefanya kuhakikisha kwamba, tunausaidia mkoa huu. *(Makofi)*

Ndiyo pale ninaposema, wakati mwingine tatizo siyo mipango, tatizo ni utekelezaji. Maamuzi mazito lazima tuyachukue wote. Lazima kila mmoja awajibike mahali pake; Mkuu wa Mkoa mahali pake, DC mahali pake, Wakurugenzi mahali pao na Wataalam mahali pao. Hivyo hivyo, Mtendaji wa Kijiji mahali pake. Tukiwajibishana nchi hii, kwa bajeti hii ndogo tunaweza tukapiga hatua. *(Makofi)*

Tunaona kabisa mahali fulani hapaendi, wanisamehe sana watani zangu nimewatolewa mfano, lakini ipo mifano mingi nisingeweza kuitaja mahali pengine; nia yangu ni njema kusema kwamba, pamoja na mipango yetu na kadhalika, lakini mwisho wa siku pale mahali ambapo watu hawa-*perform* tuwajibishane.

Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Job Ndugai, kwa mchango wako. Waheshimiwa Wabunge, nilisema sasa nitamwita Mheshimiwa Elietta Switi na Mheshimiwa Dkt. Juma Ngasongwa ajiandae.

MHE. ELIETTA N. SWITI: Ahsante sana Mwenyekiti kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa, nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali yetu kwa kwenda kwa mtindo wa bajeti ya jinsia. Bajeti ambayo inashirikisha wananchi wote kutoka chini kwenye Halmashauri zetu kwa kuweka vipaumbele, japokuwa wapo Wabunge ambao wanafanya *rubber stamping* kwenye bajeti zetu. Lakini pia tunashiriki kama hivi ambavyo leo tunafanya; jinsi gani tunaweza kufanya mipango yetu ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niwashirikishe kidogo juu ya jinsi gani Finland wanafanya mipango na bajeti zao. Nchi ya Finland, Bunge linaketi kufanya mipango, lakini wanapoanza kukusanya fedha kwenye Halmashauri zao wao wanaita Majimbo, wanakusanya zile fedha na kufanya bajeti zao ndani ya Majimbo yao. Fedha wanazokusanya kutoka kwa wafanyakazi asilimia 30 zinakwenda Serikali Kuu. Wanapoanza kufanya bajeti zao katika Halmashauri, Serikali inarudisha *percent 30* ya zile fedha walizopeleka Serikali Kuu, kama zile fedha hazijatosha wanaruhusiwa sasa kuandika na kuomba *percent 50* ya ile fedha iliyobaki Halmashauri Kuu baada ya kuwa wamepewa *percent 30*.

Labda niulize ni kwa nini sisi hatuendelei? Sisi hatuendelei kwa sababu tunapoweka vipaumbele katika utekelezaji wake tunakwenda tunasuasua. Kama tunaona mambo yanakwenda vibaya, tunageuza na wakati mwingine hatutekelezi kabisa. Ninaomba tena hapa niwashirikishe uzoefu wa China. Wachina walikuwa maskini kama sisi, lakini leo wanaogopwa na ulimwengu mzima kwa kuwa maendeleo yao yamekwenda juu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wachina walipoona wafanyeje, wakaona waweke vipaumbele vitatu tu; waliweka vipaumbele katika elimu na leo ukienda China, kwa

kweli niseme karibu kila mtu ameelimika vizuri sana. Kipaumbele kingine walichoweka ni miundombinu, kwa hiyo, ukienda leo China utakuta miundombinu yao mizuri; barabara na miundombinu mingine yote, pamoja na umwagiliaji. Waliweka kipaumbele katika masuala ya mazingira, kilimo, umwagiliaji, miti na kadhalika ili wanapoanzisha viwanda vyao waweze kudhibiti tabia ya mabadiliko ya hali ya tabia ya nchi. Sasa je, sisi tufanyeje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri vipaumbele vilivyowekwa hapa kwetu leo sio vingi sana, kwa sababu ni karibu vinaendana tu na vile ambavyo nimevitaja katika Nchi ya China. Lakini sasa tufanyeje? Kama nilivyosema, utekelezaji ndiyo tatizo. Tukiangalia katika elimu kwa mfano, tunasema wanafunzi wameandikishwa, lakini hatuhakikishi kwamba wanafunzi hawa wote wamemaliza vizuri na elimu ile ambayo tunaihitaji. Tunasema tufanye vipaumbele katika miundombinu, lakini unaona barabara nyingi tunategemea sana fedha za nje. Kwa hiyo, tunakwama. Hivi leo sisi kwetu Rukwa bado tunafikiri sijui hawa Wamarekani wataleta ile pesa ya kutengenezea Barabara ya Tunduma – Sumbawanga, hatuna uhakika ila tunaamini kwamba watatuletea fedha hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalopaswa kufanya ni kuhakikisha kwamba, bandari zetu ambazo wakati mwingi hazitumiki vizuri, sasa zinaimarishwa na kutumika vizuri zaidi. Migodi yetu ambayo inawanufaisha wageni, iwe ni migodi ambayo inachangia kabisa kwenye uchumi wa taifa letu. Viwanja vyetu vya ndege ambavyo vingi ndege kubwa kubwa hazifiki, tuweze kutafuta fedha tupanue viwanja vyetu ili ziweze kufika na sisi tuweze kupata fedha ya kutosha kuweka katika vile vipaumbele tulivyoviandaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningependa kukubaliana kabisa na vipaumbele vyetu, lakini pia nikubaliane na kwamba, watu wanaotekeleza miradi hii au vipaumbele hivi, wawe ni wale ambao wako *committed.* Wengi wa wananchi wetu siyo *committed*, wanafanya tu ilimradi kumekucha kumekuchwa. Kwa hiyo, ningeomba Watanzania tulio wengi tuwe *committed* katika kutekeleza miradi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia huduma za jamii, saa nyingine inasikitisha; ukienda kwenye Hospitali zetu zinakosa mambo mengi ambayo jamii ingeweza kuyafurahia na jamii ambayo ina afya itatekeleza mambo vizuri zaidi. Kwa hiyo, kama tukiweza kutafuta fedha na ni lazima tuzitafute wenyewe, tusitegemee sana zile tunazoletewa na wahisani ili watu wetu wawe na afya bora, waweze kufanya kazi kama vile ambavyo wengine wanafanya kazi na sisi tuweze kupata maendeleo ya kutosha. Umaskini tulionao tunaweza kuuondosha kabisa kwa kushirikiana kufanya kazi kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninasema ahsante kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

MHE. DKT. JUMA A. NGASONGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia katika hoja hii ya Waziri wa Fedha na Uchumi, kuhusu Mwongozo wa utayarishaji wa Mpango na Bajeti katika mwaka wa 2010/2011 hadi 2012/2013.

Kwanza, naomba nimpongeze ndugu yangu Mheshimiwa Mkullo, Manaibu wake na Viongozi wenzake katika Wizara, kwa kazi nzuri waliyoifanya. Vile vile naomba nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi au Mipango, kwa kazi nzuri waliyoifanya. Kabla sijachangia hoja nyingine, nilitaka nianze na hili la Kanuni ambalo wamelichokoza wao kwenye kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninadhani Kanuni ya 94 katika Kanuni zetu za Bunge, Toleo la Mwaka 2007 la kutoa mamlaka na uwezo kwa Bunge kukaa kama Kamati ya Mipango, ina historia yake na kwa hiyo basi ni jambo muhimu. Historia yake imeanza mbali kidogo; imeanzia pale tulipoamua kuunda *Planning Commission* mwaka 1989. Wakati ule *Planning Commission* Mwenyekiti wake alikuwa ni Rais na Makamu wake alikuwa Waziri wa Mipango na Waziri wa Fedha alikuwa Mjumbe pamoja na Wajumbe wengine watatu ambao walikuwa *Commissioners.*

Kwa hiyo, baada ya kuingia kwenye mfumo huu wa vyama vingi, kulikuwa na fikra kwamba, kupanga ndiyo kumekwisha kwa sababu uchumi wa soko hakuna kupanga. Tuna uzoefu mkubwa na baadhi ya Wabunge wametaja hapa China; mimi naweza kutaja Korea ya Kusini, Malaysia, Singapore, Thailand, hizi zote zina *Planning Commissions* au *Planning Mechanisms very strong.* Kwa sababu kama tulivyosema hapa kwamba, mahitaji yetu ni mengi na hatuwezi kuyatekeleza kwa wakati mmoja; ni lazima tuchague kama Mwalimu Nyerere alivyotufundisha mwaka 1968 kwamba, kupanga ni kuchagua na uchague uende mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni lazima turudie ule utaratibu wa sisi kama Bunge kukaa kama Kamati, kutazama mipango kwa ujumla wake. Kwa sasa tuendelee kujadili tu mwongozo wa matayarisho ya mpango. Nadhani mwaka kesho au miaka inayokuja, turudie kule na mimi ninaendelea kupendekeza namna ya kupanga kwa muda mfupi, kwa mwaka mmoja, maana hapa *focus* ni mwaka mmoja au mitatu na ile mingine mitatu unaweka *indicators,* lakini *actually* huweki bajeti sawasawa. Kwa hiyo, nafikiri kurudia utaratibu wa miaka mitano ni mzuri zaidi na hapo vipaumbele vyetu vinaweza kuwa na maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Mheshimiwa Kigoda amezungumzia juu ya *consistency* na *persistancy* ya mipango na vipaumbele. Huwezi kuwa na *consistency*, wengine wanazungumzia juu ya nidhamu ya mpango, maana yake ni ile ile tu; huwezi kuzungumzia vipaumbele vyako kama unavibadilisha kila baada ya miaka miwili au mitatu. Kwa mfano, hili la elimu, watu waliopiga maendeleo katika zile nchi wanazoziita *Tiger Economies*, kipaumbele chao namba moja ilikuwa ni elimu na walibaki hapo kwa miaka 15 mpaka 20. Huwezi kubadilisha elimu, kwa sababu kwa mfano, mwaka jana nadhani bajeti ya elimu ilikuwa trilioni moja na nukta tano au sita. Sasa leo ukiweka kipaumbele cha tatu unafanyaje; unateremsha bajeti? Ukiteremsha bajeti utaleta *chaos* kubwa haijapata kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa maoni yangu ni lazima kipaumbele cha elimu kitaendelea kwa muda fulani, miaka mitano au miaka 10, kwa sababu elimu ni

muhimu. Haya mambo yote tunapata matatizo ya afya kwa sababu watu wetu hawana elimu. Mambo ya kilimo, ndugu yangu Wassira leo simwoni pale, anapendelea sana *extension services;* siku zote huwa tunapisha naye, mimi napenda zaidi kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati, uwekeze kwa wakulima.

Mtu mmoja hapa kasema umpe ng'ombe mkulima, hapo ni sawasawa, mpe zana ya kazi mkulima na nyingine ni bei. Sisi unajua tunawaonea sana wakulima; ni lazima katika mpango wetu tuwe na hakika kwamba, mkulima huyu tunampa motisha gani? Ni *incentive* gani ili aendelee kuzalisha mpunga au pamba? Ni sehemu ya mpango na unapofanya ruzuku yako, unaweka kwa kuzingatia kwamba, nikimpa ruzuku hii, mkulima huyu ataendelea ku-*persist* kulima mpunga ama kulima pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja nikupe mfano mdogo wa Jimboni kwangu kule Ulanga Magharibi. Sisi tulikuwa tunalima sana pamba, lakini wale jamaa wa ushirika wakatufanyia uhuni kwa miaka mitano hawatulipi pesa wanatukopa tu, tukasema hatuwezi kulima tena pamba tutalima mpunga. Sasa katika Jimbo langu la Ulanga mpunga siyo tatizo ni mwingi sana na tunauuza sana. Barabara yangu ina matatizo kwa sababu malori kutwa yanavuka pale kivukoni siyo chini ya 30 kwenda kuchukua mpunga. Mpaka hkuna mwingine sijauuza kwa sababu nangoja bei iwe nzuri. Sasa Serikali itazame namna ya kumuwezesha mkulima huyu kwa kupitia bei ambayo ni *direct investment to the farmer* ili aongeze uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vipaumbele, nitakapokuja kuzungumza kwenye umwagiliaji nitalisema vizuri. Ninasema ni lazima turudie utaratibu wa kupanga kwa maana ya kutazama muda mrefu zaidi; miaka mitano miaka 10, miaka 15; na mipango yote hii, MKUKUTA ni wa miaka mitano, Ilani ya CCM ni ya miaka mitano, tena Ilani hii msingi wake ni mwelekeo wa miaka 10. Huu sasa ni mwisho wa kipindi cha pili cha mwelekeo na ninatumaini Chama chetu kitaanza tena kuandika mwelekeo mwingine wa miaka 10 au 15; unapopanga ni lazima upange kwa *perspective* ya muda mrefu, huwezi kupanga *annually.* Ndio maana tunachanganya sana mambo ya bajeti na kupanga; kupanga unaweka bajeti kwenye mpango, lakini ni tofauti na bajeti ya kila mwaka kwa sababu pale unaweka *precise budget,* kule kwenye mpango unaweka *figures, indicative figures.*

Allah! Kumbe rafiki yangu Wassira yupo; unaweka *indicative figures,* ni lazima hiyo. Kwa hiyo, hilo ni lazima tukubaliane kwamba, tupange kwa kuzingatia muda na kwa namna hiyo tunaweza kurudia utaratibu wa zamani wa kupanga, badala ya kupanga huu wa muda mfupi wa *cash budget.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua *pressure* tuliyokuwanayo ya wahisani wetu, lakini inatuondoa maana hata kwa mfano kwenye hili jedwali namba moja pale, umeonesha Pato la Taifa; mwaka 2004 tumepanda mpaka 7.8, tumefika mwaka 2006 pale tulikuwa tunafikiria kama tunaweza kufika hata *point* nane au tisa, lakini sasa tunarudi tena nyuma tumekwenda *point* tano mwaka jana 2009, sasa tunaanza upya 6.4; sijui mmesema *point one* pale. Sasa tunaanza upya tulikotoka zamani. Hili tatizo siyo la kupanga peke yake, ni tatizo la *perspective* yetu ya kupanga; ni muhimu kulitazama hili

vizuri. Pamoja na kuwa tuna Mfuko wa Uchumi, lakini mpango ni lazima uangalie na mpango una mambo mengine mawili makubwa; moja ni la kufuatilia *(monitoring)* na la pili ni *evaluation* wapi tume-*miss the target* na kwa nini. Kujiuliza namna hiyo ndio kunasaidia kuimarisha upangaji. Wengine wanasema nidhamu ya kupanga, *basically*, ni hiyo ya kuona kwamba, siku zote *you are not off track* na kama unakuwa *off track*, unarudi kwenye *track* na hiyo sifa yake kubwa ni ya *monitoring.* Sasa hili nalo linataka kazi nzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kutilia mkazo suala la kupanga, sasa ngoja nirudi kwenye vipaumbele ambavyo niligusia kidogo hapa. Mimi ninadhani kipaumbele cha kilimo ni safi, lakini siamini kama tutakapokuja kwenye *budgeting* itakuwa namba moja kwa fedha. Hii ni kwa sababu huu ni mwaka wetu wa tatu au wa nne wa kuweka kipaumbele namba moja elimu na namba mbili tumeweka miundombinu.

Nimefurahi sana hapa Mheshimiwa Waziri amesema katika ukurasa wa 33 pale kwamba, sasa anafanya bidii kubwa zaidi ya maandalizi ya *Sovereign State Bond.* Hili ni jambo zuri, tumelicheleweshe sana, tulilizungumza miaka ya 2006/2007, lakini mpaka leo hatujatekeleza. Sasa mlitekeleze kwa sababu hili ndilo litatuondolea tatizo la rasilimali kuwekeza katika miundombinu. Hapa ndipo unapoweza kuwekeza katika miundombinu kwa kutumia chanzo hiki. Barabara zetu ni muhimu kuzitengeneza. Unajua masharti ya maendeleo ya uchumi yapo mawili; moja ni kuwa na *National State.* Utaifa ni muhimu. La pili ni kuwa na *National Market* na hii huwezi kupata katika mazingira ambayo hayana barabara; unafanyaje *National Market?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, una mahindi mengi pale Rukwa, lakini huwezi kuyapeleka Shinyanga. Una mahindi mengi pale Mahenge, una mpunga pale Ulanga Magharibi, huwezi kupeleka Songea ambako wanataka mpunga, huwezi kupeleka Kigoma kwa sababu huna barabara. Kuna juhudi pale za kutengeneza barabara kwenda songea, lakini juhudi ile haiwezi kukamilika mapema kama tunavyotaka. Kwa hiyo, ni lazima suala la miundombinu *to open the country* ni muhimu sana, yaani kuifungua nchi ni lazima.

Kwa hiyo, njia pekee ni hii. Sasa sina hakika kama vipaumbele hivi vya mwaka huu vitaweza kutekelezeka kwenye pesa, vitangoja hapo pesa zitakapopangwa. Mimi ninaona kipaumbele cha elimu ni lazima kiendelee, cha miundombinu kiendelee, lakini kitaondolewa tu tukipata fedha za kutosha kutoka kwenye ile *sovereign bond* na kilimo; *of course*, ni lazima kiwe cha tatu au cha pili, kwa sababu kilimo ndio uti wa mgongo lakini kwa tafsiri ya ku-*invest* katika *irrigation. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale Wahindi walikuwa na njaa sana, lakini wameondokana na njaa kutokana na *Green Revolution* ambayo *key element* pale ni *irrigation.* Cha pili ni matumizi ya mbegu bora na tatu ni matumizi ya mbolea. Kwa hiyo, vitu hivi vitatu tukiviunganisha katika kilimo, unaweza kuleta *impact* unayoitaka. Vilevile hatuwezi kuendelea kulima kwa kutegemea jembe la mkono, tunahitaji zana bora za kilimo. Kwa hiyo, hilo nalo ni muhimu kulitazama. Mimi nimefurahi sana, kwa mara ya kwanza tumeleta viwanda, katika miaka mitatu hii minne hatujaweka viwanda vizuri;

sasa leo nimeona kwenye vipaumbele na viwanda vipo. Viwanda ni muhimu sana hasa vile vya kujenga uchumi vya Liganga na Mchuchuma tuvitilie mkazo na tuvihudumie sisi wenyewe kwani sekta binafsi haiwezi. Hili ninaliunganisha na ile *IPP;* tukiweza kufanya hivyo tunaweza sasa kufungua uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kuna hoja hapa imezungumzwa ya *drivers of the economy*, yaani vichocheo vya uchumi; mimi ninasema kuna sekta zinachochea uchumi, moja ni ya madini, hakuna kuidharau hii. Pili ni ya nishati. Hizi ndio zinachochea uchumi kwa nguvu zaidi kwa upande wa miundombinu na upande wa uzalishaji. Mawasiliano ya kisasa, TEKNOHAMA, huwezi kupuuza vitu hivi. Kwa hiyo, katika kupanga kwetu ni lazima tuseme ni vitu vipi vinachochea uchumi. Tukijibu jibu hilo, ndio sasa tunaweza kupanga vipaumbele; bila hivyo sioni kama tunapanga vipaumbele *realistic.*

Kila siku tukija hapa tutakuta Pato la Taifa ama linateremka au limeng'ang'ania hapo hapo, kwa sababu hatujapanga vipaumbele vyetu kwa usahihi, kwa sababu vipaumbele shabaha yake vituondoe hapa tulipo ili twende mbele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia mpango wa bajeti katika taifa letu. Kwanza, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kutimiza ahadi yake ya ujenzi wa daraja la Mto Simiyu; sisi Wanakisesa tumefurahi sana na mpaka sasa hivi tuna raha tu utadhani amefungua jana kumbe karibu wiki mbili zilizopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanza mapambano toka tulipotangaza uhuru wetu mwaka 1961, tukatangaza maadui watatu ambao ni ujinga, maradhi na umaskini. Tokea hapo tukaelekeza bajeti yetu kupambana na hao maadui watatu. Tumepambana vizuri sana katika harakati ya kufuta ujinga, mafanikio makubwa shule za msingi nyingi zimejengwa, sekondari zimejengwa, vyuo vikuu vimejengwa, tumefanya vizuri katika malazi, kuondosha maradhi nako tumefanya vizuri, lakini tatizo kubwa ni kwamba, huyu adui mwingine wa tatu (umaskini), sasa ametung'ang'ania na jitihada za kuondokana naye inaonekana kwamba tumeshindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo ushahidi; *statistical evidence* inaonesha kuwa, sisi tumeshindwa kupambana na huu umaskini. Kupitia katika Mpango wa Milenia *(MDG)* na sisi tukautafsiri katika MKUKUTA, tulijiwekea malengo kwamba, kuanzia mwaka 1990 hadi mwaka 2015, umaskini utakuwa umeshuka kwa 15% kutoka 39% mpaka 19.5%. Hivi sasa mafanikio yetu yalivyo, umaskini umeshuka kutoka 39% hadi 33.64%. Kwa hiyo, ni 5.36% tu ndizo tumeweza kuushusha huu umaskini kwa maana kwamba, kwa muda wa miaka 18 tunaushusha umaskini kwa 5.36%. Huu ni ushahidi kwamba hii vita imetuelemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unajiuliza tatizo ni nini? Kama nilivyosema kwamba, kutoka bajeti ya mwaka 1961, kila bajeti yetu tunaifanya vizuri inapita hapa Bungeni, tunaipitisha tena kidemokrasia na Serikali ikisema kwamba, bajeti hii ni kwa ajili ya umaskini. Sasa umaskini ni 5.36% kwa miaka yote hiyo 18, pamoja na mipango yetu mingi sana tunayoipanga.

Lingine sasa ambalo linachanganya zaidi ni kwamba, mapato yetu yameongezeka sana kutoka 2005/2006 mapato yetu ya ndani yalikuwa bilioni 177 kwa mwezi. Ilipofikia mwaka 2008/2009, mapato yetu yamepanda yamefikia bilioni 357.7 kwa mwezi. Mapato yamepanda, lakini bado jitihada za kupambana na umaskini zimeshindikana; sasa tunajiuliza tatizo ni nini?

Tunakosea wapi? Tujiulize kwamba; je, vipaumbele ambavyo tunavipanga *source* yake ni nini au ni utashi wa mtu tu akiamua leo kwamba vipaumbele viwe hivi vinakuwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia swali la pili tujiulize; hizi rasilimali za nchi tunazigawa kwa uwiano ulio sawa au kuna baadhi tu ya maeneo yamependelewa? Swali la tatu tujiulize; hivi kuna utafiti gani wa hivi karibuni uliofanyika ambao unathibitisha kuwa 80% ya Watanzania ni wakulima au tulishakariri tu hivyo kwamba 80% ya Watanzania ni wakulima? Wakati idadi kubwa ya Watanzania hawana ajira yoyote?

Yapo maswali mengi ya kujiuliza, kwa sababu ya muda tuache kujiuliza maswali, twende kwenye matatizo yenyewe ambayo yanasema sasa tufikirie tufanye nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza ukafanya vizuri sana, kwa mfano, kama sasa hivi mipango ya Serikali ni mizuri sana. Serikali imejitolea vizuri sana, imewezesha pembejeo, wananchi wetu wamefurahi sana. Imechangia katika ile gharama ya pembejeo 50%, mwananchi anatoa 50% na Serikali inatoa 50%.

Bado tutaendelea kupeleka mbolea, tutaendelea kupeleka matrekta na sasa hivi ninaipongeza Serikali ni mpango mzuri sana wa kuwawezesha hawa wakulima wetu waweze kwenda kwa kasi. Ukichukua plau, ukachukua trekta, uchumi utakua na wakulima wetu watakua, lakini tatizo kubwa ni kwamba, hata kama utamuwezesha huyu mkulima awe na matrekta, awe na pembejeo, kama bei ya mazao anayoyaouza hairidhishi, hakuna atakayekwenda kulima.

Kwa hiyo, tujiulize sasa katika hiki Kilimo Kwanza tunamuwezeshaje mkulima huyu kupata bei nzuri ya mazao? Mazao yetu mengi tunayauza yakiwa malighafi, tujiulize sasa viwanda vitakavyotutengenezea nguo hapa viko wapi ili pamba inayozalishwa Shinyanga na Meatu sasa tupate suti tunazozivaa tuvae za Tanzania.

Haya yanawezekana, tungekuwa na mipango madhubuti ya kuwawezesha hawa wakulima toka mwaka wa 1961 mpaka leo tungekuwa na viwanda hivyo vikubwa inawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuwa na soko huria lakini unaweka vigezo kama hivyo, mara unasema mkulima haruhusiwi kusafirisha chakula nje ya nchi, hizo ni sheria za kibepari. Kwa sababu unapomzuwia mwananchi huyu kusafirisha chakula chake nje ya nchi au kuuza kwa bei nzuri, unamnyima haki yake ya msingi katika soko huria.

Mpaka sasa hivi tunavyozungumza, wananchi wetu wanasafirisha ng'ombe kutoka Mwanza na Shinyanga kupeleka kutafuta soko Arusha na Dar-es-Salaam kwa gharama kubwa, wanatembea kwa mguu kutafuta soko. Serikali weka viwanda vile, *resources* zipo, kazi yako wewe ni kuweka viwanda tu, rasilimali ipo. Weka machinjio ya kisasa pale Shinyanga, weka machinjio mazuri wakulima wale wapate bei nzuri ya rasilimali zao karibu na walipo wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafanya kazi nzuri, mimi nimepongeza mipango ile nimesema Benki ya *TIB* sasa lile dirisha la wakulima, mikopo ya wakulima, iko vizuri na hela zipo. Ninachotaka kukizungumza; je, hawa wananchi tumewaandaa kupata ile mikopo?

Wananchi wa Kongwa na wa Shinyanga Vijijini wanazo sifa za kwenda kukopa hizo fedha?

Tulikuwa na mpango mzuri sana ule wa urasilimishaji mali ule MKURABITA, tukasema wananchi wote waweze kurasimishiwa mali zao hasa maeneo yao viwanja vyao, kwa maana ya kupata hati ya kimila. Lakini zoezi hilo linaenda taratibu mno, pale kwangu Meatu, mpaka sasa hivi hakuna mwananchi hata mmoja ambaye amepata hiyo hati ya kimila. Sasa kuna hizo sh. 714,000 ambazo Serikali inataka kila kijiji kichangie. Tumeweka kilimo kwanza, tuwawezeshe hawa wakulima wakope fedha, fedha hizi Serikali itoe tu yenyewe ivilipie vijiji ili kila kijiji kiwe na hivyo vifaa kwa ajili ya kutolea hati miliki ya kimila, tutakuwa tumetatua kabisa hilo tatizo na kila mwananchi atapata ile hati ya kimila na atapata nafasi ya kwenda kukopa benki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ninalotaka kulizungumza ni suala la usafiri vijijini, kwamba mpaka sasa hivi tunapozungumza kuna vijiji ambavyo havina barabara, yaani toka uhuru hawajawahi kuona greda. Nashauri sana tuamue hatuwezi kuwatoa hawa katika umaskini kama bado wako katika hali ya maisha duni kiasi kile. Kule kwangu mimi kuna vijiji vingi tu ambavyo ni vingi sana ambavyo haviko kwenye mtandao wa barabara, hebu tutenge fedha za kutosha safari hii ili kwamba iwe historia Tanzania kijiji kuwa na barabara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa matumizi ya fedha za umma, kama alivyoongea ndugu yangu Mheshimiwa Serukamba kwamba, kwa kweli tunalia na umaskini tu lakini Taifa hili lina matatizo makubwa sana ya kutokutumia rasilimali za umma ipasavyo. Tuliona kwenye bajeti iliyopita Wizara moja safari tu na semina ni shilingi bilioni mia nne wakati Watanzania wengine wanakufa bila matibabu. Lakini tunaweza tukajityuni tu ndani ya bajeti yetu hii tukaweza kumsaidia Mtanzania kwa kiwango kikubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo nchi ambazo ziliweza kupiga hatua kubwa katika suala zima la kupambana na umaskini hapa hapa Afrika. Wenzetu Ghana wao walijipanga wakasema katika mpango wao kwamba, wataushusha umaskini kutoka mwaka 1991 mpaka mwaka 2015, umaskini utatoka asilimia 51.7 mpaka asilimia 25.85. Kufikia mwaka 2006 wa Ghana walikuwa wameshaushusha umaskini kutoka asilimia 51.7 mpaka 28.5, kwa hiyo ilikuwa imebaki kama asilimia 2 *something* kufikia malengo. Kwa hiyo tukijipanga vizuri tunaweza, tukijipanga vizuri kumtizama huyu maskini tunayempangia bajeti kila siku tunaweza na huu umaskini hapa nchini kwetu utakwisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua muda wangu umekwisha. Baada ya kusema hayo nakushukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru. Muda wako ulikuwa bado lakini umeutumia vizuri, ungesubiri kengele muda ungekuwa umekwisha. Waheshimiwa Wabunge basi kwa kuwa Mheshimiwa Mpina amemaliza basi nimwombe Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga ajiandae halafu nimwite Mheshimiwa Magdalena Sakaya na Mheshimiwa Ahmed Ally Salum ajiandae.

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuweza kutoa mawazo yangu katika suala zima la mwongozo wa mpango wa bajeti katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Afrika ni bara ambalo linakabiliwa na changamoto nyingi sana kwa sababu ni bara maskini. Changamoto hizi zimekuwa zikisababisha matatizo na ongezeko la changamoto nyingine katika bara hili na hususan katika nchi zenyewe ambazo ziko katika bara hili la Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Dunia imekuwa ikielezea kwa ufupi kwamba, katika Bara la Afrika kuna changamoto za aina tatu. Changamoto ya kwanza ni historia, historia ambayo imepelekea nchi nyingi za kiafrika kutokuwa na elimu yenye tija kutokana na *background* yetu kutawaliwa na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya pili ambayo imekuwa ikielezwa ni kiwango cha ongezeko la watu ambacho hakiendani na ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ya mwisho ni suala zima la matatizo yanayosababisha umri wa watu kupungua *life expectance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi ambayo na yenyewe ni moja kati ya nchi zilizo katika Bara la Afrika. Kwa hiyo, hatuna budi na sisi kukaa kujiuliza kwamba sisi kama Tanzania tunafanya nini na tunajikwamua vipi ili kuweza kuhakikisha kwamba umaskini wa watu wetu, licha ya changamoto zilizopo, unapungua kama sio kutokomea kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya *pillar* ya *vision* 2025 ni kuhakikisha kwamba nchi hizi za kiafrika na hususan nizungumzie kwa Tanzania ifikapo mwaka 2025 inakuwa ni moja kati ya nchi ambazo ni *middle class economy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni *target* ambayo imewekwa na wataalam, ni kitu ambacho ni kikubwa sana, sasa hivi ni mwaka wa kumi imebaki miaka kumi na tano. Tanzania kama Tanzania hatuna budi kuangalia tumefikia wapi na tuko wapi katika kuelekea kufikia haya malengo na hatima yetu ni nini hapo baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijiuliza katika haya machache, napata tabu sana kwa sababu, ambacho nakiona kwa mawazo yangu ni kwamba, nchi ya Tanzania baadhi ya maamuzi yanafanywa kisiasa zaidi kuliko kiuchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siasa ni uchumi na uchumi ni siasa, lakini hakuna kosa kubwa kama tutakuwa tunapeleka *political thinking* kwenye *economic challenges*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imekuwa ikisababisha baadhi ya vitu ambavyo vimekuwa vikiamuliwa kuonekana kwamba haviendani havina uhalisia na hali halisi ya maisha yetu. Sera ambayo zimekuwa zikiwekwa zipo lakini baadhi kunakuwa kuna makosa ya utendaji kutokana na kuingiza sana siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipoliangalia hili kwa kweli litatufikisha pabaya na kutokana na hivyo naomba sana viongozi kuanzia juu mpaka huku chini na pia sisi wenyewe, Wabunge tukiwemo tuangalie kwamba ili kuweza kuondoa huu maskini lazima tuweke pembeni siasa ili tuweze kushughulikia matatizo ya kiuchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili kuna uwezekano mkubwa likasababisha baadhi ya wataalam wetu wakashindwa kutimiza yale ambayo wanadhani kwamba yanaweza yakatusaidia kwa sababu ya sisi kuendelea kung’ang’ania kufanya maamuzi ya kisiasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaweza ikafika wakati tukajikuta kwamba tunakaa kwa sababu wachumi wao wataangalia *cost benefit*, sisi wanasiasa tunaangalia kura. Lakini hata kama tunaangalia kura tukiendelea na mwenendo huu itafika wakati sasa hata hizo kura zenyewe zitapungua kwa sababu wananchi wataona kwamba viongozi hawajali matatizo yao, wakati viongozi wao wanashindwa kufanya maamuzi magumu kwa sababu ya kuhofia kukosa kura. Kwa hiyo nadhani ni suala ambalo lazima sisi wanasiasa tuwe nalo makini sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala zima la rasilimali, Tanzania ni nchi ambayo imejaliwa rasilimali nyingi sana. Lakini rasilimali hizi endapo kama hazitatumiwa ipasavyo hata maana ya hizi rasilimali itapotea. Jiografia ya Tanzania inaonyesha Tanzania ina rasilimali kubwa kubwa sana, lakini kama ambavyo nimeelezea kuhusu masuala ya maamuzi ambayo yamekuwa yakifanywa hapa nchini, hatuna budi pia

kuweza kuangalia kwamba rasilimali hizi zinawezaje kumkomboa Mtanzania kutoka katika umaskini uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rasilimali ambazo zimekuwepo tumekuwa tukizungumzia masuala ya ardhi, tumekuwa tukizungumzia masuala ya madini na kadhalika. Lakini baadhi ya sera ambazo zimekuwa zikiwekwa sidhani kama zimekuwa zinaingia ndani sana kuangalia rasilimali hizi ambazo *effect* yake inaweza ikasababisha umaskini kwa Watanzania. Nitolee mfano, tunapozungumza kwamba hii ni nchi maskini, tuna matatizo ya rasilimali chache. Suala la rasilimali ndiyo kitu pekee kilichobaki kwa nchi maskini kama hii cha kuweza kutukomboa. Lakini hivi sasa kuna sera ambayo imekuwa ikizungumzia suala la kuwakaribisha wawekezaji ili kuweza ku-*invest* kwenye mashamba makubwa kwa ajili ya kusaidia kuinua uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia mchango wangu huu mdogo wa muda huu mchache naomba kwamba, Serikali katika hili iweze kuangalia kwa sababu tusipokuwa makini haitakuwa tofauti na madini, haitakuwa tofauti na mambo mengine ambapo itakuwa kwamba, mashamba yapo lakini licha ya mashamba kuwepo faida itakuwa inapelekwa nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, labda nipendekeze kwamba, katika rasilimali hizi, tuangalie wa kwanza kabisa wa kuweza kujaliwa katika hili awe ni Mtanzania mwenyewe. Kwa hiyo tunapozungumzia sera za kuhakikisha kwamba tunaiondoa nchi katika umaskini, tuangalie Mtanzania kwanza yeye atafaidika katika kiwango gani kabla ya kumfikiria mtu mwingine wa nje. Kwa sababu pia labda pengine tunaweza tukapata kikwazo kwamba nchi yetu ni maskini, labda hatuna watu ambao wana uwezo wa kuwekeza katika kiwango kikubwa kama hicho lakini tufikirie basi kama hivyo ndivyo angalau yale mambo yote ya msingi katika hizi rasilimali Mtanzania awe anapata asilimia kubwa zaidi katika huu uwekezaji halafu mgeni apate asilimia ndogo. Kwa mfano kama ikiwa 52 kwa 48 haitakuwa na tatizo lolote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumzia hili suala la rasilimali, tuna madini, tuna utalii, tuna kilimo, tunapozungumzia madini na utalii tunaambiwa uchumi unakua, lakini wananchi wetu wamekuwa wakijiuliza sana hivi uchumi mnatuambia unakua lakini mbona umaskini unaongezeka? Sasa tunakubali sote kwamba uchumi unakua lakini umaskini unaongezeka, hivi kweli sisi kama viongozi pamoja na wataalam, hivi vile vitu ambavyo vina *direct effect* kwenye kuhakikisha kwamba umaskini unaondoka tumevifanyia kazi katika kiwango gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kama tukizungumzia kwamba utalii unaongeza unaleta kipato kikubwa katika Taifa, tukizungumzia madini yana mchango mkubwa katika Taifa, lakini tukizungumzia kilimo tukisema kwamba hakuna mchango mkubwa na wakati hii ndio sehemu ambayo ina wananchi wengi sana na ni sehemu ambayo endapo kama itaguswa moja kwa moja itakuwa ina *direct effect* ya kuondoa umaskini kwa Watanzania, tutakuwa hatujafanya kitu. Wakati mwingine huwa nasema, hivi hawa wataalam au hawa watu ambao wamekuwa wakipanga, nikizungumzia hata mfano wa hii Tume ya Mipango, hivi kazi yake huwa ni nini? Maana wao kazi yao

wanatakiwa wakae watupangie kwamba hiki kinatakiwa kiende hivi, hapa lianze jambo moja liingie la pili, liingie la tatu na liingie la nne. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona kabisa kwamba kuna baadhi ya vitu vinafanyika *as if* hii Tume ya Mipango haipo, sasa labda watuambie matatizo yako kwa sisi viongozi ambao hatukubali kushauriwa au matatizo yapo kwao katika hili nililozungumzia kwamba utaalam unachanganywa na siasa. Sasa labda na hii nayo tuiangalie vizuri kwa sababu haiwezekani baadhi ya vitu ambavyo tunaviona kabisa kama vile masuala ya bandari, masuala ya reli, masuala yote muhimu kwamba tukifungua nchi yetu tunajua kwamba tunapata faida. Lakini unaona kabisa kwamba hakuna kitu kinafanyika yaani hakuna jitihada za makusudi zinazofanyika, unashindwa kuelewa. Kwa mfano hata hili suala la mkataba wa *Rites*, wakati mwingine nakaa najiuliza hivi kweli hawa watu wamekwenda shule? Hawa watu wasingekwenda shule naona ingekuwa hatari kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kifanyike, naomba *technical clerks* wawe na nguvu kuliko wanasiasa. Wataalam wetu tuwape nafasi zaidi kuliko sisi wanasiasa. Mambo ya kukaa kuangalia viongozi hata kama ni Rais, hata kama ni Waziri Mkuu sio mazuri, kama kitu hakiwezekani waweze kuwa na uwezo wa kusema hiki hakiwezekani. Maana unaweza ukawa unamwona mtu kwamba ni mkubwa sana basi anakuambia kitu ambacho hakiwezekani husemi lakini ukitoka nje ndio unasema kile kilikuwa hakiwezekani lakini kwa sababu bosi naye anakiona kinafaa tutafanyaje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu waache nidhamu za uwoga, wawe na nidhamu za kuweza kufanya kazi ili angalau kutuondoa sisi katika huu umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine katika nini kifanyike, nadhani ni muda muafaka sasa tuwe na *sartorial targets*, kama tunaona kwamba nchi yetu tunapata kipato kingi sana katika labda madini na utalii basi tuamue badala ya hizi pesa kuingizwa moja kwa moja kwenye ule Mfuko Mkuu tuwe tu na *target* ya kawaida kwamba sasa hivi kipaumbele chetu ni elimu au afya. Tuangalie katika sekta hii Waziri kama ni wa Afya awe anajua kwamba kila mwaka natakiwa nijenge zahanati kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu tumeshaona, mpango huu wa kusema kwamba, pesa zote zitakwenda kwenye Mfuko Mkuu *effect* yake haionekani moja kwa moja, tusifanye kazi kwa mazoea, hivi vitu vinawezekana kama tukifanya *sartorial target*. Kwenye *private sector* wanafanya, ni vitu ambavyo vinawezekana, lakini ukisema kwamba pesa zote zinakwenda huko matokeo yake ndio tunakuta *OC* kila siku pesa ya chai milioni 20, hizo chai sijui hata wanakunywa akina nani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu vipaumbele. Kwa ufupi, naomba tuwe na nidhamu katika vipaumbele ambavyo tunaviweka. La pili tuwe tunafanya tathmini na la mwisho tuwe na ufuatiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni moja kati ya vitu ambavyo vinatusumbua sana katika nchi hii. Tutakaa, tutapanga vizuri, maneno mazuri sana, hakuna nchi ambayo

watu wanajua kuandika kama hapa Tanzania lakini kwenye utekelezaji ni tatizo kubwa sana. Kama tutakuwa tunakaa, tunapanga vipaumbele vyetu, tunaviweka *in record*, tunasema ni elimu, afya, kilimo au kingine lakini kama tusipokuwa na uwezo wa kufanya tathmini na kufuatilia, mambo mengi sana yatakuwa yanakwenda bila mipango na hatimaye badala ya kupiga hatua mbele, tutakuwa tunarudi nyuma. Matokeo yake baadaye tutaanza kukaa na kulaumiana na kuanza kushangaa ni nini kimetokea, wakati ni vitu ambavyo vingeweza kufanyika na kusaidia nchi hii bila matatizo yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kingine naomba Wizara ya Fedha ijaribu kuangalia, hivi haiwezekani kwamba baadhi ya Halmashauri katika baadhi ya *sector* zikapewa vigezo ili Halmashauri hizi kuwa na uwezo wa kukopa kama ni humu ndani au ni nje katika utaratibu maalum. Nadhani nchi tunajua inakopa nje, inakopa katika maeneo mbalimbali lakini naomba Wizara ya Fedha ijaribu kuangalia mfumo mzuri wa kuweza kuangalia hizi baadhi ya Halmashauri kwa kulingana na vigezo muhimu vya kiuchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kidogo kwenye mwongozo huu wa bajeti kwa ajili ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu wake pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kuweza kuandaa huu mwongozo na kutuletea hapa Bungeni ili tuweze kuweka mapendekezo na mawazo yetu. Pia napongeza sana maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi, ni mazuri sana na yatasaidia sana Serikali kuweza kuboresha bajeti na pia napongeza maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, ametoa *input* nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia suala moja tu dogo, suala la kipaumbele. Tangia jana Mheshimiwa Waziri alipowasilisha kwa ufupi mwongozo huu nilikuwa najiuliza masuala makubwa yafuatayo; kwanza, nini vigezo hasa vinavyotumiwa na Serikali kwa ajili ya kupanga vipaumbele? Pili, tunapopanga vipaumbele nini madhumuni hasa? Kwa nini tunaamua sasa tupange kipaumbele fulani kiwe namba moja, mbili, tatu *then* mpaka mwisho? Mwisho, nikajiuliza tunapopanga vipaumbele tunategemea nini, tunataka tu-*achieve* nini mpaka tunapoamua kuwa na vipaumbele vyetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefikiria haya yote kwa sababu nimeona kwamba kwenye mwongozo tuliopewa sasa hivi tumeambiwa kwamba kipaumbele sasa hivi kitakuwa ni kilimo. Lakini nikajaribu kuangalia mwaka uliopita wa fedha kipaumbele kilikuwa ni elimu. Nikawa najiuliza sana kwa mapana na marefu tulikuwa na kipaumbele chetu cha elimu kwa mwaka 2009/2010, kwenye elimu tulilenga nini na tumefanikiwa vipi? Tume-*achieve* nini mpaka tuamue kubadili kipaumbele kile na sasa kuwa na hiki cha kilimo. Tunapoongea elimu ina maana elimu ndiyo *base*, ndio *foundation* ya kila kitu. Lakini mpaka hivi tunavyozungumza pamoja na kwamba mwaka jana kipaumbele

chetu kilikuwa ni elimu lakini bado tuna matatizo lukuki kwenye sekta hiyo ya elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania hatujaweza kusema kwamba angalau mwaka jana kipaumbele kilikuwa ni elimu tume-*achieve* kitu Fulani. Hatuwezi kusema kitu chochote kwenye elimu kwa sababu mpaka ninapozungumza sasa hivi tuna majengo ya madarasa yametapakaa nchi nzima lakini mengine hayajakamilika, tuna majengo yaliyokamilika kwa hali ambayo sio ya kuridhisha, yaani hayajakidhi vigezo lakini bado hayana madawati, hayana maktaba, hayana maabara, hakuna vifaa, shule hazina walimu, matatizo mengi mengi. Kwa hiyo, nikawa najiuliza sasa tumehama kule tumekwenda kwenye kilimo yale ambayo kwenye elimu bado hatujayakamilisha tunayapangia mipango gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tumeamua kwenda katika kipaumbele cha kilimo, lakini Tanzania tuna uhaba mwingi sana wa maafisa ugani, bila elimu wanapatikana wapi? Tuna upungufu mkubwa wa madaktari na wahudumu wa afya kwenye hospitali zetu. Akina mama wanakufa, kila leo watoto wanafariki, tuna matatizo katika sekta zote za elimu lakini bado tunakwenda katika kilimo. Kwa hiyo, nimekuwa najiuliza maswali mengi, Serikali inatumia utaratibu gani? Kwenye mpango wa sasa basi tungeambiwa kwamba tumeamua kwenda kwenye kilimo lakini kwenye elimu tumepanga utaratibu gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napata shida sana kujiuliza maswali hapo na naendelea kusema kwamba, bajeti iliyokuwa inapelekwa kwenye elimu *per se* ilikuwa ni kidogo. Kwa mfano, inayokwenda kwenye vyuo mbalimbali kama *CBE*, vyuo vya ufundi na vinginevyo ni kidogo. Kwa hiyo, ukiangalia kiasi kinachokwenda kwenye elimu kama elimu ni kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa nategemea angalau iongezwe, kwa sababu kuna matatizo sana, Watanzania tumeshuhudia badala ya kupiga hatua katika elimu tunarudi nyuma, ni karibu miaka mitatu sasa hivi tunarudi nyuma na Serikali inajua elimu ya Tanzania inashuka je, Serikali haioni tatizo kubwa tulilonalo Watanzania kuhusu suala la elimu? Hawajaona au tunaona sisi tulio pembeni? Naona ni tatizo kubwa wale wanafunzi ambao tunawapeleka shuleni kwa sasa hivi wanakwenda kufuta ujinga sio wanakwenda kusoma, ile sio elimu. Kama mtoto anafika shuleni na hiyo shule ina walimu wawili au mwalimu mmoja, shule haina vifaa, haina maktaba, haina maabara, tunategemea kitu gani? Tunataka walimu wa sayansi, Tanzania hatuna wanasayansi wengi sana, katika *sector* nyingi nyingi hatuna wataalam wa sayansi, tunaendesha shule zetu bila kuwa na maabara, tunategemea kitu gani? Hatuna *laboratory technicians* na kwa sababu hatuna tumeshindwa kuwa na maabara kwenye shule zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna vitabu, wanafunzi wanasoma katika hali ya shida sana tofauti na tulivyosoma sisi. Elimu ya watoto wa Tanzania kwa sasa hivi kwa kweli, kama tungesoma hivyo huko tulikotoka tusingekuwa hapa tulipo sasa hivi, hata Waheshimiwa Mawaziri hapa wanaweza wakakubaliana nami kwamba, wasingekuwa hapa kama wangesoma elimu wanazosoma watoto wetu. Tumesoma tukiwa na walimu

wengi, tukiwa na maabara, tunasoma *theoriticaly* na *practically*. Leo watoto wetu wanasoma *theoritically* peke yake tunategemea kupata wapi wanasayansi? Lakini Serikali inazidi kuona elimu inakwenda chini na vifaa vile havipatikani vya kutosha lakini bado tume-*keep on changing* leo hiki, kesho kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nategemea angalau Tanzania ndani ya miaka 49 ya uhuru tuwe tunajivunia sekta moja kwamba tumeimudu. Leo tunapozungumza hakuna hata sekta moja ambayo Tanzania tunaweza kujivunia, si kilimo, elimu, afya wala kitu chochote hata katika huduma za jamii ni matatizo. Kwa nini tunagusa hapa tunagusa hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata bahati ya kwenda Ghana, Ghana kule ni nchi ya Afrika, hatuwezi kusema ina rasilimali nyingi sana ni wa kawaida, lakini angalau wao wenyewe wanachojivunia wameweza kusambaza umeme kwa zaidi ya asilimia 75 kwa wananchi wao. Wanajivunia sana hicho kwamba, kwa kutumia ziwa letu moja tumeweza kuweka *power* kubwa ya umeme, tumesambaza karibu asilimia 80 kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie Tanzania tuna mabonde mangapi, tuna maziwa mangapi, tuna maporomoko mangapi, tumeshindwa hata kusambaza umeme kwa Watanzania angalau hata kwa asilimia kumi. Ni kwa sababu kwenye vipaumbele tunavyopanga hatuendi kwa malengo ya ku-*achieve* kitu fulani bali tunagusa hapa tunaacha, mwakani tunagusa hapa tunaacha, mwisho wa yote, tunakosa yote, tunabaki hivi hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kwenye mpango sasa wa bajeti unaokuja watuambie vile vipaumbele vya mwaka tulivyokuwa tumepanga vya elimu na afya, kwa kuwa tumebadilisha sasa tumekwenda kwenye kipaumbele cha kilimo, vitu ambavyo havikukamilika kwanza waje na tathmini tuli-*achieve* kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili watuambie pale tulipoachia kumeandaliwa mpango gani? Vinginevyo kwa kweli tutakuwa hatupigi hatua na pia bado ningeomba sana suala la elimu Serikali ione kwamba ndio *foundation,* ndio *base line,* bila kuimarisha elimu kujivuna kwamba tumejenga shule nyingi wakati huduma za elimu hakuna tunajidanganya. Watoto wengi wanaosoma shule za Kata wachache sana tena ambao naweza kusema kuwa ni ma-*genius* ndio wanaoweza kuendelea, wengine wanakuwa ma-*house girl* nyumbani, wako ma-*house girl form four* wanafanya kazi nyumbani kwa watu huwezi kuamini kama katoka *form four*. Kwa sababu alikuwa anakwenda kupoteza muda, *just wastage of time,* anakwenda pale hakuna mwalimu au mwalimu mmoja madarasa manne, atafanya nini mwalimu mmoja, ambao wanasoma masomo tisa atafundisha somo gani Kiswahili, Kiingereza au nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakuwa ni tatizo, kwa hiyo ningeshauri sana kwamba Serikali inavyopanga vipaumbele ifanye tathmini, kuwepo malengo kwa nini tumepanga kipaumbele hiki, kwa nini tunabadilisha, vigezo gani tutumie katika kubadilisha kutoka kipaumbele fulani kwenda kipaumbele kingine. Kwa kwenda hivyo angalau itafika

mahali Watanzania tujivunie sekta moja tu ambayo tumeweza kuimudu, hata akija mgeni kutoka nje, tuseme kwamba hiki ndicho tunajivunia. Sasa hivi kweli tunajivunia amani, amani hatuilipii wala hakuna fedha zilizotengwa kwa ajili ya amani, lakini tunataka suala lolote linalohusu jamii ambalo tunajivunia kwamba Serikali imefanya hili ndani ya miaka 49 ya uhuru, Watanzania tunajivunia hili na kila mwananchi mwenyewe aweze kujivuna kwamba angalau Serikali yake imefanya kazi kubwa kwa ajili hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, changu ni hicho kimoja tu, suala la kipaumbele ni la muhimu sana, Serikali isiwe inabadili badili vipaumbele, hatuwezi kupiga hatua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

MHE. AHMED A. SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia kwenye suala zima la mipango ya bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nami vile vile naomba nitoe pole kwa familia ya muasisi wetu wa nchi hii Mheshimiwa Kawawa, Mungu aiweke roho yake mahali pema. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwanza na suala zima la kilimo. Napenda kuishukuru kwanza Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi kwa namna ambavyo imefanya juhudi kubwa sana kwa sasa hivi kuona kwamba kilimo kinakuwa ni kipaumbele cha kwanza kwenye Serikali yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi sana kwa Serikali, lakini moja katika vitu ambavyo nimemsikia Mheshimiwa Waziri wakati anatuletea hotuba yake hii ni kwamba kilimo kwanza kitapewa kipaumbele katika bajeti hii. Vipaumbele vitakuwa ni vitendea kazi na moja katika kazi kubwa ambayo Serikali ina mpango mkubwa ni kuhusu benki hii ya *TIB* kwa maana kwamba dirisha sasa kwa ajili ya wakulima liko wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuzungumza na kupanga na kwa suala zima la wakulima si jambo rahisi kuwa na Benki Dar es Salaam na mkulima akawa kwenye Kata ya Solwa au Kata ya Mwakitolyo aweze kwenda Dar es Salaam a-*process process* zake amalize arudi kule ili apate mkopo. Hilo ni jambo la kwanza, ni jambo zito na ni jambo kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kwamba hawa wakulima tumewaandaaje? Kwanza niunge hoja ya Mheshimiwa Mpina alivyosema kwamba tunapotaka kuwasaidia wakulima kwa mikopo tunaandaa Benki lakini wenyewe tumewaandaa namna gani ili wawe na sifa ya kuchukua mikopo kwenye Benki hizo au hata kwenye huu mfuko wa pembejeo, hakuna! Katika Jimbo la Solwa, pale Kata ya Solwa kulikuwa na *SACCOS* na wakulima wame-*apply* kupitia Halmashauri, *powertiller* tano na Kata nyingine lakini mpaka sasa hivi hakuna. Kwa hiyo, kuongea hapa na kupanga ni wazuri sana lakini tunapokwenda kwenye utekelezaji ni ngumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ifanye juhudi za juu sana hasa Wizara ya Fedha iondoe hii 700,000 kwa kila kijiji ambacho kinataka kupima ili kipate *certificate* maana mkulima hawezi kupata hati ya kimila ili awe na sifa ya kupata mkopo mpaka kile kijiji kiwe na *certificate*, sasa tayari umeshaweka 700,000, kijiji kinaona uzito mno kufanya hivyo. Kwa nini Serikali isichangie kwa kutoa ruzuku ili vijiji vyote wapimiwe kwa mara moja ili vijiji vyote vipate *certificate* ili sasa mkulima mmoja mmoja mwenye uwezo aweze kupata hati ya mila.

Mheshimiwa Mwemyekiti, ushauri wa pili, kwa kuwa mkulima yuko mbali ni kwa nini sasa Serikali baada ya kuwa mkulima yule imeshamuandaa impe hati za mila ishirikishe Halmashauri kama ni *agent* wa benki ya wakulima kwamba Halmashauri pale ndiyo inawaelewa wakulima wazuri *process* zote za mikopo ziwe zinapitia kwa Afisa Kilimo, Mkurugenzi anasaini pale, Kamati kama ni Baraza linapitisha na zile *documents* zinakuja huku mkulima anapata mkopo kwa urahisi lakini bila kumuandaa mkulima tutabaki kuongea usiku na mchana na hakuna *achievement* yoyote kwa suala zima la kilimo maana sasa hivi wakulima wengi wanalima ama kwa mkono, *power tiller* na kadhalika lakini tukitaka kupiga hatua, hatua iliyofikiwa na Serikali ni nzuri lakini naomba tupige hatua ya pili ambayo ni kuwaandaa wakulima ili wawe na sifa nzuri za kupata mkopo, benki za wakulima zitoe mikopo, tutapiga hatua sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee Elimu. Ni kweli Mkoa wa Shinyanga kidogo tumeshuka, lakini kwa utafiti wa hapa na pale tuliofanya sisi wenyewe ni kwamba moja katika sababu kubwa ni kwamba maeneo mengi ya Mkoa wa Shinyanga ni vijijini. Sasa tunapopata Walimu kuja katika Mkoa wa Shinyanga 50% wanakuja na 50% wanakimbia. Kwa hiyo, uhaba wa upungufu wa Walimu bado ni mkubwa sana sasa tunafanyaje kujaza nafasi hizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Wizara au Serikali hususan kwa Mkoa wa Shinyanga na Mikoa mingine ya nchi yetu ya Tanzania kuweka fedha za kutosha kujenga nyumba za Walimu ili kuhakikisha kwamba nyumba za Walimu *at least* kwa 70% kwa mwaka huu wa fedha zinapatikana kwenye Mkoa wa Shinyanga na Mikoa mingine yenye matatizo kama Mkoa wa Shinyanga maana tunaletewa Walimu, wewe unamtoa Mwalimu kutoka Kinondoni amezoea kujirusha unamleta Mwakitolyo ataweza kweli? Si rahisi! Au unamtoa Arusha au Mwanza unamleta Lebokando, hata mimi nitatoka tu, nimezoea kujirusha unakwenda pale unakuta mazingira ya vijijini nyumba hakuna, ukitaka kwenda kukodisha nyumba ni hali ngumu sana afadhali hata Walimu wakipangiwa maeneo ya mijini wanaweza wakajikodishia chumba akakaa akafundisha vizuri lakini kwa maeneo ya vijijini naiomba Serikali ifikirie sana nyumba za Walimu kwenye maeneo yetu ya Shinyanga na maeneo yote ya vijijini yenye matatizo kama Mkoa wa Shinyanga kwenye nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye barabara. Ziko barabara ambazo ni za Halmashauri na tumezipendekeza zipandishwe hadhi, hii itasaidia sana kuondoa mzigo kwenye Halmashauri kwenda kwenye Serikali Kuu. Barabara hizi zitakavyokuwa zimepandishwa hadhi na zitakapokuwa zimewekewa bajeti vizuri

zitatusaidia sana kwenye uchumi wa maeneo yote ya Tanzania. Tukiweka fedha za kutosha kwenye barabara zetu za vijijini, tukaweka fedha za kutosha kwenye barabara za *TANROARDS* hii ni hatua moja ya kuchochea uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali sasa hivi ifikirie mapendekezo yote ya barabara za Halmashauri kupanda hadi kuwa barabara za Mkoa. Nafikiri tathmini tayari zilishafanywa kwa Jimbo la Solwa, natoa mfano kwa sababu ni Jimbo ambalo nalielewa, moja katika vigezo vikuu walisema huku kwamba tukipata barabara ambayo inaunganisha Wilaya mbili hiyo tutai-*consider* vizuri sana na sisi tayari tunayo Solwa-Mwakitolya-Kahama tumeipendekeza vizuri sana na barabara hiyo ni barabara kubwa mno inayounganisha Kahama na Solwa kwa maana ya biashara za vijijini na za kilimo kwenye maeneo yote hayo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niiingie sasa katika viwanda. Kilimo kwanza tunamsaidia sana mkulima, anapata mazao ya biashara anauza wapi? Kwa hiyo, bado viwanda vilivyopo Tanzania havitoshi, Shinyanga tuna *export* Pamba *raw material* tu, tuna export hivi hivi tu. Katika Jimbo la Solwa tuna dengu, Tanzania sisi ndiyo tunaongoza kwa dengu, tunauza kwa mabilioni, watu pale wanauza dengu kama *raw material* tu. Sasa tunafanyaje ili wakulima waweze kunufaika na rasilimali zao kwa maana ya kuwa na soko la uhakika. Soko la uhakika ni viwanda vyenyewe na viwanda vyenyewe vinakujaje kule? Ni Serikali yenyewe kuona kwamba inafanya juu chini kuwahamasisha wawekezaji waje Shinyanga na mikoa mingine inayohitaji hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shinyanga hatuna kiwanda cha nguo, ni ajabu! Asilimia sitini ya pamba inatoka kule lakini hatuna kiwanda cha nguo, nani anaweza akaamini hayo? Hakuna! Tuna dengu, tunaongoza Tanzania lakini hatuna viwanda vya dengu. Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri wa Viwanda na Biashara mkitoka nje jamani kuomba tunataka hivi na hivi, tunaomba tuleteeni viwanda katika Mkoa wa Shinyanga, hivi mnashindwa kupata jamani? Kwa hiyo, tunaomba Serikali ifikirie kwamba viwanda ndiyo soko la mazao ya kilimo kwanza, kilimo kwanza viwanda pili. Kama hakuna viwanda ni kweli tutafanikisha katika kilimo kwanza na ni kweli wakulima watapata mazao ya biashara ? Mfano mmoja tu katika hii *financial crisis* iliyotokea juzi angalia wakulima walivyoanguka. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais Kikwete kwa namna ambavyo alichukua hatua za kuokoa uchumi katika Tanzania yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitengo ambacho ni sehemu pekee ambayo inaleta viwanda vya ndani na nje ya nchi ni *TIC* yaani *Tanzania Investment Center*. *TIC* leo kuna mgogoro mkubwa sana baina ya *TIC* na *TRA*, kwenye bajeti tuliyoipitisha hapa *TIC* haikushirikishwa katika bajeti nzima ya mwaka huu tuliyoipitisha kwa sababu walitaka kuondoa uwezeshaji kwa maana ya vivutio, wameondoa vile bila kuwajulisha *TIC* wakihofia kwamba wakiwashirikisha wale wata-*complain***.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua hebu tuipende Tanzania na tuwe na *vision* ya kuipenda nchi yetu, unaposamehe msamaha kwa ajili ya kutengeneza makampuni mapya au kwa ajili ya kutengeneza viwanda vipya ule msamaha haupotei, unakuwa *invested* pale *it will be repaid in the future*. Sasa wewe unaondoa misamaha na kwa bahati mbaya sana

wawekezaji wengi walikuwa ni Watanzania walishindwa kufanya utafiti wawekezaji wengi 80% walikuwa ni Watanzania na kwenye sekta ya utalii. Mkurugenzi Ole Naiko yuko Afrika Kusini anafanya kupigiwa simu kwamba Mheshimiwa bwana hapa misamaha ya kodi kwa ajili ya wawekezaji wote mliowapa *certificate* imeondolewa, hajui! Si ni aibu! *TIC* iko chini ya Waziri Mkuu, kwani *TRA* ni Serikali ya nani? Wanakuwa na nguvu gani ya kufanya vitu vya namna hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niingie katika suala la bandari maana muda unakwenda. Bandari yetu kilimo uti wa mgongo, Hazina moyo, Bandari mimi nasema ni maini. Bandari yetu hatuitendei haki. Mungu ametupa zawadi jiografia ya Tanzania, nchi nane zinategemea nchi yetu, sasa hivi Mheshimiwa Mbunge amekuwa akiongelea hapa kwamba Kenya sasa inatupiku hivi wao wana akili gani kuliko sisi? Bandari yetu tunaichafua hovyo hovyo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kuchangia nikasema, upo umuhimu sasa bandari yetu ikawa kwenye mfumo au muundo wa Wizara kamili. Kuna bandari ya Tanga, Dar es Salaam, Mtwara, Kigoma na nyingine nyingi, bandari ndiyo nchi, nchi kama Singapore ina Wizara ya Bandari, Dubai ina Wizara ya Bandari, kwa nini sisi bandari zote hizi tena wale wana bandari mojamoja tu, sisi Mungu ametupa bandari zaidi ya saba tunashindwa kuwa na Wizara? Kama ni masuala ya Sheria kwa maana ya kwamba ije hapa Bungeni tuipitishe Makamishna watakuwa ndani ya Wizara ya Bandari wawe na *authority* na maamuzi ya moja kwa moja. Tukiwa na Wizara ya Bandari itatusaidia kuwa na maamuzi ya haraka ya kutoa mizigo, leo hapa tunaongelea kutafuta maeneo ya makontena, tunawapa kazi tu, ile ni dili tu, lakini tukiwa na bandari na mizigo ikatoka haraka hatuhitaji hata maeneo ya kutafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri nimemsikia anasema kwamba wanataka kufikia mahali kontena moja iwe siku mbili, si kweli! Wala sasa hivi si siku tano, kuna ushahidi na ukitaka ushahidi waite hao ma-*clearing agents* waulize, kuna matatizo makubwa sana ya *bureaucracy*. Moja katika matatizo makubwa katika bandari ni *bureaucracy* ambazo hazina ulazima, lengo ni fedha, wafanyabiashara hawana tatizo na kulipa fedha unamsumbua nini? Mtu ana-*lodge* leo tazama historia kesho alipe ushuru keshokutwa atoe Kontena. Lakini kama kuna wafanyabiashara hapa najua wanajua ninachokiongea. Ukiwa mzoefu wa biashara mpaka leo si chini ya siku 14 kontena iko pale, ukiwa siyo mzoefu wa biashara mpaka leo kontena ni siku 30. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari tukiitumia vizuri ile ni *direct income*, ni kubwa sana, mizigo ya Rwanda, Burundi, Malawi na kadhalika wanapokuja hapa wanakuja na dola wanaziacha, hatuhitaji kufanya mambo mengi lakini leo tunaichezea hivi hivi tu, matokeo yake Kenya wanatupiku kwani Kenya wana uwezo gani? Mimi juzi nilikuwa pale Kenya lah!.....

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa kuchangia wa Mheshimiwa Mbunge)

MHE. AHMED A. SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nashukuru sana.

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Ahmed Ally Salum muda umekwisha basi unaweza ukamalizia kwa maandishi.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, nilisema baada ya Mheshimiwa Ahmed nitamwita Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah na Mheshimiwa Ruth B. Msafiri ajiandae.

MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa mwongozo ambao ametupa hapa wa bajeti. Vile vile nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa maelezo mazuri ambayo Serikali ikiyazingatia tunaweza tukafika pahala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshazungumza sana hapa Bungeni, tukija tukikusanya *Hansard* tutakuta maneno yote sasa hivi tunayarudia kwa nini hayatekelezwi? Ndiyo maana naweka alama ya kujiuliza, hakuna jipya tunalolizungumza hapa Bungeni. Tunazungumzia bajeti, tatizo ni kutafuta fedha na fedha zinatafutwa kutokana na rasilimali tulizokuwa nazo, yamezungumzwa hapa nitayarudiarudia ili kwenda kwenye *point*. Tuna Bahari, Ardhi, Maziwa na Mito, hizi ni rasilimali ambazo tumepewa, basi tuzichangamkie ili tupate fedha tukuze uchumi, watu tunao wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukianza na mwananchi mwenyewe tunamwezeshaje? Maana yake hilo ndiyo la msingi, ili huyu Mtanzania aondokane na njaa kutokana na rasilimali hizi tunafanyaje? Tumeweka mipango mizuri sana ya kilimo, sina haja ya kurudia. Lakini kuna tatizo moja, niungane na Mheshimiwa Mbunge aliyemaliza kuzungumzia suala zima la MKURABITA na MKUKUTA, tumeona ndiyo dira nzuri ya kumuondoa huyu Mtanzania aondokane na umaskini. Baada ya mjadala huu tutapitisha hapa Sheria ya kuongeza pesa za shilingi bilioni kumi na tisa kwa ajili ya kilimo. Je, zitakwenda kweli kwa mwananchi huyu mdogo au watachukua Makampuni mengine wanunue mbolea na matrekta kisha pesa zimekwisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba ule utaratibu wa MKUKUTA na MKURABITA tuutumie ili mwananchi yule anufaike na hizi pesa ziende kwake, ardhi ya mwanakijiji ipimwe, tumeshapitisha hapa Sheria kamili kwamba kuna hati za kimila imeshazungumzwa lakini utakuta hatuna wataalam wa kupima haya maeneo, wanasema hakuna bajeti, basi kama hii bajeti iliyotoka ya shilingi bilioni kumi na tisa tutenge fungu ili wataalam wakapime, si lazima tupime kote kwa mara moja, twende kwa *phases*, akishakuwa na hati miliki au ya kimila ana haki ya kwenda benki na kuchukua mkopo, atakwenda *TIB,* atachukua mkopo kwa kuweka *collateral* gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema huyu mkulima Mtanzania tumwezeshe kwanza kwa kumwekea mazingira mazuri ili aweze kunufaika na ardhi yake na yeye ajipatie

kipato. Kuna wale wajasiriamali wadogo wadogo sasa hivi wanachimba dhahabu, shaba na madini mengine, wale pia tuweke utaratibu wa kuwasaidia, leo Serikali imepiga marufuku kusafirisha mchanga wa shaba, sasa unapiga marufuku, haya! Sasa yule alikuwa anapata shilingi 5,000/=, umemkatili kabisa hapati. Sasa kwa nini na wao tusiwawezeshe kwa kuwaletea mitambo midogo midogo, wataalam tunao, waka-*process* ile shaba hapa hapa, wakauza shaba yao hata kama kila siku watatoa kilo moja lakini amepata shaba safi. Kiwanda kama hiki *simple*, ni dola 100,000/=, hivi dola 100,000/= kwa kikundi kikubwa katika maeneo, nichukue mfano wa Kongwa wanachimba shaba lakini sasa *process* yake ni lazima wauze *raw material* na wanaofaidika ni wengine. Tuwapelekeeni mashine ili waweze kunufaika na kile wanachokitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni hilo la mwenyewe Mtanzania maskini tunamwezeshaje ili aweze kunufaika na raslimali ardhi ambayo tumekuwa nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka kulizungumzia ni suala la *Private Public Partnership,* hili ni eneo lingine ambalo nasema kwa makusudi Serikali haitaki kuliendeleza siyo kwa sababu hatuna wataalam wala siyo kwa sababu watu hawaelewi na wala siyo kwa sababu yoyote, hakuna kisingizio kwa nini tunakwama katika suala zima la *Private Public Partnership?* Tukizungumzia ujenzi wa bandari nakumbuka bandari ya Mwambani, Serikali ilisaini *MOU* na kampuni au watu binafsi nafikiri kutoka Kuwait *MOU* ilichukua mwaka mzima, hakuna kilichoendelea na sababu zisijui lakini tunaambiwa urasimu. Hivi hii *definition* ya urasimu ni nini? Tunataka tujue urasimu huu ni kitu gani? Maana yake hatutaki kusikia maneno hayo, tuambieni Serikali nini tatizo la urasimu? Wengine wanasema ni lazima utoe 10% hivi ni kweli? Mradi kama huu ni lazima mtu atoe 10%, siamini! Lipo tatizo hebu tuambieni nini tatizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kenya wamesaini *MOU* na China kwa ajili ya ujenzi wa bandari, sisi ile bandari ya Mwambani nimesoma *Business Times* ya tarehe 22 mpaka 28 Januari, 2010, Bandari ya Tanga Mwambani utekelezaji wake utaanza 2018, *information* hizi zimeandikwa, *reference* ni *Business Times* ya tarehe 22 mpaka 28 itagharimu *68.5 million US Dollars* lakini ni baada ya miaka minane kuanzia sasa, *are we serious*? Bandari ya Mwambani siyo kwa sababu ikijengwa na mipango mizuri kuna *export processing zone* pale na kadhalika lakini package nyingine ni reli ambayo itakwenda mpaka Musoma na itapita *Lake Natron, Lake Natron* pale kuna *deposits* za *soda arsh millions of tones,* Mchina leo yuko tayari kuinunua yote, tunataka nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunataka Serikali ndiyo itafute pesa kujenga Bandari hatutajenga, ni lazima kuwe na *Private Public Partnership*. Mchina leo yuko tayari kuijenga Bandari ya chini, kwa taarifa nilizozipata tunatakiwa sisi *Government of Tanzania* tu-*contribute only 10% which is almost 14 or 15 billion. TPA* peke yake inaweza ika-*contribute 14 billion* siyo lazima zitoke Hazina, sasa jamani nauliza *are we serious*? Hivi tunataka kitu gani ili haya mambo yatekelezwe? Kweli ni urasimu? Kweli ni 10% inayozungumzwa? Siamini kwa sababu sisi wote hapa ni watu wazima, kila mmoja ana fani yake na elimu yake, hakuna kitu ambacho hakieleweki. Sasa hii inanipa tabu kweli kweli sijui tutafika wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna bandari ya *Mtwara natural harbour*, tuna gesi pale. Mheshimiwa Waziri kama utakumbuka wakati wa bajeti yako nilizungumzia gesi iliyokuwepo pale *natural harbour,* siyo lazima Serikali tujenge bandari *Private Public partnership*. Kuna utaratibu wa *build operate on or build on operate and transfer* mambo yamekwisha, tunaingia mikataba mizuri hivi tunakosa kitu gani? Nakosa usingizi nikifikiria haya mambo, wala sisemi kwamba wewe hapo Waziri utaleta maajabu lakini lazima kuna tatizo fulani linakwamisha haya mambo, sielewi ni kitu gani. Nimezungumzia Bandari ya Mtwara, Tanga, Reli ya kwenda mpaka Musoma ambayo nimezungumza hapa na Waheshimiwa Wabunge wamezungumza kwamba tunapakana na nchi nane Rwanda, Burundi, Kenya, Zambia, Malawi, Msumbiji, Uganda na Kongo wataitumia Bandari ya Tanga na hapa kuna Reli ya Kati pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Kenya wametoa pesa za kutosha ku-*renovate* bandari ya Mombasa ili ku-*cope* na mizigo, leo watu wanapeleka mizigo bandari ya Tanga wanakimbia, haya! Kama ni suala la kwamba wanakwepa ushuru hilo nakubali, lakini *is it*? Kwa sababu hawapati mwanya wa kukwepa ushuru, kama ni hilo sawa! Lakini sidhani kama ni tatizo, kwa nini mizigo sasa hivi watu wanahama kutoka Bandari ya Tanga? Labda Kamishna wa Forodha atueleze huyo mtu wake kule anfanya kazi gani? *Why* yame-*drop* sana maingizo ya mapato katika Mkoa wa Tanga na sababu moja kubwa ni Bandari ya Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna suala zima la Mchuchuma na Liganga la kukuza uchumi, tunakubali. Haya yote yataongeza mapato, ndiyo vyanzo vya mapato vipya, lakini kila siku tutatazama bia, sigara au soda, hivi ni vitu gani vya kutazama? Zamani mtoto alikuwa anakunywa soda 200/= lakini sasa hivi hawezi kunywa tena soda ni shilingi 500/= hamudu kwa sababu tumeongeza kodi, lakini hivi kweli hizi ndiyo kodi zitakazotusaidia na ni mpaka lini? Maana yake ukishafika kwenye bajeti tunategemea na watu wanasikiliza, bia itapanda au itashuka? Sigara zitapanda au zitashuka? Soda zitapanda au zitashuka? Lakini ni kitu *very minor thing* katika *budget* ya Serikali.

Sasa nasema kama Kamati ya Fedha na Uchumi ilivyosema, lazima kuwe na Kamati ya *Budget*. Nafikiri na Serikali ina Ofisi ya bajeti na Ofisi ya bajeti lazima iimarishwe na iwe na wataalam wa kutosha ili waweze kuchambua mambo vizuri ili wakikaa na Kamati ya Bunge ya Bajeti twende vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna Wizara ya Fedha na Uchumi, huko nyuma tulikuwa na Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji, ubinafsishaji umekwisha lakini tunataka uwekezaji basi, sasa hiyo Tume ya Mipango basi ishughulikie huu uwekezaji. Halafu nauliza, hivi hii miradi ya *Private Public Partnership* ni nani ambaye ana *last say*? *Is it the President? Is it the Minister?* Ni nani? Kwa nini inakwama? Hapo ndiyo najiuliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda Uganda na Rwanda, wenzetu wakienda kwa Rais pale Ikulu anaitwa na Waziri na wataalam, kusema huyu kama anataka ekari 2000 basi mpeni ekari 2000, halafu mwonyesheni kuna ardhi nzuri na nataka majibu baada ya siku tatu. Kule kwa Kagame usipofanya hivyo anakuweka ndani au

anakufukuza Uwaziri, sisi kweli tuna siasa nyingi lakini mambo ya utekelezaji yanaturudisha nyuma vibaya sana. Hatuwezi kila siku tukawa tunapiga kelele juu ya Walimu, madawa, Zahanati na kadhalika wakati *resources* za kuleta au kuibua fedha na uchumi zipo za kutosha. Tunazungumzia kuagiza mbolea, gesi tunayo pale, kwa nini hatujengi kiwanda? Serikali nayo kwa nini hai-*take off*? Kwa nini ile gesi iliyopo pale hatuiuzi? Sina majibu, Serikali mtatufanya sisi tuzungumze, tupandishe *pressure* hapa za bure, tunaona uchungu wa nchi hii, watu wanaitwa maskini wala hakuna sababu ya kuwa maskini, mipango yetu ni mizuri katika makaratasi, mpaka leo *Stiggler's George* imekuwa ni historia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mipango ya kuweka mitambo ya umeme pale Mtwara 400 *megawatts*, leo Mchuchuma na Liganga uki-*take off* umeme utapatikana wapi? kiwanda kile peke yake tunahitaji 400 *megawatts*, sasa haya mambo yote barabara, shule, Walimu, Zahanati na kadhalika tukiyaibua haya *we have the solution* lakini sasa tunang'ang'ania tupige kelele hapa kila siku ya kuomba Walimu na nyumba za Walimu, madarasa na kadhalika, tunatakiwa sasa hivi watoto wetu wasome bure kuanzia darasa la kwanza mpaka chuo kikuu, uwezo huo upo Tanzania. Mpaka leo tunaagiza watu wa kuhudumia mahoteli wanatoka Kenya jirani tu wanatushinda, Uganda na Rwanda wanatushinda wakati sisi ndio tumewasaidia kule katika masuala ya ukombozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na hayo ya kusema ni matumaini yangu Serikali *please do something!* Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia jioni ya leo, inavyoonesha mimi ndiye leo nitafunga dimba la wachangiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Serikali yetu kwa ujumla kwamba imeweza kutuletea mwongozo wa bajeti kwamba tuweze kutoa mawazo yetu, tuishauri kuhusu mapendekezo ambayo wamekuja nayo kwa mwaka wa fedha unaofuata. Sasa na mimi katika hilo naomba basi niwaombe wajitahidi kwa kadri inavyowezekana kufuata ushauri tutakaowapa isije,kuwa kukaa kwetu jana, leo na kesho kukawa ni bure, yale yale yalitokea katika mawasilisho yao basi yakawa ni yale yale yanayotokea katika bajeti. Nitajisikia vizuri kweli kama nitaona tunayowashauri watayafuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niungane na wenzangu katika hoja hii niseme kwamba, nafikiri ili bajeti yetu iweze kwenda vizuri, Serikali ituletee kitu ambacho ni kizuri, kitajadilika kwa umakini na nafikiri kwamba tujikite katika kuona kwamba nchi yetu inajiinua vipi kiuchumi. Lakini tunapolenga kwenda kuiinua nchi yetu kiuchumi, vilevile tuone mwananchi wa Tanzania anainuliwa vipi kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo basi tuwea na mambo ambayo yanamlenga moja kwa moja mwananchi ambayo hayo ndiyo yanayokuja na yakapelekea kuinua nchi kwa ujumla. Kwa mfano, tuna mambo mengine ambayo tunayaona ni kama

mambo madogo lakini ni mambo ya msingi sana katika kuinua uchumi wa nchi na pia ni mambo ya msingi sana katika kuinua uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano suala zima la muda, tunapoteza muda mwingi sana katika kusafiri ambao hauonekani kama ni mali, lakini ukihesabu muda ambao Mtanzania anapoteza kwa mwaka mmoja na kwa miaka thelathini mpaka thelathini na tano (30-35) anayofanyakazi, utagundua kwamba, tunapoteza rasilimali kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna vyombo vyetu vinavyotusaidia katika uzalishaji. Kwa mfano, tuna riba za benki, hizi riba za benki ni kikwazo kikubwa na hatuwezi kuinua uchumi wa Mtanzania, riba ziko juu sana. Sasa hili lingeangaliwa riba za benki zetu zikawa zile ambazo zinalenga kumwinua Mtanzania, siyo tu walenge kupata faida kubwa na kuondoka, hapana, pia walenge kuhakikisha kwamba riba zinamwezesha Mtanzania kubaki na kitu ambacho kitamwezesha kumwinua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna vitu vingine ambavyo ni lazima viangaliwe, kama vile nishati. Sijaona ni kwanini Wizara ya Nishati, nimesoma kwenye gazeti kwamba, wanaweza kuongeza wateja wapya kwa kila mwaka, nafikiri kiwango hiki ni kidogo sana kwa kulinganisha na mahitaji ya Watanzania na mahitaji yetu. Kwa hiyo suala zima la nishati si suala la kuangalia upande mmoja tu, mbona nishati ina maeneo mengi; kuna jua, kuna maji, kuna mafuta, kuna gesi, kwa kweli ziko njia nyingi ambazo zinawezesha kuhakikisha kwamba, nishati inawafikia Watanzania wengi. Nishati inasaidia kuinua uchumi wa mtu mmoja mmoja na hata kuinua uchumi wa Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la maji. Watanzania kama hawana maji ni kikwazo pia katika kujitafutia maendeleo yao. Lakini kuna lingine la ujambazi; ujambazi umegeuka kuwa ni tatizo. Watu hawasafiri toka eneo moja hadi jingine kwa sababu ya hofu ya ujambazi na hili limeambatana sasa hivi na tatizo la ajali za barabarani. Sasa hivi hakuna mtu ambaye ana hakika ya kufanya safari na akafika salama kwa sababu ajali za barabarani wakati wote zinaweza zikajitokeza, mtu au watu wengi wakapoteza maisha na mali. Hivi ni vitu ambavyo ni vidogo vidogo lakini ni muhimu sana katika kusema tunapokwenda kutoa vipaumbele vyetu, ni lazima tulenge Taifa, tuliinue kiuchumi ikiwa namba moja na pia tumwinue mwananchi katika suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa tunawezaje katika mambo haya; ndipo ninapokuja hapo kuongelea vipaumbele, niseme huo ulikuwa ni utangulizi wangu. Vipaumbele vyetu ni lazima vilenge kuhakikisha kwamba, tunakua makini. Lakini hatuwezi kuwa na kipaumbele mwaka huu wa fedha tukaamini kwamba, mwaka unaofuata tumekikamilisha tuhamie kingine. Kwanza hatujafanya tathmini, tulizonazo ni hizi za ujumla ambazo tunazipata kwa ujumla lakini tumefanikiwa sehemu moja, kuna sehemu pia ambayo kutokana na mafanikio hayo imejitokeza, sasa ni changamoto, hatuwezi kuacha changamoto hizi tukarukia kitu kingine, tutakuwa hatujafanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo basi, napenda niishauri Serikali kwamba, kipaumbele cha kwanza kiendelee kuwa ni elimu, tumefanikiwa sana upande wa elimu tangu Shule za Msingi, Sekondari hata na Vyuo tunaendelea vizuri. Kila eneo tuna takwimu za kuongezeka, lakini sasa wakati ambapo tumeweza kujenga shule, tumeweza kuzisajili, tuna watoto wengi wanasoma, lakini tuna changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hizi katika upande wa elimu hatujafanikiwa kuwezesha kupatikana kwa walimu wa kutosha katika shule zetu na hatuwezi kusema tutaajiri walimu bila malipo. Wizara ya elimu itapata wapi pesa kama tumeipa elimu kipaumbele cha tatu au cha nne? Lazima tuhakikishe kuwa tunawapa pesa za kutosha ili watoto wetu wapate kufundishwa sawasawa na walimu walioelimika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilisikia mpango wa kuwachukua waliosoma *Diploma* ili wakawe walimu wa Sekondari, hivi watakwenda wapi na tutawalipa nini? Maana yake lazima pia wanataka mishahara, lakini kingine ambapo pia tunatakiwa tukisimamie hatuwezi kuwa na walimu ambao kila siku wana madai yasiyolipwa, tufike mahali tuhakikishe kwamba, madai ya mwalimu yanapotokea sasa hivi tuna Maafisa Elimu Wilayani yamalizike mara moja, tusiendelee tena kukerwa na haya madai ambayo kila siku yanamfanya mwalimu afuatilie madai badala ya kukaa darasani kufundisha, hii ni changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile hatuwezi kusema tumefanikiwa sana katika elimu wakati bado tuna tatizo la vitabu, watoto wetu hawana vitabu vya kujifunzia, ndiyo kwanza jana Waziri katoka kuzungumza kwamba, sasa kuwe na vitabu vinavyofanana nchi nzima, lakini vitabu hivyo sasa hivi vipo? Je vitakapokuwa tayari vitakwenda kwa maneno? Ni lazima vipelekwe na Serikali kwa pesa, sasa hivi ni vitu ambavyo ni lazima tuviangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna kitu kingine kinakabili watoto wetu, tena kinakabili hawa ambao ndiyo viongozi wa kesho; njaa mashuleni. Watoto wetu wanasoma bila kula, hivi ni kwanini Serikali haiwezi ikakubali angalau kusaidiana na mzazi ikachangia mlo mmoja kwa mwanafunzi? Huyu mtoto wa shule yangu ya Kata anayetembea kilomita karibu kumi na sita kila siku kwenda na kurudi, hawezi kurudi nyumbani kula, akija kurudi jioni tayari anakuwa amekwishaathirika kiafya. Kwanini tunataka kufundisha watoto ambao kesho pia ni wagonjwa? Mimi ninao watoto ambao wamehitimu *form four* lakini tayari wana vidonda vya tumbo, lakini wakati wanakwenda pale *form one* walikuwa wazima, kwa sababu tumejenga shule moja kwenye Kata nzima tukitafuta *catchment's area* kwa hiyo tumewachukua watoto kutoka katika vijiji tumewaweka kwenye *center* moja, lakini hawali shuleni, hiki ni kitu ambacho ni lazima tuongeze pesa kwenye elimu ili watoto wetu wapate elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiendelea hapo, hawa walimu wanakaa mbali na kwenye mazingira magumu, lazima tuhakikishe kwamba, pale shuleni kuna nyumba za walimu, tena zilizo bora. Umeme lisiendelee kuwa ni ombi, pale ambapo umeme wa gridi hauwezi kufika ni lazima tupeleke jenereta, lazima tupeleke umeme wa *solar* kusudi tuhakikishe kwamba, mazingira ya mwalimu huyu unayempeleka akafundishe Sekondari,

amehitimu *degree*, amesomea *university* yenye umeme leo unamwambia akafundishe shule ambayo hakuna umeme, hii haikubaliki. Kwa hiyo, haya ni mambo ambayo ni lazima tuya-*improve* kwa kuhakikisha kwamba, tunaongeza pesa katika elimu ikiwa ni kipaumbele cha kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mengi lakini naamini kwamba, kwa upande huo nimeeleweka. Kingine cha pili ambacho kama Taifa ni lazima lijikite katika kuinua uchumi ni miundombinu. Sasa hivi Serikali yetu inatoa pesa nyingi sana katika ujenzi na ukarabati wa barabara na sasa imeleta kingine tunapopita barabarani, mizani kibao, lakini tazama jinsi barabara zinavyoharibika kwa sababu mizani haisaidii. Tumeongeza mizani lakini hatujapunguza uzito wa magari yanayobeba mizigo barabarani, kuna mizigo haigawanyiki ni lazima iingie kama ilivyo kwenye gari. Kwa hiyo huu mzigo utakuwa unalipa faini ya barabara lakini umeharibu barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachopenda kuiomba Serikali ni kwamba, kipaumbele cha pili kiwekwe kwenye miundombinu ili kusudi tufungue reli ikiwa namba moja, tuweze kusafirisha mizigo yetu kutoka bandarini Dar es Salaam, kwenda Kigoma, kwenda Mwanza na kwa nia nyingine ambazo ni za muhimu, reli ya Tazara, reli ya kwenda Kilimanjaro kama ilivyokuwa zamani kusudi mizigo mizito yote iweze kusafirishwa kwa njia ya reli, lakini reli inasaidiana na bandari, tu-*improve* pale bandarini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenzangu alisema ni mzoefu anamaliza siku 14 kuondoa mzigo bandarini, nimewahi kutoa gari kwa miezi minne bandarini pale, miezi minne sasa katika hali kama hiyo nililipa faini za uwekezaji zaidi ya thamani ya gari mara tatu, sasa hivyo ni vitu ambavyo kwanini tusi-*improve* bandari? Bandari tunazo nyingi Tanzania, tuna bahati kweli nadhani kuliko nchi nyingi za Afrika, lakini ni kwa kiwango gani tunatumia bahati hii? Bandari zote, ya Mtwara, Dar es Salaam, Tanga na kuna uwekezekano wa kuwa na bandari nyingine, tuhakikishe kwamba, tume-*improve* bandari zetu ili kusudi mizigo ikifika itoke haraka watu waende wakazalishe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia hatuwezi kukataa kuimarisha viwanja vya ndege, sasa hivi ulimwengu ni mmoja, hivi sisi Nairobi wanatuzidi nini? Leo ukifika kwenye uwanja wa ndege wa Nairobi unasikia wivu wa maendeleo na kujiuliza kwamba, hivi sisi Tanzania tuna tatizo gani! Kiwanja kimoja tu cha ndege cha Dar es Salaam kimetushinda, kinatia aibu ya kucha, ehe, hata *VIP* si *VIP*, mahali pa wageni wa kawaida si pa wageni wa kawaida, watokao nje hawaeleweki, hivyo ni vitu vya aibu sasa ni lazima uhakikishe kwamba, tuta-*improve* hivyo kwa kuweka kipaumbele cha pili katika viwanja vya ndege, ili ndege kubwa ziweze kutua, watu wanaokuja kuwekeza Tanzania waingie haraka, halafu waweze kuhakikisha kwamba, wanaondoka haraka kwani kwanini mtu aje Tanzania kupoteza muda wake!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni vitu ambavyo ni lazima viangaliwe, hata hayo mahoteli mazuri ambayo tunataka tujenge watu watalala kama wanajua kwamba, watafika na kuondoka Tanzania kwa haraka na ndege ambazo wako *comfortable* nazo. Wafanyabiashara wanataka ndege za *business*, lakini ndege hizo ziko ngapi Tanzania?

Siku hizi tunapanda tu za daraja la *economy*, za *business* zinakuja mara chache sana, hatuwezi kujiinua kiuchumi kama Taifa, hatutaweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile nizungumzie barabara. Tuache kung'ang'ania barabara moja tu, kwa mfano Dar es Salaam ambako tayari kuna *population* kubwa watu ni wengi sana, kila mbinu ifanyike kuhakikisha kwamba, barabara mpya zinatobolewa ili watu watembee haraka, lakini vilevile barabara za juu, hivi tutaendelea kusema, hatuna uwezo mpaka lini, wakati watu wanaendelea kuongezeka mijini. Hakuna njia ni lazima tuwe na barabara zinazopita juu, mtu ambaye halazimiki kuingia katikati ya mji apite moja kwa moja atokee Kibaha, aondoke aende anakokwenda, haya mambo ni lazima tuyaangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini na barabara zingine, hatuna sababu leo ya kutokuwa na barabara inayotoka Dodoma kwenda Kigoma, kwa sababu asiyetaka kupanda ndege au kusafiri kwa kutumia treni basi aende kwa njia ya barabara. Tuna barabara nyingi ambazo zinafahamika kwa wataalam wa nchi hii, jamani tuhakikishe kwamba zimekuwa *cleared*, zitengenezwe ili kusudi Watanzania wasafiri jinsi wanavyoweza kusafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo ambayo nimeyazungumza napenda kusema kwamba, tujitahidi kwa kadri inavyowezekana na naishauri Serikali katika hili, tuunde Kamati ya Bajeti. Kamati hii itasaidiana na Serikali kuweka vipaumbele mapema na pia itasaidiana na Serikali kufanya tathmini kwa sababu tunatoa pesa, tathmini hakuna, sasa kama hakuna tathmini maana yake hata unapotaka kutoa pesa kwa ajili ya mwaka mwingine kwa kweli unakwenda kwa hisia tu, lakini si kitaalam. Sasa huu si wakati tena wa kwenda kihisia tu, siasa za sasa hivi ukitaka kuzisimamia kwa uongo uongo wananchi wakikugundua kuwa wewe ni muongo, aise, watakuadhibu na hutasahau, kwa sababu watu unapowaeleza wanakusikiliza, wakitoka pale wanajadili, wanatafakari hivi kuna ukweli humu? Kama kuna ukweli wamekupata, kwa hiyo hatuna siasa za uongo, tuna siasa za ukweli na kwa hiyo lazima siasa iende kisayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma *political science* sikusoma *political* uongo maana yake lazima siasa ziende na ukweli, si uongo. Kwa hiyo, anayesema kuna *political* uongo huyo hajui asemacho, kuna *political science* maana yake ni lazima uvipime vitu kwa njia ambazo umepewa uangalie matokeo yake, uangalie leo, kesho itakuwa vipi ndiyo *political science* na ndiyo tutaweza kwenda vizuri na mambo yaangaliwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wachumi na wao watuletee bajeti, mwongozo mzuri ambao utakwenda kuishia kwenye bajeti nzuri ya kiuchumi ili tuinue Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, naomba uaminifu. Kama hatusimamii mambo haya kwa uaminifu, uadilifu, kuchapa kazi kwa bidii pasipo kuchoka tutaendelea kuleta wageni waje wafanye kazi za Tanzania na wala tusilalamike. Sisi Watanzania tumejitahidi kidogo kusoma, lakini tuna uaminifu kidogo tunapopewa kazi,

tunapoteza muda mwingi kwenye gumzo na mambo yetu binafsi badala ya kufanya kazi yetu kwa bidii, tunajiangalia nimepata nini badala ya kusema kwamba, nimefanya nini na hata watazamaji wanatuangalia, hivi huyu amefanya miaka kumi amepata nini, unataka nipate nini? Usiniulize nimekufanyia nini, kwa sababu unapotaka kuniuliza nimepata nini, unaniongoza niwe mwizi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa, kengele ya pili!

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona umeinua *microphone* nikafiri labda kengele sikuisikia, basi nakushukuru kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msafiri, ahsante sana. Kwa kweli hiyo dakika ya mwisho ndiyo kasi yako ilikuwa kama treni inakaribia Bukoba kabisa. Waheshimiwa Wabunge, naomba niwashukuru kwa siku hii ya leo na niwapongeze, kwa kweli kila mtu amejitahidi kufuata utaratibu na kuelekea kule tulikokuwa tumekubaliana katika mchango wa leo. Sasa kwa orodha ya wachangiaji niliyokuwa nayo, bado ni ndefu, naomba tu labda niwataje wale ambao wanatakiwa wajiandae kusudi kesho wawe tayari kuanza, tutaanza na Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Mporogomyi atafuatia na Mheshimiwa Dkt. Getrude Mongella yeye atakuwa mchangiaji wa tatu kwa siku ya kesho.

Baada ya kusikiliza michango hii ya leo, hoja hii itaendelea kesho. Sasa naomba niahirishe shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi ndani ya ukumbi huu.

(Saa 1.45 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa, Tarehe 5 Februari, 2010 Saa Tatu Asubuhi)